# NGELI ZA NOMINO

Nomino za Kiswahili zimegawanyika katika makundi mbalimbali. Nomino zinazounda kundi moja huwa na sifa zinazofanana. Wataalamu wa isimu wamezigawa nomino au upatanisho baina ya nomino na maneno mengine katika makundi.Makundi hayo ya nomino huitwa NGELI ZA NOMINO.

A. **<u>DHANA YA NGELI ZA NOMINO</u>**

Neno ngeli limetokana na lugha ya kihaya "engeli" lenye maana ya "aina". Ngeli ni aina au namna ya kuweka  majina katika makundi yanayofanana au yanayowiana.

Nomino za Kiswahili zinaweza kugawanywa katika makundi mbalimbali. Ngeli za nomino kuhusu mgawanyo wa makundi ya majina, kila kundi likiwa na mabadiliko ya aina moja ya viambishi vya umoja na wingi wenye kuleta upatanisho wa kisarufi kwa maana moja katika vitenzi, vivumishi na viwakilishi. Kila ngeli ina kiambishi cha nomino zake ambacho kinatawala viambishi vinavyorejea nomino hiyo katika aina hizo nyingine zinazoandamana nayo.

1. **<u>UAINISHAJI WA NGELI ZA NOMINO KATIKA KISWAHILI SANIFU</u>**

Wataalamu mbalimbali wamekuwa wakitumia misingi tofauti katika kuainisha ngeli za majina. Hata hivyo misingi mikuu ambayo imekuwa ikitumika sana ni mitatu ambayo ni;

1. Msingi wa kutumia jozi ya viambishi vya umoja na wingi
2. Msingi wa kutumia kiambishi cha upatanisho wa kisarufi
3. Msingi wa kutumia kiambishi cha nomino na cha upatanisho wa kisarufi

**1) <u>MSINGI WA KUTUMIA VIAMBISHI VYA UMOJA NA WINGI</u> <u>(Msingi wa kimofolojia/ sarufi mapokeo)</u>**

Uambishaji wake ulikuwa na ngeli 9. Huu ni mtazamo mkongwe zaidi uliofuatwa na wanasarufi mapokeo. Miongoni mwao akiwa; Coal Meinhot, baadae akifuatiwa na Broamfield (1931) na Ashton (1944) ambao waliziambisha nomino kulingana na maumbo ya viambishi vinavyofanana ziliwekwa katika kundi moja na kufanya ngeli moja. Uchambuzi wa majina kutumia kigezo hiki ni kama ifuatayo

I. Ngeli ya 1: M- /MU- /MW- /A

Katika ngeli hii majina yenye sifa zifuatazo yanaingia katika ngeli hii

a) Majina ya viumbe yenye uhai isipokuwa mimea;

- Mzee – Wazee
- Mtoto – Watoto
- Mtu – Watu

- Muuguzi – Wauguzi

b) Majina yanayotokana na vitenzi yanayotaja watu

- Mfugaji – Wafugaji
- Mchezaji – Wachezaji
- Mkulima – Wakulima.

II. Ngeli ya 2: M- /MW- /MI

a) Yanaingia majina ya mimea

- Mti – Miti
- Mchungwa – Michungwa
- Mpapai – Mipapai
- Mwembe – Miembe

b) Yapo majina yanayoingia vitu vinavyoanza na M- /MW-

- Mto – Mito
- Msumari – Misumari
- Mwiko – Miiko
- Msumeno – Misumeno

c) Yanayoingia majina ya matendo yanayoanza na M-

- Mchezo – Michezo
- Mkato – Mikato
- Mtego – Mitego
- Mkeka – Mikeka

III. Ngeli ya 3: KI- /VI-

a) Hapa yanaingia majina ya vitu yanayoanza na KI- (umoja) na wingi VI-

- Kiti – Viti
- Kisu – Visu
- Kikapu – Vikapu
- Kito – Vito

b) Majina ya vitu yanayoanzia na Ch- (umoja) na Vy- (wingi)

- Chakula – Vyakula
- Chuma – Vyuma

- Chungu – Vyungu

c) Majina ya viumbe yanayoambisha Ki- ya kudumisha

- Kitoto – Vitoto
- Kizee – Vizee
- Kisichana – Visichana
- Kivulana – Vivulana

IV. Ngeli ya 4: N- /N-

a) Yanaingia majina ambayo huanza na N- inayofuatiwa na konsonati

-chi-, -d-, -g-, -j-, -z-, -y-

b) Yanaingia majina yanoyaanza na Mb-, Mv-

-Mbuga, mboga, mvua, mvinyo n.k

c) Yanaingia majina ya mkopo

barua, kalamu, taa, meza, redio n.k

Maumbo yote ya majina haya hayabadiliki kwa umoja na wingi

V. Ngeli ya 5: JI- /MA

a) Yanaingia majina yanayoanza na Ji- (umoja) na Ma- (wingi)

- Jiwe – mawe
- Jicho – macho
- Jina – majina
- Jino – meno

b) Yanaingia majina ya sehemu za mwili na sehemu za mti

- Goti – magoti
- Sikio – masikio
- Ini – maini
- Ua – maua
- Jani – majani
- Tawi – matawi

c) Yanaingia majina ya mkopo

- Bwana – mabwana
- Shati – mashati

d) Majina yenye kueleza dhana ya wingi japokuwa hayahesabiki

Mfano; maji, manukato, mate, mafuta, marashi, mavi, maziwa, masizi.

VI. Ngeli ya 6: U- /N-

Yanaingia majina yanyoanza na U- (umoja) na N au Mb- (wingi)

- Uso – nyuso
- Uzi – nyuzi
- Ubao – mbao
- Ulimi – ndimi
- Ukuta – kuta

1. Ngeli ya 7: U- /MA-

Yanaingia majina yanayoanza na U- (umoja) na Ma- (wingi)

- Uasi – maasi
- Ugonjwa – magonjwa
- Uchweo – macheo
- Uelewano – maelewano
- Ununuzi – manunuzi

1. Ngeli ya 8: KU-

Yanaingia majina yale yanayohusu vitenzi (vitenzi jina)

- Cheka – kucheka
- Cheza – kucheza
- Imba – kuimba
- Oga – kuoga

IX. Ngeli ya 9: PA- /MU- /KU-

- Mahali pale – "pahala"
- Mahali mule (mle) – "mwahala"
- Mahali kule – "kwahala"

**MSINGI WA KUTUMIA VIAMBISHI VYA UPATANISHO WA KISARUFI**

Upatanisho wa kisarufi ni utaratibu wa kupatanisha viambishi vya maneno ili kuleta mshikamano wa maneno katika tungo. Upatanisho wa kisarufi katika Kiswahili hujitokeza zaidi kati ya nomino au kiwakilishi na kivumishi na kati ya nomino au kiwakilishi na kitenzi.

Mtazamo huu wa uanishaji ngeli ambao umefuatwa na Nkwera (1978). Taasisi ya elimu (1988) na Kapinga Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili wa kisarufi kati ya nomino na viambishi awali vilivyo katika vitenzi yaani vipatanishi kwa mujibu wa mtazamo huu, ngeli za majina ya kiswahili ni 9 kama ifuatavyo

| **NAMBA** | **VIAMBISHI AWALI VIPATANISHI** | **MFANO** |
|---|---|---|
| 1. YU – A – WA | YU – A – (Umoja)<br>WA – (wingi) | • Mtu anakuja<br>• Watu wanakuja |
| 2. U – I | U – (Umoja)<br>I – (Wingi) | • Mti umeanguka – miti imeanguka<br>• Mto umefurika – mito imefurika<br>• Mguu unauma – miguu inauma |
| 3. LI – YA | LI – (Umoja)<br>YA – (Wingi) | • Jicho linaauma – macho yanauma<br>• Panga linakata – mapanga yanakata |
| 4. KI – VI | KI – (umoja)<br>VI – (Wingi) | • Kisu kinakata – visu vinakata<br>• Chakula kimechacha – vyakula vimechacha |
| 5. I – ZI | I – (Umoja)<br>ZI – (Wingi) | • Kalamu imekatika - kalamu zimekatika<br>• Nyumba imeanguka - nyumba zimeanguka |

| | | |
|---|---|---|
| 6. U – ZI<br><br><br><br>7. U – YA | U – (Umoja)<br>ZI – (Wingi)<br><br><br>U- (Umoja)<br>YA – (Wingi) | • Ufa unazibwa – nyufa zinazibwa<br>• Ukuta umejengwa – kuta zimejengwa<br><br><br>• Ugonjwa umeenea – magonjwa yameenea |
| 8. KU | KU – (Umoja) | • Kuimba kunafaa<br>• Kucheza kunachosha |
| 9. PA – MU – KU | PA –<br>MU –<br>KU – | • Mahali pale panafaa<br>• Mahali mule mnafaa<br>• Mahali kule kunafaa |

3. **<u>MSINGI WA KUTUMIA KIAMBISHI CHA NOMINO NA KIAMBISHI CHA UPATANISHO WA KISARUFI</u>**

Utaratibu huu wa uanishaji wa ngeli unaozingatia viambishi vyote viwili yaani viambishi vya nomino na viambishi vya upatanishi wa kisarufi kutokana na tatizo/ matatizo yaliyojitokeza katika mtazamo wa kutumia kiambishi cha kisarufi peke yake bila kuhusisha nomino zake za awali. Mfano wa utaratibu huu wa uainishaji ngeli za Kiswahili sanifu ni;

| NAMBA | JINA LA NGELI | MFANO |
|---|---|---|
| | MU – A<br>WA – WA | Muuguzi anasoma<br>Watu wanalima |

| | | |
|---|---|---|
| | M – U | Mti umeanguka |
| | MI – I | Miti imeanguka |
| | JI/Q – LI | Jiwe limeondolewa |
| | | (Q) Panga limenolewa |
| | MA – YA | Majani yamefagiwa |
| | | Mawe yameanguka |
| | KI – KI | Kiti kimevunjika |
| | VI – VI | Viti vimevunjika |
| | N/Q – N/Q/J | Nyumba zinapendeza |
| | | (Q)mboga zinapikwa |
| | N/Q – ZI | Nyumba zinapendeza |
| | | (Q) mboga zinapikwa |
| | (L) U - (L)U | Ubao umeanguka |
| | M – ZI | Mbao zimeanguka |
| | KA – KA | Kavulana kamekuja |
| | U – U | Ugonjwa umeingia |
| | KU – KU | Kuimba kumeendelea |
| | MA – MA | Mahali mnapotoa |
| | MA – KU | Mahali kunakofaa |

**<u>KASORO/ UDHAIFU/ MATATIZO/ YANAYOJITOKEZA KATIKA UANISHAJI WA NGELI</u>**

1. Wanamapokeo au wataalamu walioainisha ngeli katika misingi ya kuangalia umoja na wingi tatizo lao kuu ni kwamba wamechanganya majina ya viumbe hai na visivyo hai

katika ngeli zao. Mfano katika ngeli ya KI – VI, hapa wamechanganya na kuingiza majina ya vitu vilivyo hai na visivyo na uhai. Mfano; kipepeo, kipofu, kiziwi, kilema. Hii ni kutokana na dhana yao na kuanisha ngeli katika jozi ya umoja na wingi na kuangalia viambishi awali katika nomino.

2. Kuna majina mengine hayana ngeli zake. Tukitazama hasa katika uanishaji wa 1 na 2, mfano majina ya vimiminika kama vile maji, maziwa, mafuta n.k. Japokuwa wameweza kulitatua hili kwa kuweka maneno/ majina haya katika ngeli ya Ji/Q – Ma; katika sehemu ya vitu visivyohesabika na visivyokuwa na wingi
3. Kuna baadhi ya ngeli huwa zinawakilishwa vilevile. Mfano ngeli ya 9 na 10, vyote vinawakilishwa na kiambishi N ambacho katika mazingira ya kawaida hujulikana kama (ny-) pia ngeli ya 11 na 14 zinawakilishwa na kiambishi U- na ngeli za 15 na 17 zote zinawakilishwa na kiambishi Ku-
4. Kuna baadhi ya majina hayakubali kuwekwa katika makundi ya umoja na wingi. Mfano; sisimizi, nyama, maiti, ndizi, ndama, panzi, simba n.k.
5. Kwa kigezo cha upatanishi wa kisarufi, muainisho huu unaongelea ngeli za nomino lakini hazigusii nomino zenyewe moja kwa moja bali unatumia tu upatanishi wake wa kisarufi
6. Pia kwa upande mmoja ngeli zinahesabiwa katika jozi za umoja na wingi, lakini kwa upande mwingine zimehesabiwa katika ngeli moja moja Mfano; katika ngeli ya 2, 6 na 7 (katika umoja) zote zimewakilishwa na kiambishi Zi- ni wazi kwamba hili ni tatizo
7. Ngeli ya kwanza imepewa viambishi viwili vya YU – na A – , lakini ukweli ni kwamba matumizi ya kiambishi cha YU – ni ya kilahaja zaidi kuliko ya Kiswahili sanifu. Si jambo la kawaida kukuta wasemaji wa Kiswahili sanifu wakisema kitu kama, “mwalimu yu afundisha. Mtoto yu aja, mzee yu azeeka” n.k kwa misingi hiyo basi tunasema kiambishi hiki kisitumike. Hata hivyo pengine ni muhimu kusema katika Kiswahili sanifu matumizi haya ya Yu – hujitokeza katika vivumishi vya maneno yupi, huyu n.k
8. Ukweli ni kwamba ngeli za 16, 17 na 18 ni ngeli za mahali kwa hivyo kiambishi halali katika ngeli zote hizi 3 ni Mu – na wala si Pa – Mu – ku – kama ilivyoelezwa kimapokeo. Tunasema ni Ma – kwa sababu ukiyachunguza maneno mahala, pahali, utaona kwamba katika mifano iliyotolewa katika uanishaji yote yanahusu mahali

---

# MJENGO WA TUNGO

Tungo – Ni neno au maneno yanayotoa taarifa fulani ambayo yanaweza kuwa kamili au yasiwe kamili.

Neno hili tungo ni nomino ambayo hutokana na kitenzi ‘tunga’ ambacho kinamaana ya kushikanisha vitu pamoja kwa kupitisha kitu mfano uzi kwenye sindano.

**Kisintaksia**

Neno tungo humaanisha kupanga pamoja vipashio sahihi ili kujenga vipashio vikubwa zaidi. Katika lugha, tungo ya chini kabisa ni neno ambalo linaundwa na mofimu na tungo ya juu kabisa ni sentensi.

**<u>AINA ZA TUNGO</u>**

Kuna aina kuu 3 za tungo nazo ni;

1. Tungo kirai
2. Tungo kishazi
3. Tungo sentensi

**TUNGO KIRAI (KIKUNDI)**

**KIRAI** – Ni tungo isiyo na muundo wa kiima na kiarifu au ni kipashio cha kimuundo chenye neno moja na kuendelea lakini ambacho hakina muundo wa kiima na kiarifu.

AU

Ni kipashio ambacho sio lazima kiwe na kitenzi

Kwa kawaida kirai ni kikubwa kuliko neno lakini ni kidogo zaidi ya kishazi

Katika kiwango hiki miundo ya tungo huhusisha maneno mawili au zaidi ambayo huwekwa pamoja katika mpangilio maalamu unaozingatia uhusiano uliopo baina ya neno kuu na maneno mengine.

**AINA ZA VIRAI**

- **Kirai Nomino (KN)**

Ni kirai kinachotawaliwa na nomino au mahusiano ya nomino na neno au mafungu ya maneno

Muundo wa Kirai Nomino ni kama ifuatavyo

- Nomino peke yake

Mfano; Baba analima. Juma anasoma

- Nomino mbili au zaidi zinazounganishwa

Mfano; Juma na Ali wanacheza mpira. Kaka na dada wanaenda sokoni

- Nomino na kivumishi (N + V)

Mfano; Mwalimu hodari ameandaa somo. Mtoto mzuri anacheza

- Kivumishii na nomino (V + N)

Mfano; Wale wazee wameondoka

- Kiwakilishi peke yake

Mfano; Mimi ninasoma kitabu. Wewe unaumwa malaria

- Nomino na kitenzi jina

Mfano; Kilimo cha kufa na kupona kimezingatiwa.   Kucheka kwa fisi hakunitishi

- **Kirai Kitenzi (KT)**

Ni kirai ambacho kimekitwa katika kitenzi au katika uhusiano wa kitenzi na neno au mafungu mengine ya maneno. Kirai kitenzi kimeundwa na vipashio vifuatavyo;-

- Kitenzi peke yake (T)

Mfano; analima, anapika

- Kitenzi + jina na kielezi

Mfano; Anamfundisha mtoto vizuri.   Wanasoma kivivu

- Kitenzi kisaidizi kimoja au zaidi na kitenzi kikuu (Ts + Ts + T/Ts + T)

Mfano; Alikuwa analima.   Alikuwa anataka kulala

- Kitenzi kishirikishi + Nomino (shamirisho)

Mfano; Ni mpole.   Ndiye shujaa

- **Kirai Kielezi (KE)**

Miundo yake hailekei kukitwa kwenye mahusiano baina ya neno kuu (kielezi) na neno au fungu la maneno linaloandamana nacho. Badala yake miundo inayohusika hapa ni ya maneno ambayo hufanya kazi pamoja katika lugha.

Mfano; Wanafunzi wanaandika vizuri.   Alitembea polepole sana

Kazi kubwa ya miundo hii katika sentensi ni kueleza wakati, mahali, jinsi na kinachofanya tendo lifanyike. Tofauti na virai vingine ambavyo nafasi yake ndani ya sentensi huwa ni ya kudumu. Virai vielezi huweza kushika nafasi mwanzoni mwa sentensi au baada ya kitenzi.

Mfano; Juma alikuja jana jioni.   Jana jioni, Juma alikuja

- **Kirai Kihisishi (KH)**

Ni kirai ambacho muundo wake umekitwa katika mahusiano baina vihisishi hivi; kwa, na, katika, au na fungu la maneno linaloandamana nalo. Katika kirai kihusishi neno kuu ni kihisishi katika Kiswahili, muundo wa KH ni mmoja tu, nao ni kihisishi na kikundi nomino

Mfano; Kwa amri ya jeshi. Mwizi amekamatwa na polisi. Amekwenda kwa kaka yake

## TUNGO KISHAZI

Kishazi ni tungo yenye kitenzi. Kitenzi hicho kinaweza kuwa kinachojitosheleza na hapo huitwa kishazi huru au kikuu au chaweza kuwa kitenzi kinachojitegemea na hivyo huitwa kishazi tegemezi

AU

Kishazi ni tungo yenye kitenzi ambacho kinaweza kujitosheleza na kukamilisha ujumbe uliokusudiwa na mzungumzaji au kuwa na kitenzi kisichoweza kutegemea kingine

## AINA ZA VISHAZI

Kuna aina mbili za vishazi

(i ) Vishazi huru

(ii) Vishazi tegemezi

**Vishazi huru**

Ni kishazi kinachotawaliwa na kitenzi kikuu ambacho kwa kawaida hutoa ujumbe uliokamilika usiohitaji maelezo zaidi ya kukamilisha maana.

Pia maana kamili yaweza kupatikana hata kama vishazi tegemezi vikifutwa katika sentensi zinazohusika, juu ya hayo vishazi huru vyaweza kuwa kabla au baada ya vishazi tegemezi

Mfano; watoto wazuri wanakimbia

Mama anapika chakula

Asha naye mpumbavu

**Vishazi Tegemezi**

Ni kishazi kinachotawaliwa na kitenzi kisaidizi ambacho kwa tabia yake hakikamilishi ujumbe uliokusudiwa bali hutegemea kitenzi kikuu kuweza kutoa ujumbe uliokusudiwa

Mfano; mzee aliyekuja jana

Mbwa aliyepata kichaa

Nyumbu aliyepigwa risasi

## SIFA ZA VISHAZI TEGEMEZI

- Kishazi tegemezi hakitoi maana kamili ikiwa hakijaambatana na vishazi huru. Mfano; Somo lililoanza asubuhi. Mtoto aliyekuja jana

- Vishazi tegemezi vinaweza kufutwa katika sentensi bila ya kuharibu maana kamili ya sentensi nzima. Mfano; mtoto aliyekuja jana amekwenda sokoni. Katika sentensi hii kishazi tegemezi 'aliyekuja jana' kinaweza kufutwa na kupata sentesi kama; Mtoto amekwenda sokoni

- Vishazi tegemezi aghalabu vinaweza kutambulika kwa kuwa na viambishi rejeshi. Mfano; aliyekuja Jana ameondoka. Kitabu kilichopotea juzi kimeonekana

- Vishazi tegemezi vinaweza kutambulika kwa kuwepo vishazi tegemezi kama vile; kwamba, ingawa, ili, kwasababu, mpaka na vinakitwa hivi kwa ajili ya vihisishi vilivyopo. Mfano; a) Hamisi anasema kwamba watoto wengi wamekuwa wahuni, b) tumeingia shuleni ili tupate elimu.

- Vishazi tegemezi vinaweza kutanguliwa au vikafuatiwa na vishazi huru. Mfano; i) nilimuona Rehema nilipokwenda sokoni, ii) utakuja nyumbani leo, kufuatana na ndugu yako.

## AINA ZA VISHAZI TEGEMEZI

Vishazi tegemezi vinaweza vikawa na tungo kama hizi

1. Tungo zenye viambishi rejeshi vya viwakilishi nafsi au viambishi ngeli vilivyoambatanishwa ndani ya kitenzi au mwisho.

- Anayevunja sheria lazima aadhibiwe haraka
- Kilichopotea sikijui
- Miti iliyoanguka imeibiwa pande hizi

Vishazi kama hivi vilivyoelezwa hapo juu huwa vishazi tegemezi vivumishi (v) kama inavyoonekana kuna vishazi vilivyotumiwa pamoja na jina lake linalovumishwa.

2. Tungo zenye kueleza mahali wakati masharti au kasoro na sababu. Vishazi tegemezi vielezi (E), mfano

- Ninamolala mna kunguni wengi
- Alipoondoka walifika wageni
- Ukija nitakupa hicho kitu
- Japokuwa inanyesha mvua nitatoka nje hivi punde

3. Vishazi vyenye vitenzi vinavyoanza na kiambishi Ku – vilivyoambatana na maneno mengine. Mfano;

- Saidi hataki kununua matunda sokoni
- Kukaa tu, akatokea mjomba wangu
- Kuulizwa tu, wakataka kuondoka

## DHIMA NA HADHI YA VISHAZI

Kishazi huru kina hadhi ya sentensi (sentensi sahihi) lakini kishazi tegemezi hakina hadhi hii. Vishazi tegemezi ambavyo hutegemezwa kwenye vishazi vingine katika tungo ambavyo huwa kwa kawaida ni dhima ya kikundi au neno. Vishazi hivyo huvumisha nomino iliyoko kwenye tungo hiyo. Mfano;

(a) Askari walioenda vitani wamepewa mshahara

(b) Shule iliyofunguliwa kijijini imepata walimu

Vishazi tegemezi vingine hufanya kazi ya vielezi viwapo katika tungo, sawa na vikundi vielezi kutokana na hali hii, vishazii huru navyo huwa pia vimehusishwa hadhi, kwani vimeteremka daraja kutoka kishazi na kuwa sawa na kikundi ambacho kwa kawaida kina hadhi ndogo kuliko kishazi . mfano; (a) Juma alipigwa, alipoiba mahindi. (b) watoto walikimbia alipowaona

**KIKUNDI SENTENSI**

**Sentensi**

Ni kifungu cha maneno  kuanzia neno moja na kuendelea chenye kiima na kiarifu na kinaleta maana kamili. Sentensi ndio kipashio cha juu kabisa katika daraja la vipashio vya lugha

Muundo wa sentensi una sehemu kuu mbili yaani kiima na kiarifu (kikazi/kidhima) ina KN na KT (kimuundo)

**KIIMA** – ni sehemu au nafasi inayokaliwa na nomino au kikundi nomino ambacho kinaweza kujulikana mara nyingi kuwa mtenda

Mfano; Ali/ amewapiga watoto

Yeye/ ananitukana

Mkulima na bwana shamba/ wamelima kwa pamoja

**KIIMA**

Kiima ni sehemu au nafasi katika sentensi inayokaliwa na jina au kikundi jina ambacho huwa na kiambishi awali kipatanishi katika kitenzi kikuu. Mfano; Juma analima

Vipashio vya kiima

Kiima huundwa na;

- Jina (N) mfano; Mtoto/ anacheza mpira
- Jina na jina (N + N); Baba na mama? Wanalima
- Jina + kishazi tegemezi kivumishi (N + V); Kitu kinachompendeza/ ni kuwa na nguo nzuri
- Kivumishi na jina (V + N); Yule mtoto/ ni mzuri
- Kiwakilishi peke yake; Wewe/ huna matatizo
- Kitenzi jina: kilimo cha kufa na kupona/kinaanzishwa nchini. Kuimba na kucheza/ kwako/kunafurahisha. Kuiba/ hakupendezi
- Jina + kivumishi. Watoto wote/ni watundu

**KIARIFU**

Ni sehemu inayokaliwa na maneno yanayoarifu funzo lililofanywa, linalofanywa au litakalofanywa.

**AU**

Ni sehemu au nafasi inayokaliwa na kishirikishi peke yake au kitenzi kikuu kimetumika sambamba na kitenzi kisaidizi kimoja au zaidi.

Mfano; Kaka alikuwa anaumwa

Vipashio vya kiarifu

- Kitenzi kikuu – Haji/ atalima kesho asubuhi. Karama/ anacheza mpira
- Kitenzi au vitenzi visaidizi vinavyoambatana na kitenzi kikuu

Mfano, mtoto/ alikuwa analima kila mara

Wavulana/ walikuwa wamekwisha kula

- Kitenzi kishirikishi na nomino

Juma ni mtoto

Mtoto/ ni mgonjwa

## SHAMIRISHO

Ni sehemu au nafasi inayokaliwa na nomino au kikundi nomino ambacho kinaweza kujulikana kuwa ni mtendwa, mtendewa au kitendwa (a/a)

Mfano; (a) Juma amempiga mtoto,

Mtendwa(sh)

(b) Mwalimu amempa mtoto zawadi

(mtendewa)

(c) Mwalimu amempiga mtoto fimbo (a/a)
(mtendwa)

## CHAGIZO

Ni sehemu au nafasi inayokaliwa na kiulizi au kikundi kielezi. Chagizo huweza kutokea mara baada ya kitenzi kikuu au shamirisho

Mfano; Juma ataondoka kesho

| Mama | anasoma | kitabu | polepole |
|---|---|---|---|
| N | T | Sh | Ch |

## AINA ZA SENTENSI

1. **Sentensi sahili**. Hii ni sentensi ya kishazi huru, kishazi hiko kinaweza kuwa na kifungu kitenzi kimoja, kifungu kitenzi hicho kinaweza kuwa cha kitenzi kikuu, kisaidizi au kishirikishi

Mfano;

- Ali analima shamba

T

- Musa ni mzembe

t

- Mzee alikuwa anataka kwenda kuona mpira

Ts Ts Ts

Sifa za sentensi sahili

- Ina kiima ambacho kimetajwa wazi, kiima hicho huweza kuwa jina, jina na jina au jina na kivumishi
- Ina kiarifu ambacho kimeundwa na kitenzi kikuu kimoja au kitenzi kishirikishi au kitenzi kikuu na kisaidizi pamoja na shamirisho na chagizo
- Haifungani na sentensi nyingine na hivi inajitosheleza kimuundo na kimaana

2. **sentensi changamano**. Hii ni sentensi inayoundwa na kishazi huru kimoja au zaidi na kishazi tegemezi kimoja au zaidi

Mfano; Nyumbu aliyepigwa risasi amekufa

Miundo ya sentensi changamano

- Muundo wenye kishazi tegemezi vumishi
- Mtoto anayeumwa kichwa amepona
- Kisu kilichopotea juzi kimepatikana leo asubuhi
- Muundo wenye kishazi tegemezi kielezi
- Juma alikimbia aliponiona
- Saidi hataki kununua matunda sokoni

3. Sentensi ambatano. Hii ni sentensi ambayo huundwa na sentensi mbili au zaidi ambazo huunganishwa kwa kiunganishi. Miundo ya sentensi ambatano ni;

- Muundo wa sentensi sahili (vishazi huru) viwili au zaidi vilivyoambatanishwa kwa kutumia viunganishi
- Mama analima na baba anapanda
- Yeye anapenda kusoma na mwanawe anapenda kucheza
- Juma ni mrefu lakini saidi ni mfupi

- Sentensi sahili (kishazi huru) pamoja na tungo changamano
- Mtoto aliyekuja jana amekwenda sokoni lakini mama yake anapika jikoni
- Msichana uliyemwona juzi ameondoka na mimi nimefurahi ameondoka salama

- Muundo wenye sentensi changamano mbili zilizounganishwa kwa kiunganishi
- Ng'ombe aliyezaa amepotea na ndama aliyezaliwa amekufa
- Mtoto aliyesimama njiani ni mwanangu lakini yule aliyekaa chini ni mwanafunzi

- Miundo yenye vishazi visivyo unganishwa kwa viunganishi, Vishazi vyote vinavyohusika katika miundo ya aina hii ina virai vitenzi vyenye kiambishi tamati – e na hiki kinaeleza hali ya matibabu au nia ya kutenda jambo. Kila kishazi katika miundo kama hii kikiendelezwa katika muktadha wa sentensi kubwa kinakuwa sentensi inayojitegemea
- Niambie, niondoke
- Mwache, aende tu
- Mfundishe, aelewe

4. Sentensi shurutia. Hii ni sentensi ambayo ina vishazi tegemezi viwili ambavyo hutegemezi wake hutokana na mofimu – nge – ngali – ngeli – ki

- Angejibu maswali angefaulu mtihani
- Juma angelikuja mapema angelimkuta Mussa

## UCHANGANUZI WA SENTENSI

Kuchanganua sentensi ni mbinu ya kuigawa sentensi katika sehemu mbalimbali ambazo huunda sentensi hiyo

### Hatua za uchanganuzi wa sentensi

- Kutaja aina ya sentensi yaani kama ni sentensi sahili, ambatano au changamano.
- Taja sehemu zake kuu yaani; kiima na kiarifu (kishazi) au KN na KT (kimuundo)
- Kama ni sentensi sahili onyesha vipashio vya kiima na kiarifu; yaani jina, vivumishi, vitenzi, shamirisho na chagizo n.k

Kama ni sentensi changamano taja vishazi vyake na kazi ya kila kishazi tegemezi katika hiyo sentensi changamano yaani taja: kama kishazi tegemezi kinavyovumisha jina au KN kilicho katika kiima au KN cha kishazi huru. Mfano; Mzee uliyemwona jana ni baba yangu. "uliyemwona jana" ni kishazi tegemezi kivumishi kinachovumisha jina "mzee" lililo kiima cha kishazi huru (K/H) "mzee ni baba yangu"

- Kutaja aina za maneno yote yaliyomo katika sentensi hiyo. Mfano;

Baba na mama wanakula ugali

N t N T N

- Kuandika tena sentensi


## NJIA YA UCHANGANUZI WA SENTENSI

Kuna njia kuu nne za uchanganuzi wa sentensi

- Matawi/ ngawe/ michoroti
- Jedwali/ visanduku
- Mishale/ mistari
- Sentensi/ maelezo/ maneno


Mfano;

- Mwalimu mwema amemsaidia mwanafunzi




Mwalimu mwema amemsaidia mwanafunzi

- Mbuzi aliyenunuliwa juzi amechinjwa leo asubuhi




Mbuzi aliyenunuliwa juzi amechinjwa leo asubuhi

**<u>VISANDUKU/ JEDWALI</u>**

Mfano;

- Gari lililopinduka jana limeinuliwana dereva wake amefariki dunia

S. ambatano

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| $S_1$ | | | | $S_2$ | |
| K | | A | U | K | A |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | KE | KT | | | | KT KN |
| N | V | E | T | U | N | V | T N |
| Gari | lililopinduka | jana | limeinuliwa | na | dereva | wake | Amefariki dunia |

- Wanafunzi waliimba wimbo wao vizuri sana

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| S. Sahili | | | | |
| K | | A | | |
| KN | KT | KN | | KE |
| N | T | N | V | E |
| Wanafunzi | waliimba | wimbo | wao | Vizuri sana |

**<u>MISHALE/ MISTARI</u>**

Mfano;

- Shangazi anasoma kitabu polepole

S → sahili

S → K + A

K → KN

KN → N

N → shangazi

A → KT + KN + KE

KT → T

T → Anasoma

KN → N

N → Kitabu

KE → E

E → polepole

- Mbwa aliyepata kichaa mwogope

S → Changamano

S → K + A

K → KN

KN → N + V

N → mbwa

V → aliyepata kichaa

A → KT

KT → T

T → mwogope

**<u>MANENO/ MAELEZO</u>**

- Juma anacheza mpira na Damasi anasoma kitabu

Hii ni sentensi ambatano

Sentensi hii ina sentensi mbili na kiunganishi

Sentensi ya kwanza ina kiima na kiarifu

Kiima kina jina

Jina ni juma

Kiarifu kina kitenzi na nomino

Kitenzi ni anacheza

Nomino ni mpira

Kiunganishi ni na

Sentensi ya pili ina kiima na kiarifu

Kiima kina jina

Jina ni Damasi

Kiarifu kina kitenzi na jina

Kitenzi ni anasoma

Jina ni kitabu

- Balozi wetu ni mtu jasiri sana

    Hii ni sentensi sahili

    Sentensi ina kiima na kiarifu

    Kiima kina jina na kivumishi

    Jina ni balozi na kivumishi ni wetu

    Kiarifu kinakitenzi kishirikishi + Kirai nomino

    Kirai kielezi

    Kitenzi kishirikishi ni Ni

    Kirai nomino kina jina na kivumishi

    Jina ni mtu na kivumishi ni sana

---

# MAENDELEO YA KISWAHILI

Kila lugha Ina asili yake. Lugha huwepo ili kukidhi haja ya mahitaji ya kimawasiliano ya jamii inayohusika

Lugha ya asili ya jamii yoyote ile hutupa picha halisi ya shughuli za maisha za jamii hiyo. Mfano shughuli za kazi, sanaa, ufundi, mila na desturi n.k

Ijapokuwa lugha ni kipengele kimojawapo cha utamaduni lakini ndicho chombo muhimu kinachotumika kuwasilisha hisia na fikra za wanajamii

Asili ya lugha ya Kiswahili ni nini?

Kuna nadharia mbalimbali zinazoelezea asili na chimbuko la lugha ya Kiswahili, nazo ni;

- Nadharia ya asili ya Kiswahili ni kongo
- Kiswahili ni pijini au krioli
- Kiswahili ni kiarabu
- Kiswahili ni lugha ya vizalia
- Kiswahili ni kibantu

## **Kiswahili ni kibantu**

Wataalamu wa lugha za Afrika wanatambulisha lugha ya Kiswahili kuwa ni lugha mojawapo ya lugha za kibantu. Kwa msingi huo hapana budi ufafanuzi wa chimbuko na maendeleo yake ufanywe kwa kuzingatia historia ya kuzagaa kwa wabantu kusini mwa jangwa la sahara.

Neno bantu lina maana ya watu katika lugha nyingi za waafrika wanaoishi kusini mwa jangwa la sahara. Lugha za watu wanaoishi katika eneo hili huitwa lugha za kibantu

Kuna mitazamo miwili juu ya nadharia hii. Ushahidi wa kiisimu na ushahidi wa kihistoria

## **USHAHIDI WA KIISIMU**

Huu ni mtazamo unaothibitishwa kwa misingi inayohusu sayansi ya lugha. Unadhihirisha kuwa Kiswahili ni kibantu, katika ushahidi huu wa kiisimu kuna vipengele kadhaa vinavyothibitisha kuwa Kiswahili ni kibantu.

- **Msamiati**

Msamiati wa lugha za kibantu na Kiswahili zina mfanano mkubwa. Msamiati wa msingi ni ule unaohusu mambo ambayo haubadilikibadiliki kutokana na mabadiliko ya utamaduni. Tofauti zinaweza kujitokeza katika matamshi au mabadiliko kidogo ya viambishi vyake lakini sio mzizi. Mfano;

| Kiswahili | Kihaya | Kijita | Kilugulu |
|---|---|---|---|
| Maji | amaizi | amanji | manzi |
| Kichwa | omutwe | omutwa | litwi |
| Macho | amaiso | ameso | sinenge |

- **Muundo**

Muundo wa sentensi za Kiswahili unafanana sana na miundo ya sentensi za kibantu. Muundo wa sentensi za Kiswahili na lugha za kibantu unachukua muundo wa kiima na kiarifu.

| Mfano | Kiima | Kiarifu |
|---|---|---|
| Kiswahili: | Juma | anafuga kuku, mbuzi na ng’ombe |

Kinyaturu: Juma ugufugha nkuku,mburi na ng'ombe

Kihaya: Juma nafuga unkoko ,embuzi, n'ete

Kinyakyusa: Juma ikutima nguku, imbene ni ng'ombe

Katika sentensi hizo hapo juu inaonyesha kuwa kuna mfanano kati ya sentensi ya Kiswahili na kibantu, kwani kiima kina nomino (jina) mtenda na kiarifu ambacho hufafanua tendo linaliofanywa na nomino pamoja na nomino mtendwa

- **Ngeli za majina**

Hapa kuna makubaliano kufuatana na ngeli katika maumbo ya nomino na upatanisho wa kisarufi kati ya lugha ya Kiswahili na lugha za kibantu

- Maumbo ya umoja na wingi .

Majina ya lugha za Kiswahili na lugha za kibantu yana maumbo dhahiri ya umoja na wingi. Mfano;

Kiswahili: mtu – watu

Kijita: omunu – bhanu

Kisukuma: munhu – bhanu

Kihaya: muntu – abantu

- Kigezo cha upatanisho wa kisarufi

Sentensi za lugha ya Kiswahili na kibantu zina upatanisho wa kisarufi kwenye kiambishi awali cha kitenzi na nomino. Mfano;

Kiswahili: mtoto anacheza

Kijita: omwana Kenya

Kisukuma: ng'wana alibina

Kisinza: omwana na nazana

1. Kiambishi awali, kipatanishi cha nafsi (kiima)
2. Kiambishi cha wakati
3. Mzizi/ kiini
4. Kiambishi tamati

- **Mnyambuliko.**
- Mnyambuliko wa vitenzi vya Kiswahili hufanana na ule wa vitenzi vya lugha za kibantu. Mfano;

Kiswahili: Piga – kupigana, pigana, pigika

Kisukuma: Tolaga – itolagi, kivitolaga, tolekaga

Kisinza: tela – mwitele, kwitelya, teleka

Kijita: bhuma – mwibhuna, kwibhuna, bhumika

- Mwanzo wa vitenzi. Vitenzi vyote huanza na kiambishi awali cha nafsi viwe vya lugha za kibantu au Kiswahili. Mfano;

Kiswahili: Ni – nakwenada

Kisukuma: Na – leja

Kisinza: Ni – nzenda

- Mwisho wa vitenzi. Vitenzi vyote vya lugha za kibantu na lugha za Kiswahili huishia na irabu – a. mfano;

Kiswahili: nakul – a

Kihaya: nindy – a

Kisukuma: nalily – a

Kimsingi sababu zote zilizotolewa zinathibitisha kuwa kiswahili asili yake ni hapa hapa Afrika mashariki (kibantu)

## USHAHIDI WA KIHISTORIA

Ushahidi wa kihistoria unathibisha kuwa lugha ya Kiswahili ilizungumzwa pwani ya Afrika mashariki, hata kabla ya ujio wa wageni kama vile waarabu na wazungu.

- **Ushahidi wa Al – Idris**

Yasemekana uzinduzi huu ulifanywa huko sicily yapata mwaka 1100 – 1166 kwenye mahakama ya mfalme Roger II, licha ya kufahamika kuwa Kiswahili kilipata kuandikwa kabla ya 10BK Ali Idris alikuwa wa kwanza kugundua jina la zamani la Zanzibar kuwa ni unguja pia kwenye maelezo yake ameandika majina ya aina ya ndizi mbalimbali ambazo zilipatikana huko kama vile kikombe, sukari na mkono wa tembo

- **Ushahidi wa Ibn Batuta karne ya 14BK**

Huyu ana asili ya kiarabu na alifika miji ya upwa wa Afrika mashariki mwaka 1331 BK. Katika maandishi yake anaongelea miji ya kilwa na Mogadishu na analeza maisha ya huko katika nyakati hizo'

"Basi nilianza safari toka Mogadishu kwenda nchi ya waswahili na mji wa kilwa ambao umo katika nchi ya zenji. Tulifika Mombasa kisiwa kikubwa, mwendo wa siku mbili kutoka nchi ya

waswahili ” Alikuta watu hawajishunghulishi na kilimo ila huagiza nafaka kutoka kwa waswahili alikuta watu hawajishughulishi na kilimo ila huagiza nafaka kutoka kwa washahili .

- **Historia ya kilwa kivinje na kilwa kisiwani**

Kimsingi, habari zinaelezea historia ya Kilwa karne ya 10 – 16 BK na inahusisha na kutaja majina ya utani waliokuwa wanatumia masultani wa kwanza wa kilwa. Ali Ibn Hussein na mwanaye Mohamed Ibn Ali majina hayo ni kama vile “mkoma watu” na “nguo nyingi” n.k Kutokana na habari hizi inawezekana lugha ya Kiswahili ilianza kutumika mnamo karne ya 10 – 16 BK. Na pia baada ya sultani aliyeitwa TaltIbnal Hussein ambaye alipewa jina la utani“hasha hazifiki”

- **Ushahidi wa Marcopolo**

Ni mzungu ambaye alikuwa ana jishughulisha na maswala ya kijografia na alisafiri sehemu mbalimbali duniani. Na katika maandishi yake anasema kwamba Zanzibar ni kisiwa kizuri ambacho kina ukubwa wa mzunguko wa maili 200, watu wanamwabudu Mungu na wana mfalme wao na wanatumia lugha pia hawalipi kodi (ushuru)

Pia inasemekana ameandika kitabu cha kijografia ambacho hakikupatwa kuchapishwa lakini sehemu zake zilipata kutafsiriwa kifaransa na kirusi. Mfano; katika kitabu chake aliandika hivi

“Kisiwa cha maajabu ambacho mji wake mkuu huitwa katika lugha ya kwao Zanzibar – unguja na wakazi wake ijapokuwa ni mchanganyiko kwa sasa, wengi wao ni waislamu, chakula chao kikuu ni ndizi. Kuna aina tano za ndizi nazo ni fili, kundi mwiyani, sukari”

- **Ushahidi wa Al – Masudi (915 BK)**

Katika maandiko yake, al masudi anazungumzia juu ya wakazi wa mwambao ambao walijulikana kwa jina la “wazanji” kwa maana hii neno Zanzibar linatokana na zanjibar yaani pwani ya “zanji” Pia anaendelea kueleza kuwa wazenji walikuwa na watawala wa kilimi ambao waliaminiwa kutawala kwa nguvu za mungu viongozi hawa pia walikuwa wacha mungu.

Inasemekana pia neno wakilimi lina maana ya “wafalme” pia anaendelea usisitiza kuwa wazenji walikuwa na kiongozi wao wakihutubia kwa lugha yao kutokana na neno zenji, kuna uwezekano kuwa kabla ya kuja kwa waarabu Kiswahili kiliitwa “kiazania” au “kizenji” na wageni walipofika pwani.

- **Ushairi wa Kiswahili.**

Tukichunguza maandishi ya fani ya ushairi (tenzi) Kama vile utenzi wa fumolyongo ambao uliandikwa karne ya 13 BK. Kuwepo utenzi huu kunadhihirisha kuwepo kwa lugha ya Kiswahili kabla yahapo na huenda Kiswahili kilianza kutumika tangu karne ya 10 BK

Kwani Kiswahili kilichotumika katika utenzi huu ni aina ya lahaja ambayo ni ya zamani sana, kwahiyo kutokana na hayo tunaanza kudhihirisha kwa Kiswahili ni kibantu.

- **Maandishi ya Morice karne ya 18BK**

Maandishi ya morice yalijitokeza mwaka 1776. Yeye anawagawa wakazi wa afrika mashariki katika makundi matatu "waarabu" "wasuriyama" na "waafrika" anasema kuwa wasuriyama na waafrika walikaa na kuungana kama jumuiya moja wakaoana na kusema lugha moja ya kisuriyana na inawezekana kwamba kisuriyana ndicho Kiswahili cha leo.

- **Utenzi wa tambuka karne ya 18 BK**

Utenzi huu uliandikwa karne ya 18 kuanzia 1700 katika uchunguzi uliofanywa na dokta E.A Alpers huko Gao mji wa Panjiu ligundua barua 14 ambazo zimeandikwa kwa hati na tafsiri iliyotolewa kwa kireno. Huko ushahidi kuwa barua hizi ziliandikwa kati ya mwaka 1711 na 1725 zilitumia lugha ya lahaja ya kimvita.

## KUSAMBAA KWA WABANTU

Inasadikiwa kuwa baadhi ya wabantu walifanya maskani yao ya kudumu kaskazini mwa mto Tana. Kikundi hiki cha wabantu ndicho kinasadikiwa kuwa chimbuko la Kiswahili. Katika mabonde haya wabantu walianzisha makazi yao shupatu na shingwaya.

Mnamo mwaka 500 AD, makazi ya mto tana yalivamiwa na kushambuliwa na kabila la wagala. Uvamizi huu uliwafanya wenyeji wake kukimbia na kusambaa katika sehemu mbalimbali za pwani ya bahari ya hindi. Huko pia walianzasha tena makazi yao katika sehemu mbalimbali kuanzia sehemu za kusini mwa Somali kwa upande wa kaskazini mpaka sehemu za mto pangani kwa uoande wa kusini. Wengine walivuka bahari na kuishi katika visiwa vya pemba, unguja na kimero. Kote walipokwenda wabantu hawa waliendelea kuzungumza lugha zao zenye asili ya kibantu, uzungumzaji wa lugha zao kutokana na athari ya mazingira ya pwani, wakazi wa sehemu mbalimbali walianza kutofautiana katika maumbo ya maneno na matamshi. Tofauti hizi zilisababisha kuzuka kwa lahaja au vilugha vya Kiswahili

**Lahaja** – Ni tofauti zilizomo ndani ya lugha kuu moja ambapo watumiaji wa eneo moja hutofautiana na watumiaji wa eneo jingine

**AU**

Ni mojawapo kati ya lugha ambazo husema kweli huhesabika kama lugha moja isipokuwa zinatofautiana katika baadhi ya vipengele fulani kama vile lafudhi (matamshi), msamiati uliokuwa msingi/ muundo

### Aina za lahaja

- Lahaja za kijamii – ni lahaja ambazo huzuka kutokana na kuwepo kwa matabaka mbalimbali yatokanayo na tofauti za kiuchumi, kimadaraka na kisiasa. Watu wa tabaka moja huwa na lugha yao sio tu kwa ajili ya kutambulisha tabaka lao. Lahaja za kijamii zinaonekana wazi bara la ulaya kwa sababu matabaka yako wazi kabisa

- Lahaja za kijografia – ni lahaja ambazo hutokana na lahaja hiyo kuzungumzwa na watu wanaoishi katika eneo moja lakini wanatengwa na kilima au kisiwa. Lahaja zote za Kiswahili ni lahaja zilizotokana na umbali wa kijografia. Lahaja hizo ni;

a. Kiunguja na kimakunduchi – ni lahaja ambazo zilizungumzwa katika kisiwa cha unguja na viunga vyake

b. Kingozi – lugha hii ilizungumzwa tangu kale huko kisimanyuna kaskazini mwa lamu. Lugha hii ilitokana na watu walioishi sehemu iliyoitwa "ngozi" na watu hao kabila lao liliitwa wangozi pia walitumia lugha hii katika balaa kuu la nchi ya Pate (bungu na serikali ya nchi hiyo).

c. Kihadimu/ kitumbatu – kihadimu ambacho pia huitwa kikae au kimakunduchi kina maneno mengi ya asili ya Kiswahili. Kimsingi kitumbatu na kihadimu kinatofautiana sana na kiunguja lakini kina karibiana sana na kipemba

d. Kingao – kinatumika sehemu za kilwa na kuendelea kusini. Lugha hii imefanana na lugha za makabila yanayoizinguka kilwa.

e. Kimtang'ata – lugha hii inasemwa sehemu za mlima hasa sehemu za Tanga na Pangani na miji iliyopakana nayo. Kimkang'ata kinafanana na kimvita na kyomuu

f. Kiungwana – lugha hii inatumika mashariki mwa Zaire, kiungwana ni mchanganyiko wa lahaja za kienyeji na Kiswahili pamoja na Kifaransa. Chimbuko lake ni baada ya wenyeji wa pwani ya Africa mashariki kuhamia huko kongo/ Zaire

g. Kimrima – ni lahaja inayozungumzwa sehemu za Tanga, Pangani, Dar es salaam, Rufiji na Mafia. Kimrima kinafanana na kimtang'ata, kingao, kivumba na kiunguja kwa kiasi kikubwa

h. Chimbalazi/ chimani – kinazungumzwa sehemu za Pwani ya Somalia, Mogadishu, mahali ambapo lugha hii inazungumzwa sana na miaka na barawa na inafanana kitukuu.

i. Kipemba – kinazungumzwa katika kisiwa cha Pemba pia kipemba kinachanganya maneno ya lugha mbalimbali kama vile kimvita, kitumbatu na kimtang'ata.

j. Kivumba – kinazungumzwa sehemu za kaskazini mwa tanga (Tanzania) na kusini mwa Kenya sehemu za vanga na wasini.

k. Kisiu – lugha hii husemwa kuzunguka mji wa Siu, kisiu ni lugha inayofanana sana na lugha ya kipate na kiamu.

l. Kiamu – lugha hii inazungumzwa katika kisiwa cha amu (Lamu) kiamu kina maneno mengi ya lugha za kibantu

m. Kitukuu (kibajuru/kigunya) – vinazungumzwa kusini mwa Somali na kaskazini mwa Kenya (lamu) hadi kisimanyu. Sehemu hii ndiyo inayoitwa shungwaya na ambapo watu wanaamini kuwa chimbuko la Kiswahili kitukuu kinafanana sana na Kiswahili cha leo.

n. Kipate – lugha hii inasemwa katika kisiwa cha pate. Kisiwa hicho kipo kaskazini mwa pwani ya Kenya, mashariki mwa lamu

o. Kimvita – chimbuko la lugha hii ni kisiwa cha Mombasa, ni lugha iliyo katikati yaani matenga, lugha ya kaskazini kiamu, kisiu, kipate na kadhalika na zile za kisiu, kivumba kipemba kimtang'ata.

p. Kingare, kijomvu na chichifudi – chichifudi husemwa sehemu za kusini mwa gaza kati ya mji wa mkunumiji na ranisi. Kingare huzungumzwa Mombasa sehemu ya bandari ya kilindini na kijimvu kaskazini mwa Mombasa

q. Kimafia – kinazungumzwa Mombasa sehemu ya bandari ya kilindini na kijimvu kaskazini mwa Mombasa

r. Kimafia – kinazungumzwa sehemu za Mafia

Lahaja hizi za Kiswahili zinawezwa kugawanywa katika makundi makuu manne, ambayo ni;

- Lahaja za kusini – hizi ziko visiwa vya pemba, unguja na Komoro na hujumuisha kipemba, kiunguja, kihadimu, kingazija, kitumbatu n.k
- Lahaja za bara – hizi hujumuisha kiungwane na misumo ya wageni kama vile wahindi na wazungu
- Lahaja za kaskazini – hizi ziko mwambao wa Somalia na Kenya. Hizi hujumuisha lahaja ndogondogo kama vile ya kiamu, kisiu, kingozi, kipate, kishale, kitukuu na chumbauzi n.k
- Lahaja za katikati – hizi hujumuisha lahaja za kivumba, kimrima, kijomvu na kimtang'ata

## Chanzo cha lahaja

Lahaja hizi zimetokea kutokana na sababu zifuatazo;-

- Utengano wa kijografia – kuna mambo mbalimbali yanayotokea na kusababisha watu wanaosema lugha moja kutengana kijografia. Wakitengana mawasiliano yao hupungua kuna uwezekano mpana wa watu walioachana kukuza upekee na usemaji kwahiyo msingi wa upekee katika usemaji ni utengano wa kijiografia (mazingira)
- Kupita kwa wakati – wakati pia ni kitu muhimu kinachoweza kusababisha kuzuka kwa lahaja. Kwahiyo upekee wa usemaji hutokea taratibu kadri wakati unavyopita
- Utengano wa kitabaka – kwenye jamii moja huweza kuwa na matabaka mbalimbali na kila tabaka hujitambulisha kwa namna ya pekee japokuwa matabaka hayo yapo katika eneo moja. Sababu za utengano huo waweza kuwa wa kiuchumi, kisiasa, elimu na dini kwa sababu ya muachano huo mawasiliano ya mara kwa mara kujitokea husababisha balaa na upekee wa usemaji kupanuka.

## Mambo yanayosababisha kudhoofika kwa lahaja

- Maendeleo ya njia za usafirishaji – njia za usafirishaji kama vile barabara, meli (mitumbwi), reli n.k husababisha kudhoofika kwa lahaja kwasababu njia hizi huwakutanisha watu pamoja waliotengana kijografia. Matokeo ya kukutana huku ni kusawazisha hata namna ya kuongea
- Kuwepo chini ya utawala au dini moja
- Vyombo vya habari -vyombo hivyo ni kama vile redio, televisheni, magazeti husaidia katika kuunda umoja na upekee miongoni mwa watu. Umoja ni kichocheo cha ukaribiano katika usemaji.

## Matumizi ya lahaja

Lahaja ina dhima (matumizi) mbalimbali katika lugha husika dhima ya lahaja katika lugha ya Kiswahili

- Hukuza lugha – lugha ya Kiswahili hukua kwasababu ya kuchukua baadhi ya misamiati kutoka katika lahaja mbalimbali mfano; kivumba – kawashindi – aliwashinda, sinakuja – minakuja
- Kupamba mazungumzo ya wasemaji – husaidia kupamba mazungumzo ya wazungumzaji husika kwasababu huibua misemo mbalimbali wanayoitumia katika mazungumzo yao ya kila siku
- Kusanifisha lugha – usanifishaji wa lugha unatokana na kuteuliwa kwa lahaja moja kati ya lahaja nyingi. Mfano, kiunguja kiliteuliwa kuwa lahaja ya usanifishaji miongoni mwa lahaja za Kiswahili
- Kuonesha mitindo mbalimbali ya wasemaji mfano – mpemba – kipemba Zaire (kingwana) mfano Batoto bangu bana kula kingwana

## KUKUA NA KUENEA KWA KISWAHILI NCHINI TANZANIA

Wageni walipokuja pwani ya Afrika mashariki waliwakuta wenyeji tayari wana lugha yao ya mawasiliano ambayo ni Kiswahili na pia lugha hiyo ilikuwa inatumika katika shughuli za kibiashara miongoni mwao. Kwahiyo wageni walipofika pwani ya Afrika mashariki hawakuona sababu ya kutumia lugha nyingine zaidi ya Kiswahili katika shughuli zao mbalimbali pia wageni waliofika pwani ya Afrika mashariki, walifika kwa nyakati tofauti tofauti na walifika wageni kama vile waarabu, wareno, wajerumani na waingereza na wageni hawa kuna baadhi walikiendeleza Kiswahili na wengine walikidumaza Kiswahili

## KUKUA NA KUENEA KWA KISWAHILI ENZI ZA WAARABU

Kuenea kwa lugha ni kuongozeka kwa watumiaji. Wageni wa kwanza kuja pwani ya Afrika mashariki ni waarabu na kutokana na kuingiliana na wabantu katika Nyanja mbalimbali Kiswahili kilichukuliana maneno na kuathiriana na lugha ya kiarabu

Sababu zilizochangia kukua kwa Kiswahili enzi za waarabu

- **Biashara** – Waarabu walipowasili katika mwambao wa pwani ya Afrika mashariki walianza kufanya biashara na wabantu. Kutokana na maingiliano hayo Kiswahili kilianza kupanuka na kuongozeka misamiati kwa hiyo bila shaka Kiswahili kilikuwa kutokana na maingiliano hayo. Mfano wa msamiati uliochukuliwa katoka kwa waarabu ni kama vile jahazi, kodi, adesii n.k
- **Utawala** – waarabu pia walitumia Kiswahili katika shughuli mbalimbali za kiutawala. Waarabu walitawala Zanzibar, sehemu za pwani ya bara na pemba kutokana na shughuli za kiutawala kuna maneno ya kiarabu ambayo yameingia kwenye Kiswahili. Mfano; mwinyi, sultani, mtukufu, enzi n.k
- **Dini** – Hali kadhalika walipowasili walianzisha dini yao ya kiislamu kwenye upwa wa Afrika kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Waafrika walifundishwa kuandika na kusoma kwa hati za kiarabu ili waweze kusoma na kuelewa kurani. Hivyo wakajikuta wanaingiza baadhi ya maneno ya kiarabu kwenye lugha ya Kiswahili. Baadhi ya maneno ni kama vile elimu, alasiri, alfajiri n.k
- **Ndoa** – wageni hawa pia walipofika pwani ya Afrika mashariki waliishi kwa miaka mingi na hivyo kuchangamana na wenyeji na baadae waarabu wakaoa wanawake wa kibantu na hata vizazi vyao vilipozaliwa. Walitumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao na pia hata utamaduni wao ulijiegemeza kwenye lugha ya Kiswahili. Hata jamii ya watu wa pwani waliwaita watoto wao

waswahili badala ya maneno kama vile chotara, kwahiyo kutokana na hivyo basi ndoa kati ya waarabu na wabantu ulichangia kwa kiasi kikubwa kukua na kuenea kwa waswahili

## KUKUA NA KUENEA KWA KISWAHILI ENZI ZA UTAWALA WA WAJERUMANI NCHINI TANZANIA

Wajerumani pia walitawala Tanganyika kwa muda wa miaka 30 na walipofika walikuta Kiswahili kimekua sana katika nchi za Afrika mashariki kwahiyo walipofika Tanganyika walitumia lugha ya Kiswahili kama chombo cha mawasiliano katika shughuli zao mbalimbali za utawala na hata kwenye kutolea elimu kwa ajili ya manufaa yao. Pia mfanyakazi yeyote wa kiafrika ili kupata kazi ilimbidi ajue Kiswahili kwa kuongea na kuandika ndipo apate kazi pia ripoti zote za utawala wa kijerumani zilitakiwa kuandikwa kwa Kiswahili. Vilevile wanafunzi waliohitimu walisambazwa sehemu mbalimbali nchini na kwa njia hiyo kiswahili kilikua na kuenea sana halikadhalika mashamba yaliyoanzishwa na wajerumani yalikuwa na wafanyakazi mchanganyiko kutoka sehemu mbalimbali na lugha ya mawasiliano miongoni mwao ilikuwa ni kiswahili kwa hiyo walichukua na baadhi ya msamiati kutoka kwenye kabila zao na kuingiza kwenye Kiswahili na hivyo kuchangia ukuaji wa Kiswahili

### Mbinu zilizotumika kueneza kwa Kiswahili nchini Tanzania wakati wa utawala wa wajerumani

- **Mahakama** – utawala wa kijerumani ulitumia pia lugha ya Kiswahili katika shughuli zake kwa hivyo kazi zote ziliendeshwa kwa lugha ya Kiswahili na pia wafanyakazi na wazee na mahakani walihoji na kutoa hukumu kwa watuhumiwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili na hivyo kuchangia kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili

- **Elimu** – mashuleni pia Kiswahili kilitumika kama lugha ya kufundishia na kijerumani kilifundishwa kama somo la kawaida tu katika shule za msingi. Wajerumani walijenga shule sehemu za tabora, ujiji, kilimatinda, mpwapwa, kasangu mwaka 1905, iringa, mwanza, bukoba, kilosa, tukuyu, na moshi pia vyuo vya kufundishia walimu vilianzishwa huko tabora na bukoba hivyo basi walimu na wanafunzi walijifunza na kukitumia Kiswahili katika shughuli zao za elimu na kusababisha kuenea na kukua kwa Kiswahili

- **Utawala** – wajerumani walipofika nchini walikuta lugha ya Kiswahili imekua na kuenea sana hivyo nao katika utawala na hivyo kuamua kujifunza Kiswahili kabla ya kuja nchini na pia hapa nchini wajerumani walitoa mwongozo kwa viongozi wa nchini kwa kutumia lugha ya Kiswahili na hivyo viongozi wote wa kiafrika mfano akida, jumbe n.k walitakiwa kujifunza lugha ya Kiswahili kwasababu walikuwa wanatumwa sehemu mbalimbali sio nchi walikozaliwa tu hivyo kuchangia kukua na kuenea kwa haraka.

- **Shughuli za kilimo (mashamba)** – wajerumani pia walianzisha mashamba makubwa ya mazao ya biashara na kuwalazimisha watu wafanye kazi kwenye mashamba hayo mfano, mashamba ya katani Tanga, kahama, Kilimanjaro kwahiyo kwenye mashamba hayo kulikuwa na idadi kubwa ya watu kutoka sehemu mbalimbali na lugha yao ilikuwa ni Kiswahili kwahiyo wale waliobahatika kurejea majumbani mwao walisaidia kukieneza Kiswahili kwasababu waliendelea kutumia lugha ya kiswahili.

# UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI ANDISHI

**Uhakiki** – ni kazi au kitendo cha kuchambua na kufafanua kazi ya fasihi, kuweza kupata maadili na ujumbe uliomo katika maandishi ya mwandishi asilia

**Au**

Ni sayansi maalumu ya kuchambua na kuona ubora wa kazi hizo kwa kutumia vipengele vya fani na maudhui na kuangalia uwiano na uhusiano ama kuathiriana kwake

**Au**

Ni kitendo cha kuchambua na kufafanua vipengele vya fani na maudhui katika kazi ya fasihi

**Mhakiki** – ni mtu anayechambua kazi ya fasihi au ni mchambuzi wa maandishi ya kisanaa hasa yale ya kifasihi

### Sifa za mhakiki

- Mhakiki anatakiwa ajue historia na mazingira yaliyomkuza mwandishi.
- Mhakiki anatakiwa kuelewa historia na siasa ya jamii inayohusika. Hii inamuwezesha kujua matatizo ya jamii hiyo.
- Mhakiki anatakiwa asome tahakiki za wahakiki wengine katika uwanja wa fasihi na hata nje ya jamii yake.
- Mhakiki anatakiwa awe anasoma kazi zingine za fasihi sio tu ile anayoifanyia uhakiki, kwani hii itamsaidia zaidi katika uwanja  wa uhakiki.
- Mhakiki asiwe anasifia au kuponda kazi za wasanii kwasababu zake binafsi bali kueleza ukweli wa kazi hiyo.

### Vigezo vya uhakiki

Fasihi hueleza shughuli zinazofanywa katika jamii fulani kuna vigezo vya kupima uhakiki navyo ni;

- Uhalisia wa watu, mazingira na matukio katika jamii. Mhakiki hulinganisha wahusika wa fasihi na watu halisi na kujiuliza kama wahusika wanayotenda yanaendana na watu halisi kwenye hiyo jamii
- Ukweli wa mambo yanayoelezwa. Mhakiki atajiuliza je ni kweli kuwa jambo hilo linafanyika katika jamii inayozungumziwa. Mfano kama anahakiki riwaya, inayohusu ujambazi, atajiuliza je ni kweli kuna ujambazi kwenye jamii hiyo?

### Dhima za mhakiki

- Kuchambua na kufafanua picha za kisanii zilizotumika katika kazi ya fasihi
- Kumshauri mwandishi ili afanye kazi bora zaidi
- Kuchambua na kuweka wazi funzo ambalo linatolewa na kazi ya fashi
- Kumwelekeza msomaji ili apate faida zaidi kuliko yale ambayo angeweza kuyapata bila dira ya mhakiki

- Kuweka na kukuza kiwango cha utunzi na usomaji wa fasihi
- Kuonesha kuwa kwa kila kizuri kuna kizuri zaidi na hakuna kizuri kisicho na kasoro
- Kuhimiza na kushirikisha fikra za uhakiki katika kazi za fasihi
- Kuheshimu na kuthamini kazi za waandishi na kuzifanyia kazi

### Uhakiki wa riwaya, tamthiliya na ushairi

Kazi yoyote ya fasihi lazima iwe na mambo mawili nayo ni fani na maudhui

### MAUDHUI

Ni jumla ya mawazo yote yanayozungumzwa pamoja na mtazamo wa mwandishi juu ya mawazo hayo

**Vipengele vya maudhui**

Dhamira. Ni wazo kuu/ mawazo mbalimbali yanayojitokeza katika kazi ya fasihi. Dhamira hutokana na jamii. Kuna aina mbili za dhamira nazo ni;

- **Dhamira kuu**, ambacho ndicho hasa kiini cha kazi ya fasihi ambayo ndiyo sababu iliyomsukuma mwandishi kuandika kazi hiyo
- **Dhamira ndogondogo** – hizi ni dhamira zinazoambatana nazo katika kukamilisha ujumbe. Mfano; dhamira kuu inaweza ikawa “ujenzi wa jamii mpya” lakini zikiambatana na dhamira nyingine ndogondogo kamavile “nafasi ya mwanamke katika jamii” “malezi” n.kMtazamo – ni hali ya kuyaona mambo katika maisha kwa kuzingatia maisha aliyonayo msanii mwenyewe. Wasanii wana mitazamo ya aina mbili.

**Mitazamo ya kiyakinifu**

Kwa kutumia mtazamo huu msanii hutazama ulimwengu au mazingira yanayomzunguka binadamu kisayansi. Msanii huona ulimwengu kuwa ni kitu kinachobadilika kufuatana na mfumo wa kihistoria. Mtazamo huu humfanya msanii kuutazama ulimwengu kama kitu dhahiri katika uhalisia wake

- Mtazamo wa kidhanifu

Msanii mwenye mtazamo huu huchukulia ulimwengu kama kitu kinachobadilika kulingana na matakwa ya Mungu kwahiyo hata kwenye uchambuzi wake hatachambua vitu kisayansi.

- Msimamo – ni hali ya mwandishi kuamua kufuata au kushikilia jambo fulani. Jambo hili linaweza kuwa halikubaliki na wengi lakini yeye atalishikilia tu. Msimamo ndio unaweza kuwatofautisha wasanii wawili au zaidi wanaotunga kazi za fasihi zilizo na kiini chimbuko moja kwa moja kutokana na hayo tunaweza kugundua msimamo wa msanii kama wa kikasuku.

- Falsafa – ni mchujo wa uelekeo wa mawazo muhimu yajitokezayo kila mara katika kazi mbalimbali za msanii. Hii inamaanisha kuwa siyo rahisi kuamua falsafa ya/za msanii katika kazi yake moja tu.

- Migogoro – ni mivutano au misuguano mbalimbali katika kazi ya fasihi. Katika migogoro tunapata migogoro katika wahusika ama vikundi vya wahusika, familia zao, matabaka n.k migogoro mara zote hujikita katika michuano ya kijamii. Migogoro hii inaweza kuwa ya kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kinafsi.

- Ujumbe na maadili. Ni mafunzo mbalimbali ambayo hupatikana baada ya kusoma kazi za fasihi.

Tamthiliya – ni mchezo wa kuigiza ulioandikwa ili upate kuigizwa jukwaani.

Riwaya – ni hadithi ndefu ya kubuni yenye mawaidha mapana ya kifani na maudhui na ambayo hutumia lugha kwa mtindo wa kinadharia (masimulizi)

**Au**

Ni kisa changamano ambacho huweza kuchambuliwa na kupimwa kwa mapana na marefu kifani na kimaudhui.

Ushairi – ni utanzu unaohusu sanaa inayopambanuliwa kwa mpangilio maalumu wa maneno fasaha. Lugha ya mkato, picha, sitiari ili kueleza wazo kwa muhtasari katika njia inayogusa hisia za watu.

**FANI**

Ni jumla ya mbinu, ufundi, mtindo wa vipengele vingine vinavyotumika kuwasilisha maudhui.

**Au**

Ni ule ufundi wa kisanaa anaoutumia msanii katika kufikisha ujumbe wake kwa jamii inayohusika.

**Vipengele vya fani**

1. **MUUNDO**

Ni mpangilio wa mtiririko wa kazi hiyo kwa upande wa visa na matukio, katika uhakiki tunachunguza jinsi msanii alivyounda na kufuma na kuliunganisha tukio moja na lingine na hata kitendo kimoja na kingine, wazo na wazo, ubeti na ubeti na hata mstari mmoja na mwingine.

Sura mara nyingi hujitokeza kwenye riwaya, maonesho/ onesho na tamthiliya, mistari ya ubeti kwenye shairi mfano ubeti kuwa na mistari;

Mmoja

Miwili

Mitatu

Minne (tarbia)

Mitano (takmisa)

Sita na kuendelea (sabilia)

**Aina za miundo**

- Muundo wa msago – ni muundo wa moja kwa moja ambao tunafuatilia matukio mbalimbali toka la kwanza hadi la mwisho kwa mbinu ya utelezi. Mfano; mhusika huzaliwa, hukua na huolewa na hadi kufa.
- Muundo wa kioo (rejeshi) – ni muundo changamano utumiao mbinu rejeshi ambayo huweza kurudisha ama kumpeleka mbele msomaji wa kazi hiyo ya fasihi.
- Muundo rukia (changamano) – ni muundo ambao visa hurukiana. Katika muundo huu kunakuwa na visa viwili ambavyo hurukiana (urejeshi wa msago) katika kusimuliwa kwako na mwisho visa hivi huungana na kujenga kisa kimoja.

2. **MTINDO**

Ni ile namna ambavyo msanii hutunga kazi hiyo na kuipa sura ambayo kifani na maudhui huanisha kanuni au kawaida zilizofuatwa kama ni zilizopo (za kimapokeo) au ni za kipekee.

**Au**

Ni upangaji wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi kwa njia ambayo hatimaye hutokeza au huonyesha nafsi na labda upekee wa mtungaji wa kazi hiyo.

**Katika mtindo tunaangalia**

- Nafsi alizotumia msanii mfano;

Nafsi ya 1 – mwandishi ndiye msimuliaji wa matukio.

Nafsi ya 2 – watu wawili au zaidi wanajibizana

Nafsi ya 3 – mtu wa tatu anatusimulia mimi na wewe.

- Mbinu ya kutumia tanzu nyingine za fasihi simulizi mfano; nyimbo, vichekesho n.k
- Matumizi ya barua
- Matumizi ya monolojia (maelezo) mara nyingi huwa riwaya (masimulizi)
- Tamthiliya huwa dialojia
- Matumizi ya lugha

Vilevile katika ushairi tunaangalia kama anatumia mtindo unaofuata kanuni za ushairi wa kimapokeo.

Urari wa vina na mizani. Mtindo unaofuata kanuni za ushairi wa kisasa (mapingiti/masivina) usiofuata kanuni za urari wa vina na mizani.Lakini jambo la msingi katika mtindo ni lugha na ndiyo hufuatisha fasihi na sanaa nyingine

3. **WAHUSIKA**

Ni watu ama viumbe waliokusudiwa wawakilishe tabia za watu katika kazi za fasihi

**Aina za wahusika**

- **Wahusika wakuu**

Ni wale ambao wanajitokeza kila mara katika kazi ya fasihi tangu mwanzo hadi mwisho. Maudhui ya kazi ya fasihi huwa yanamzunguka na hata kutolewa na mhusika mkuu zaidi ya wahusika wengine kwa hiyo, mara nyingi mhusika mkuu huwa “midomo ya wasanii” (vipaza sauti vya watungaji)

- **Wahusika wadogo/ wasaidizi**

Hawa hujitokeza hapa na pale katika kazi za fasihi ili kuukamilisha ulimwengu wa kazi hizo. Wakati mwingine wahusika wadogo huweza kusaidia kujenga dhamira fulani, inaweza ikawa ndogo au kuu na pia wahusika hawa wadogo husaidia kumjenga mhusika mkuu kutokana na matendo yao

1. **MATUMIZI YA LUGHA**

Kipengele cha lugha ni muhimu sana kwani ndicho kinachotofautisha fasihi na sanaa zinginezo. Pia lugha ndiyo mzizi wa kazi ya fasihi kwani bila yenyewe kuwepo haiwezekani tuwe na fasihi kwani mwandishi ama mtunzi wa kazi ya fasihi hutumia lugha kuyabainisha mawazo yake katika hiyo kazi na kuyaeleza mambo mbalimbali ya jamii yake kwa njia ya ubunifu na kiusanii.

### Tamathali za semi

Ni maneno, nahau au sentensi ambazo hutumiwa na msanii wa fasihi ili kutia nguvu katika maana na hata sauti katika maandishi ama kusema. Pia hutumiwa ili kupamba kazi ya fasihi na kuongeza utamu wa lugha.

- Tashibiha (mshabaha) – ni tamathali ambayo watu au vitu viwili hulinganishwa na watu au vitu vingine kwa kutumia viunganishi . mfano kama, mithili ya, kwamba, sawa na n.k

Mfano: Bwana Musa ni mweusi kama mkaa

Chedi na Aisha wanao uzuri sawa na malaika

- Sitiari – ni tamathali inayolinganisha vitu ama watu wawili bila kutumia viunganishi.

Mfano: Nywele za Rubanza ni kichaka

Maisha ni moshi

Penzi upepo

- Tashihisi – ni tamathali ambazo huvipa vitu uwezo wa kutenda kama binadamu

Mfano: Baridi kali ilimkaribisha

Usiku ulikumbatia ulimwengu kwa kumbato la kutisha la giza nene na kimya kingi

- Taashira – tamathali iliyo na jina la sehemu ya kitu kimoja kidogo kinacho husiana na kingine kikubwa hutumiwa kuwakilisha kitu kamili

Mfano: Kanzu – yaweza kutumiwa kumaanisha shekhe

Jembe – mkulima

Mvi – mzee

Kalamu – mwanafunzi

Kiti – uongozi fulani

- Takriri – ni kurudia rudia kwa neno, sentensi au semi ambayo nia yake ni kusisitiza

Mfano: dunia ni ngumu, jamani ni ngumu

Nitakufa, usiponiona nitakufa

- Msisitizo bayana – tamathali hii husisitiza maana ya sentensi kutumia kinyume

Mfano : Alikuwa msichana mzuri, ukimwangalia kwa mbali huwezi kujua kama anakuja au anakwenda

Mwandiko wako si mbaya, ni mzuri

- Tashtiti – ni usemi ambao swali linaulizwa huku jibu lake linafahamika waziwazi kwahiyo swali hili huweza kuwa kwa ajili ya msisitizo tu au wakati mwingine mshangao

Mfano: Mtu akapoteana na rafiki yake kwa muda mrefu halafu ghafla wakakutana huweza kuulizana “aisee, ni wewe?” japokuwa anajua kuwa ni yeye

- Tanakali sauti – ni maneno au nomino zinazoundwa katika sentensi kutokana na sauti zinazofanana na kuiga sauti za milio mbalimbali

Mfano: Alitumbukia mtoni “chubwi”

- Tafsida – hujitokeza kwa utumizi wa neno, maneno na nahau ambavyo hupunguza ukali wa maneno

Mfano: “Kujifungua” badala ya kuzaa

“Kuaga dunia” badala ya kufa

- Mubalagha au udamisi – tamathali hii hutia chumvi kuhusu uwezo wa viumbe, tabia zao na kuhusu sifa zao kwa madhumuni ya kuchekesha au kusisitiza

Mfano: Tulimlilia Nkurumah hadi kukawa na bahari ya machozi

- Mdokezo – ni kipengele cha kitamathali ambacho msomaji au mwandishi hukatiza maneno au kuacha kitu fulani bila kukitaja, maneno ambayo kwa kawaida ni wazi na huweza kujazwa kwa ubunifu

Mfano: "Sasa basi kuhusu hawa makaburu wa Afrika ya kusini… Ah" Methali pia huweza kugeuzwa pia kwa mdokezo iwapo anayesimulia ataisema na kumwachia msikilizaji amalizie na ajipatie maana iliyokusudiwa.

- Kejeli au kinaya – Hii ni tamathali ambayo maneno yake huwa kinyume kabisa na maana inayotakiwa kutolewa.

Mfano: Mtu anaweza kuwa bepari mkubwa mwenye ubinafsi mwingi kwa kutaka kumkejeli mtu huyo mtu mwingine huweza kumwambia "Kivuli wewe ni mkubwa mpenda mapinduzi na rafiki wa kweli wa wakulima na wafanyakazi"

- Ritifaa – Hii ni tamathali ambayo mtu huzungumza na kitu au mtu ambaye humsikiliza katika fikra tu

- Taswira – Ni lugha inayochora picha ya vitu au mahali kwa kutumia ishara

**<u>ISHARA</u>** – Ni dhana au mawazo mbalimbali yanayotumiwa na wanafasihi mbalimbali katika kazi zao za fasihi kuwasikiliza dhana au mawazo mengine

Matumizi mazuri ya taswira na ishara hutegemea ufundi wa mwandishi kuweza kuchota mambo mbalimbali yaliyomzunguka yeye na jamii yake pamoja na historia ya jamii na sehemu nyingine za jamii azijuazo

2. Matumizi ya mbinu nyingine za fasihi/sanaa

### Matumizi ya ucheshi

Ni mbinu ya kifani ambayo wasanii huitumia katika kazi zao za fasihi kuzichekesha hadhira zao au kuzifanya hadhira hizo zitabasamu. Ucheshi hutumiwa kwa mambo mbalimbali k.v kuondoa uchovu, kufurahisha hadhira au kujenga kejeli kwenye kazi zao

### <u>TAHARUKI</u>

Ni hali ya kusisimshwa kwa hadhira na shauku ya kutaka kujua jinsi mambo yatakavyojiri katika sura au sehemu zijazo za kazi ya fasihi. Hali ya taharuki hujengwa makusudi katika sura ama sehemu zijazo za kazi ya fasihi. Hali hii hujengwa na msanii ili kumfanya msikilizaji au mtazamaji/ msomaji aendelee kusubiri litakalotokea

- Nidaa – ni msemo unaonyesha kushangazwa kwa jambo fulani, msemo huu huambatana na alama ya mshangao

Mfano: Zaituni mpenzi wangu! Ningekuwa na uwezo ningekuandalia harusi ya ndovu kumla mwenyewe.

- Methali – ni sehemu ya lugha (ambayo) inaweza kufananishwa na kiungo cha lugha. Ni kitoweo cha lugha pia hutumiwa kwa kuyatafakari na kuyapima maisha kufunzia jumuiya na kutawala amri na mazingira ya binadamu.

Methali hufunua falsafa ya jamii na hekima ya wale wanaoitumia katika mazungumzo yao. Methali hutayarisha fani na maudhui ya kazi ya fasihi kutokana na kutumiwa kama daraja la kupitisha hekima.

- Misemo – hutumika wakati mwingine kutambulisha mazingira au kujulisha hadhira wakati unaohusika katika kazi ya fasihi inayoshughulikiwa. Hii ni kwasababu misemo huzuka, huibuka na kutoweka kutofautiana na hali mbalimbali za mazingira

- Nahau – ni msemo uliojengwa kutumia maneno ya kawaida ambayo huwa umesitiri maana tofauti na ile inayobebwa na maneno hayo katika matumizi ya kawaida

Mfano: Ali kavaa miwani

Ali ameyachapa maji

Christina ana mkono wa birika

- Mandhari/ mazingira – Ni sehemu ambayo matukio ya hadithi au masimulizi yanafanyika. Mandhari haya yaweza kuwa ya kubuni au halisi lakini katika masimulizi mengi ya kihistoria, mandhari yake ni halisi. Mandhari pia hutegemea na ubunifu wa mtungaji kwa kuyachukua na hali halisi.

- Jina la kitabu na kava yake – hapa tunaangalia kama jina na kava la kitabu yanasadifu yaliyomo ndani ya kitabu hicho. Mfano Riwaya ya "watoto wa mama ntilie" kava kwa jina la kitabu yanasadifu yaliyomo ndani.

- Kufaulu na kutofaulu kwa mwandishi – tunaangalia ubora na udhaifu wa mwandishi kifani na kimaudhui katika kazi yake

---

# UTUNGAJI WA KAZI ZA FASIHI ANDISHI

Utungaji wa kazi za fasihi andishi ni mada inayogusa au inayohusu ubunifu wa maandishi.

**Kubuni** ni kutunga kisa kutokana na matukio ambayo mwandishi ana uzoefu nayo kupitia milango yake ya fahamu.

Uwezo wa msanii kueleza visa vya uongo kutokana na matukio ya kweli kwa lengo la kuburudisha, kuelimisha au kuakisi hali halisi ya jamii hiyo ni kutunga.

Kimsingi siku zote msanii hatungi kitu ambacho hakipo duniani bali hutunga kutokana na mambo yaliyomo ndani ya jamii husika.

**UTUNGAJI WA HADITHI**

Hadithi ni kazi ya sanaa inayotumia lugha ya nathari. Hadithi yaweza kuwa masimulizi ya kweli au ya kubuni

Sanaa ya hadithi ni kazi ya mtu, yenye wigo wa uyakinifu ambao umefungamana na wakati, mazingira na mfumo wa jamii

Kwa kawaida masimulizi yanayokuwa katika hadithi yanaweza kumhusu mtu mmoja au watu wengi

Pia masimulizi hayo yanaweza kuhusu mambo yaliyotokea au yanayoweza kutokea

Hadithi hutofautiana kwasababu ya tofauti za uwezo wa wasanii wa hadithi yenyewe. Kwa hiyo uwezo wa msanii ni muhimu katika ujenzi wa hadithi na pia sio tu uwezo wa msanii aidha wakati mwingine na lengo la msanii mwenyewe

**TANZU ZA HADITHI**

Kuna aina mbili za hadithi

- Hadithi fupi (visa)
- Hadithi ndefu (riwaya)

**HADITHI FUPI**

Ni aina ya kazi ya sanaa ya utanzu wa hadithi inayotumia lugha iliyoandikwa katika nathari au iliyo katika masimulizi kama haijaandikwa

Hadithi fupi huwa na tukio moja au mawili na mawanda yake sio mapana sana, haina mchangamano mkubwa na matukio.

Wahusika wa hadithi fupi ni wachache ukilinganisha na hadithi ndefu na hutendeka kwa muda mfupi

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA UTUNZI WA HADITHI**

**MAUDHUI**

Mwandishi ana uhuru wa kuandika kitu chochote ambacho kina manufaa kwa jamii na umma kwa ujumla pia maudhui ya hadithi hutofautiana toka jamii moja na nyingine na hutofautiana na mazingira na mahitaji ya jamii hiyo. Riwaya huwa na dhamira kuu na dhamira ndogondogo

**MBINU ZA KIFANI NA HADITHI**

**MIUNDO**

Mpangilio wa visa na matukio. Mtunzi mzuri ni yule anayejua kupangilia visa na matukio na kusuka visa vyake kwa umakini zaidi kiasi cha kumvutia msomaji wake awe na shauku ya kuendelea kusoma kazi hiyo ya fasihi. Mara nyingi hadithi huwa na muundo wa msago, riwaya huwa na muundo wa rukia na msago

**MTINDO WA KAZI**

Kazi iliyo nzuri mara nyingi huwa na vionjo kwa msomaji, msanii inabidi atumie mbinu mbalimbali za kumvutia msomaji kwani msanii anaweza kutumia mbinu za kifadi/fasihi simulizi na pia kuchanganya tanzu za fasihi katika tanzu yake hiyo. Pia muundo wa monolojia na dialojia.

**MATUMIZI YA LUGHA**

Lugha ndiyo nyenzo kuu ya fasihi yoyote ile. Kwani kwa kiasi kikubwa lugha husaidia katika kuunda fani na maudhui kwa kazi ya fasihi

Ni vema mtunzi akitumia lugha yenye vionjo ili kuweza kuwa na umakini wa msomaji

Hali kadhalika msanii inabidi atumie usanii katika kuweza kumpa kila mhusika na lugha yake ili imsaidie katika kutambulisha mhusika wa kazi hiyo pia lugha yake iwe inaendana na wasifu wa mhusika wa kazi hiyo. Pia lugha iwe na tamathali za semi kujitosheleza, taswira na mbinu nyingine za kisanaa.

**UTEUZI WA UUMBAJI WA WAHUSIKA**

Mwandishi anapaswa kuchagua na kuumba wahusika wake kiasi cha kukubalika na hali halisi kitabia na maumbile. Mfano: kama ni kiongozi basi aonekane ni kiongozi kweli. Riwaya huwa na wahusika wakuu na wahusika wasaidizi na wote wanaelezwa na kujengwa kirefu.

**UTEUZI WA JINA LA KITABU**

Msanii anapaswa kuwa makini katika kubuni jina la kitabu kwa sababu ndilo linalomvutia msomaji wa kazi ya fasihi

**UTEUZI WA MANDHARI**

Ujenzi mbaya wa mandhari huleta athari mbalimbali katika hadithi na riwaya. Kuna mandhari za aina mbili ambazo ni kubuni na halisi

Vilevile mandhari ya kuelezwa vizuri huimarisha mfumo wa hadithi/ riwaya pamoja na ujengaji wa wahusika wake.

Mandhari ikiumbwa vibaya huathiri mfumo mzima wa kazi ya fasihi, pia matumizi ya vifaa viendane na wakati.

**HADITHI NDEFU (RIWAYA)**

Riwaya – ni kisa changamano ambacho huweza kuchambuliwa na kupimwa kwa mapana na marefu kifani na kimaudhui

Hufungamana na wakati (visa vinaendana/ vinatendeka katika wakati fulani)

Ina mawanda mapana (kwa upande wa yale yanayozungumzwa wakati na mahali pia matukio hayo)

Changamano (visa, dhamira, tabia, wahusika)

| | RIWAYA | HADITHI FUPI |
|---|---|---|
| Upana wa mawanda | Hutumia mawanda mapana. Hii ina maana kuwa kila jambo linapewa uzito wake na kuelezwa kwa mapana ya kutosha | Hutumia mawanda yasiyo mapana. Kila jambo huelezwa kwa kifupi na kimkato tu |
| Wahusika | Hutumia wahusika wengi. Mfano mhusika mkuu, wasaidizi na huelezwa kwa kirefu | Hutumia wahusika wachache, mara nyingi huwa wawili wakizidi sana hawafiki 10 na wahusika hawa wanagawanywa katika mafungu makuu mawili wema na ubaya |
| Mazingira/ mandhari | Riwaya hutumia mazingira yenye kuwa na uhalisi na wakati mwingine hutumi mandhari dhania | Hutumia mazingira yenye uhalisi na aidha mazingira dhama |
| Urefu | Riwaya ni kazi ya kubuni ambayo ni ndefu. Urefu unatokana na uchangamano wa visa na wahusika wengi | Hadithi fupi ni kazi ya sanaa ambayo ni fupi |
| Uchangamano | Ina muundo changamano kutokana na wingi wa matukio | Ina muundo sahilii usiochangamana na tukio moja tu |
| Dhamira | Huwa na dhamira kuu na ndogondogo | Huwa na dhamira chache na wakati mwngine 1 tu |

## UTUNZI WA TAMTHILIYA

Tamthiliya ni utungo wa kidrama ambao ni aina mojawapo ya maandishi ya sanaa za maonyesho. Ni sanaa inayoonyeshwa kwa ufundi

Tamthiliya huonyesha matendo ya wanajamii kwa njia ya kuigiza, maigizo ambayo hatimaye huweza kuonyeshwa kwenye majukwaa katika sanaa za maonyesho

## SIFA ZA TAMTHILIYA

Tamthiliya huwa na sifa za kawaida za sanaa za maonyesho

- Dhana inayotendeka
- Mtendaji
- Uwanja wa kutendea
- Watazamaji
- Kusudio la kisanaa – hii hutupa uhakika kuwa kinachotendeka hapo kimedhamiriwa kwa sanaa na sio kitu kingine

- Muktadha wa kisanaa – unafafanua mazingira ya tukio hilo
- Ubunifu – ni muhimu ili kutofautisha kati ya tendo la dhati na tendo la kisanaa

## DHIMA YA TAMTHILIYA

**KUELIMISHA**

Kutunza kumbukumbu (mali) za jamii

Kuonya na kuadabisha

Kuhamasisha shughuli za kimaendeleo

Kusisimua – kuhuzunisha, kuburudisha

Tamthiliya huwa na vipengele vifuatavyo

## HADITHI (simulizi)

Huwa ni kisa cha kubuni au cha ukweli au mchanganyiko wa vyote viwili

Hadithi huwa na mzozo fulani wa pande mbili hadi kufika mwisho wake.

AB – chanzo au mwanzo wa mchezo, chanzo cha mgogoro, huelezwa na hali ya tamthiliya kama ni ya majonzi au furaha

Wakati na mahali panapotokea vitendo vya hadithi

Wahusika hutambulishwa

BC – Kukua kwa mgogoro, mvutano baina ya pande mbili hujitokeza chanzo cha mgogoro huelezwa. Njia ya kutatua tatizo hujaribu kutatua

C – Tatizo limefika kileleni ambapo uwezekano wa kulitatua huwa hamna

CD – migogoro huanza kuleta mshtuko na taharuki hutokea

DE – mgogoro hufika mwisho

## VITENDO

Kitendo – tamthiliya hugawanyika katika sehemu kuu ziitwazo vitendo. Kila kitendo huzingatia tendo moja kuu, tamthiliya huwa na vitendo vitano

Vitendo hugawanywa katika sehemu ndogondogo ambazo ni maonyesho, ambapo onyesho moja huwa na tukio moja linalotendeka mahala pamoja.

Onyesho moja hutenganishwa na lingine kutegemea na kitu kinachosimuliwa. Kumalizika kwa tukio huashiria kwa wahusika kuondoka kuzima taa n.k

## WAHUSIKA

Uhusika wao hufanywa kwa matendo yanayohusiana na kile wanachokizungumzia. Na pia wahusika wake hawatofautiani na wa hadithi ambapo kuna wahusika wakuu na wadogo

## DAYALOJIA

Ni mazungumzo ya wahusika huitwa dayalojia kufanikiwa na msanii ni jinsi ambavyo anavyotunga dayolojia yake kwa namna ya kuvutia na azingatie maneno machache yanayojitosheleza

Pia monolojia huweza kutumika pale ambapo mhusika anakuwa anawaza mwenyewe moyoni.

## MBINU NYINGINE

Kama nyimbo huweza kutumika, mbinu za utambaji, ngano n.k

## UTUNGAJI WA UANDISHI WA INSHA NA MATANGAZO

Utungaji ni kazi ambayo humdai mwandishi kufikiria jambo la kutunga. Utungaji unaweza kufanywa kwa kuandika au kuzungumza

Pia unaweza kufanywa kwa kutumia maumbo mbalimbali kama insha, barua, hotuba, mashairi, risala, matangazo na midahalo

## UANDISHI WA INSHA

**INSHA** – ni kifungu cha habari chenye aya moja au zaidi. Ni habari yenye lengo moja au zaidi. Insha inaweza kuwa ya kisanaa au isiyo ya kisanaa.

Insha ya kisanaa na insha ambayo maelezo yake au hoja zake hutolewa kwa kutumia lugha ya kitamathali huwa na vivumishi vingi na kwa hiyo huwa na mvuto kwa wasomaji

Insha ambayo siyo ya kisanaa nii insha ambayo huwa na mawazo au hoja ambazo hotolewa kwa mtunzi. Mtunzi huyo hutoa hoja nyingine za kuzitetea au kuzipigia hoja hizo.

Insha za wasifu ni insha ambazo husifia mtu, vitu au mahali, mfano; insha za wasifu wa kisanaa hutumia lugha ya kitamathali ambayo humfanya msomaji apate hisia ya jambo.

Mfano wa insha ya wasifu

Ali maftaha (form 1)

Misingi ya uandishi wa insha

- Kichwa cha insha

Huandikwa kwa herufi kubwa, katikati juu ya insha. Huandikwa kwa ufasaha na kwa muhtasari, husizidi maneno matano

Huzingatia wazo kuu la insha na wakati mwingine hupigiwa mstari

- Utangulizi

Huzingatia fasili ya jambo linalozungumziwa, uhusiano wake na vitu vingine na muhtasari wa insha inayotungwa na utangulizi wa insha hauzidi njia moja

- Kiini cha insha

Ndio sehemu ambayo huzingatia mawazo makuu ambayo hupangwa katika aya zenye mtiririko mzuri wa mawazo. Sehemu hii huonyesha kwa undani jambo linalozungumziwa

- Mwisho/hitimisho

Ni maelezo ya umalizaji juu ya yale yaliyojadiliwa. Maelezo hayo huweza kuwa maoni au mapendekezo ya jambo lilozungumziwa mara nyingine huonyesha muhtasari wa yale yaliyojadiliwa.

Mfano wa insha ya kiada

Inafahamika wazi kuwa ukuta wa nyumba ukipasuka tunatakiwa kutengeneza haraka. Tusipo fanya hivyo unaweza kuharibika zaidi na kusababisha madhara makubwa

Methali hii inaweza kutumiwa kwa mambo mbalimbali ya maisha. Inatuhimiza tufanye shughuli zetu ipasavyo

Mfano: mwanafunzi akisoma kwa bidii atafaulu mtihani. Akiwa goigoi hatafaulu. Atajiona amezongwa na shaka kubwa ya masomo na atakata tamaa.

Tabia mbaya zikomeshwe mapema. Watoto wavivu, watundu na wadokozi wakanywe mapema. Wizi wa vitu vidogo vidogo kama kalamu na daftari ukemewe la sivyo mtoto anaweza kuwa mwizi mkubwa.

Methali hii inatuonya kwamba tusidharau mambo madogo kwani huenda yakazaa makubwa nayo yakaleta matata. Tujiandae kuyaepuka matata kwani “cheche huzaa moto, tone huzaa mto, mto huzaa jito, ziwa huzaa habari”

---

# UANDISHI WA MATANGAZO

Matangazo ni habari za kijamii katika vyombo vya habari kwa lengo la kushawishi au kutoa taarifa kwa jamii ili kununua, kuuza au kupata taarifa iliyokusudiwa kwa muhtasari. Matangazo hulenga watu mahsusi kwa jamii

**Dhima za matangazo katika jamii**

- Kutangaza bidhaa mbalimbali
- Kutoa tahadhari kabla ya tukio linalokusudiwa kutekelezwa siku za usoni
- Kuelimisha jamii – hutumika kama kutoa ujuzi, stadi, maarifa mbalimbali: mfano; kuhusu **UKIMWI**, Malaria, Kipindupindu n.k
- Kusaidia kuboresha shughuli za kiuchumi

**<u>Mambo muhimu katika uandishi wa matangazo</u>**


- Kichwa cha habari (kuandikwa kwa herufi kubwa)
- Kufanya aina ya biashara (kama matangazo ya biashara)/ aina za bidhaa
- Mahali inapopatikana hiyo bidhaa au huduma
- Kufanya njia ya mawasiliano

## <u>UANDISHI WA MATANGAZO MAGAZETINI</u>

### <u>Vitu vya kuzingatia</u>

- Kutilia mkazo dhumuni la tangazo hilo
- Kutumia lugha rahisi yenye sentensi fupi zenye tamathali za semi na mbinu nyingine za kisanaa
- Kutumia vivumishi vyenye kuvutia na kushawishi walengwa
- Kutumia lugha ya kibunifu

Mfano wa matangazo




UANDISHI WA INSHA ZA KISANAA

INSHA- Ni kifungu cha habari chenye aya moja au zaidi. Insha hizo zinaweza kuwa za kisanaa au zisizo za kisanaa.

Insha za kisanaa-Hizi ni Insha ambazo hutumia vipengele mbalimbali vya fasihi katika kuwasilisha ujumbe. Mfano nahau, methali, misemo au tamathali za semi huweza kutumika

Mfano wa Insha za kisanaa

**Mzee toboa mpenda haki**

-Mzee toboa ni dereva wa teksi kwa miaka mingi jijini Dar es Salaam kutokana na uzoefu wa

kazi yake, Uaminifu, Uzungumzaji na Ucheshi kwa wateja wake aliweza kujipatia chumo nono la kila siku. Wenzanke walimwonea gere mzee huyo, maana hata anapokuwa katulia katika kundi la madereva akisubiri abiria wa kukodi teksi wengi humtaka yeye. Alikuwa na Umri wa miaka arobaini au hamsini hivi, mwenye Umbo la wastani si mnene wala si mwembamba aidha si mrefu wala mfupi kichwa chake hakikuwa kikubwa lakini kilijaa busara. hulka njema na hekima yake kubwa vilimfanya aheshimiwe na watu.

Japokuwa hakusoma sana, mzee Toboa alijaliwa kuijua siasa ya nchi yake barabara. Alikuwa na tabia ya kuongea na kila mtu, watoto, vijana,wazee, viongozi matajiri na makabwela, kwa maneno mengine mzee Toboa alikuwa mcheshi na mwema. Kwa tabia yake hiyo aliweza kujua matukio mbalimbali mitaani kwa urahisi zaidi. Yeye hakupenda Uovu wala dhuluma. Alisubiri kwa hamu siku ambapo maovu yangetoweka kabisa .

Mzee Toboa aliweza kukemea watoto wenye tabia mbaya kwani aliweza kuwaambia Asiyesikia la Mkuu huvunjika guu, kwa maana kwamba Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu. Mzee Toboa aliweza kufanikiwa kujua kila Ovu lililokuwa likitokea kwani aliweza kuchukua hatua harakaharaka.

---

# UFAHAMU NA UFUPISHO

**UFAHAMU**

**Ufahamu** Ni hali ya kulijua na kulielewa jambo kwa usahihi na kuweza kulielezea kwa ufasaha bila kupoteza maana yake ya msingi

**Au**. Ni kujua na kuelewa jambo na kuweza kulifafanua

Madhumuni ya kufundisha ufahamu ni kumwezesha mwanafunzi kuelewa mambo mbalimbali kwa njia ya lugha pamoja na kukuza ustadi wake katika kuzungumza kusoma na kuandika

**<u>Aina za ufahamu</u>**

- **Ufahamu wa kusoma**

Ni kuzingatia maana ya neno sentensi na habari yote. Msomaji lazima aweze kutambua mpangilio wa herufi maneno na tarakimu na kuzitofautisha

Upo usomi wa aina mbili

(I) Kusoma kimya

(II) Kusoma kwa sauti

Usomaji wa makini na kina katika habari husika

## KUSOMA KIMYA NA KWA HARAKA

Ni njia ambayo msomaji anapitisha macho kwenye maandishi bila kutilia makini na sio kwa kina

Ili kufaulu kwa habari kwa usahihi, maswali yanayotokana na habari ya kusoma sharti azingatie mambo yafuatayo

- Kuwa mtulivu na makini

Msomaji anapaswa kuwa mtulivu na makini katika kile anachokisoma kwa kufanya hivyo huweza kuelewa vizuri mada kuanzia utangulizi wake hadi hitimisho na bila kuruka baadhi ya aya

- Kuelewa maana ya maneno na misemo

**Zipo njia mbili za kupata maana ya maneno katika habari**

- Kwa kutumia kamusi
- Kwa kuzingatia muktadha (mazingira) ambamo neno au maneno yametumika. Hapa tunapata kama lilivyotumika kwenye kifungu cha habari kwa kuwa neno moja huweza kuwa na maana nyingi. Msomaji anapaswa ajizoeshe kupata maana kama ilivotumika katika habari

- Kubuni mawazo

Kwa kawaida aya moja huzungumzia wazo kuu moja. Msomaji anatakiwa abainishe wazo kuu kwa kila aya.

Msomaji hanabudi kuzingatia mbinu za kujiuliza katika kubainisha wazo katika aya hatimaye kiini cha habari nzima ambacho hutoa picha ya aya zote

- Kubainisha matumizi mengine ya lugha

Katika nakala/ habari kuna kuwa na matumizi mbalimbali ya lugha kama vile nahau na misemo, methali, tamathali za semi, ishara/taswira

**Kujibu maswali kutokana na taswira uliyosoma inabidi uzingatie mambo yafuatayo**

- Soma nakala inayohusika
- Ukishasoma, soma maswali uliyoulizwa ili kujua kinachotakiwa
- Ukishajua kinachotakiwa rudia kusoma nakala yote, safari hii kwa makini zaidi huku ukijitahidi kupata mawazo muhimu ya maswali yaliyoulizwa
- Msomaji katika hatua hii anaweza kutumia kalamu ya risasi kuweka alama katika sehemu anayodhani ni jibu sahihi

- Baada ya kusoma nakala hiyo na kuweka alama majibu yako sasa msomaji anaweza kujibu maswali

## KUSOMA KWA SAUTI

Ni aina ya usomaji ambao humwezesha msomaji kupata ujumbe na kuweza kutamka lafudhi ya Kiswahili

- **Ufahamu wa kusikiliza**

Ni ule ambao muhusika anaupata kwa kusikiliza habari fulani. Inawezekana kupata kwa kusimuliwa au kusomewa

Ili kupata ufahamu kutokana na habari unayosikiliza lazima msikilizaji azingatie mambo yafuatayo;-

- Kusikiliza kwa makini ili kuelewa wazo kuu
- Kuhusisha mambo muhimu na habari inayosimuliwa
- Kujua matamshi ya mzungumzaji
- Kubainisha mawazo makuu

Mambo ya kuzingatia katika ufahamu wa kusikiliza

- **Kubaini mawazo makuu**

Msimulizi akizungumza huwa ana ujumbe anaotaka uwafikie watu. Wakati mwingine hupanga ujumbe huo kwa namna nyepesi ili msikilizaji aupate kwa haraka.

Mara nyingine huchanganya wazo zaidi ya moja kutoka aya moja lakini mawazo hayo yanakuwa yanahusiana.

Ili msikilizaji aweze kubaini wazo kuu, atalazimika kusikiliza kwa makini

- **Kubaini maana ya maneno na misemo**

Katika habari ambayo mtu anapata katika kusikiliza aghalabu kuna maneno magumu. Hivyo maana ya maneno itapatikana kulingana na matumizi (maana iliyokusudiwa) kama msomaji ameshindwa kupata maana anashauriwa kutafuta katika kamusi ya Kiswahili

- **Kusikiliza kwa utulivu**

Ni wajibu wa msikilizaji kusikiliza kwa utulivu maelezo ya msomaji. Mbinu hiyo itamwezesha kuelekeza fikra zake kwenye maelezo yanayotolewa na hivyo kuweza kuelewa mada vizuri pamoja na maswali kwasababu kuna wengine hawamudu vizuri matamshi sahihi ya Kiswahili

Mfano; raha – laha

Fedha – feza

- **Kujibu kwa ufupi**

Baada ya kubaini majibu/ jibu la maswali/swali unatakiwa kujibu kwa kutumia maelezo machache tu. Maelezo hayo sharti yawe tu yanahusiana na kipengele kinacholengwa na swali.

## UFUPISHO

Ni maelezo mafupi yaliyoandikwa kutokana na habari ndefu bila kupoteza maana ya msingi ya habari hiyo.

**Ufupisho husaidia katika shughuli mbalimbali kama**,

- Husaidia wakati wa kudondoa hoja kutokana na mihadhara, hotuba n.k
- Husaidia katika uhariri wa habari
- Hutumika katika kuandika kumbukumbu za kila siku
- Huokoa fedha kama vile upelekaji wa simu za maandishi
- Hutumika wakati wa kutayarisha ripoti na kumbukumbu za mikutano

**Hatua za kufupisha habari**

- Kuisoma au kuisikiliza habari kwa makini ili kuelewa vizuri.
- Kutambua au kubaini mawazo makuu yanayojitokeza katika kila aya.
- Kuyaunganisha mawazo makuu na kuiandika au kuielezea habari hiyo kwa maneno yako mwenyewe
- Kuhesabu idadi ya maneno ya ufupisho ili kuyapunguza ikiwa yanazidi idadi inayotakiwa
- Kuandika idadi ya maneno mwisho wa ufupisho upande wa kulia wa chini kidogo

Wakati wa kufupisha ni muhimu kuzingatia njeo, kauli na nafsi kama ilivyotumiwa katika matini ya awali. Kwa kawaida habari hufupishwa hadi kufikia theluthi moja 1/3 ya maneno ya matini awali

Ufupisho pia hufanywa kwa kubaini kichwa cha habari kwani ndicho kiini cha habari hupatikana baada ya kutambua mawazo makuu ya kila aya na kuyafupisha

Kichwa cha habari kinatakiwa kisizidi maneno matano.

---

**VITABU TEULE VYA FASIHI**

**UCHAMBUZI WA RIWAYA.**

**Jina la kitabu: TAKADINI**

**Mwandishi: BEN J. HENSON**

**Wachapishaji: METHEWS BOOKSTORE AND STATIONERS**

**Mwaka: 2004**

A: UTANGULIZI

*Takadini* ni riwaya inayoeleza maisha ya jamii za Kiafrika na tamaduni zao. Hii ni desturi ambayo imeandikwa kulenga watu au jamiii ya watu wanaokumbatia mila na desturi zilizopitwa na wakati. Riwaya hii imeelezea namna jamii nyingi za Waafrika walivyowakandamiza au kuwanyanyapaa watu waliozaliwa na ulemavu katika jamii.

Mwandishi ametumia 'Zeruzeru' Kama mfano tu wa wahanga wa mila na desturi zilizowataka wanajamii kuwafutilia mbali walemavu hao katika uso wa dunia hii.

Mwandishi amejaribu kuonesha baadhi ya mila zilizopo katika Jamii kuwa hazifai kuendelea kutumiwa kwani hazizingatii utu wa mtu. Tofauti za rangi au upungufu wa viungo vya mwili si kigezo cha kutotambua utu wa watu.

Katika riwaya hii, mwandishi anatuonesha maisha anayopitia Takadini kuwa yalijaa unyanyapaa, ubaguzi, uonevu na kudharauliwa n.k. Kuzaliwa kwa Takadini kulisababisha mgawanyiko mkubwa sana katika jamii kwani hakutakiwa na jamii nzima isipokuwa mama yake Sekai tu ambaye alilazimika kwenda uhamishoni ili kunusuru maisha ya mtoto wake. Takadini anatengwa na watoto wenzake, watu wazima na jamii nzima. Anakua katika maisha ya kutengwa sana. Hata hivyo Sekai na baba Chivero ndio walibaki kuwa wazazi na marafiki wa kweli maishani mwake.

Je, Zeruzeru (sope) hakuwa na haki ya kuishi kama jamii yake ilivyoamini? Je, Zeruzeru hana nafasi katika ujenzi wa jamii mpya kama walivyo watu wengine?

Takadini katika maisha yake anatupatia majibu ya maswali yote haya. Takadini kama Zeruzeru (sope) aliweza kufanya shughuli mbalimbali kwa umaridadi kama watu wengine au hata kuwazidi watu wasiokuwa na ulemavu. Takadini alionyesha kuwa sope ni mtu kama walivyo watu wengine na kwamba wana hisia na haki ya kupenda na kupendwa. Takadini aliangukia katika penzi la dhati la Shingai. Walifanikiwa kupata mtoto ambaye hakuwa Zeruzeru.

*Kwa nini Zeruzeru wauliwe?*

*Kwa nini Zeruzeru watengwe?*

*Kwa nini Zeruzeru wadharauliwe?*

*Kwa nini Zeruzeru wavuliwe utu wao?*

Hakuna sababu ya msingi inayoweza kuhalalisha unyama wanaotendewa walemavu wote. Ni baadhi ya mila na desturi ndizo zimejaribu kuhalalisha hayo kwa muda mrefu. Jamii sasa inabadili mtazamo wake kuhusu zeruzeru na walemavu wote wanalindwa na kupewa fursa sawa na wengine ili utu na heshima zao ziweze kutambuliwa na kuzingatiwa na jamii nzima.

**PITIO LA KITABU**

1. ***Familia ya mzee Makwati***

Mzee Makwati alikuwa na wake wanne na wote aliwapenda sana. Mke wa kwanza alikuwa Sekai wa pili aliitwa Pindai, watatu Dadirai na wa mwisho ambaye alikuwa ni mdogo kuliko wote aliitwa Rumbiozai.

Katika familia hii wake wa mzee Makwati wanaonekana wakibaguana wenyewe kwa wenyewe na pia wanakuwa hawaelewani huku wivu ukiwatawala. Mfano, Mke wa kwanza alikuwa ni rafiki mkubwa wa mke wa pili na ndivyo hata mke wa tatu alikuwa rafiki wa mke wa nne ambaye ni wa mwisho. Sekai ni mke wa kwanza wa mzee Makwati na aliishi kwa miaka tisa pasipo ujauzito na hatimaye kupata ujauzito. Lakini ujauzito ule wa Sekai unaibua minong'ono ya chinichini kwa wake wenza na walimkejeli kwa kumwambia *"ni ndama wangapi ambao ng'ombe wake mzee amepata kwa miaka minne iliyopita?* Rumbiozai alihoji *oh amezaa watatu kwa miaka minne*. (Dadirai alijibu kwa sauti ya juu na Sekai akasikia).

Kuwepo kwa imani za kishirikina hasa pale walipohisi ni kwa vipi Sekai anaweza kuishi muda mrefu pasipo kuwa na mtoto na mumewe. Pia tunaona kuwa chakula cha jioni kinaandaliwa na wake wote wanne wa mzee Mkwati lakini mzee Mkwati baada ya kuonja vyakula vyote ndipo anaishia kula chakula kilicholetwa na Sekai.

Hatimaye Sekai anapata ujauzito na yeye analiona kitendo kile ni cha ajabu kwa kubeba mtoto mchanga katika mwili wake na anajiuliza je mtoto huyu atakuwa wa kike au wa wakiume na atakuwa na kasoro na mbaya zaidi kiumbe hicho kitakuwa binadamu au la maana ameshawahi kusikia kuhusu wanawake waliojifungua juu ya ujauzito ule wa mkewe. Sekai. Anatabiri juu ya ujauzito ule kuwa ni wa mtoto wa kike lakini mzee Makwati anakuja juu na kumwambia mkewe kuwa yeye haitaji tena mtoto wa kike bali anahitaji mtoto wa kiume. Hivyo Sekai anamhakikishia mumewe kuwa mtoto huyo atakuwa wa kiume na tena shupavu kama mzee Makwati mwenyewe.

Pia tunaona juu ya msimamo alionao mzee Makwati allipokuwa akimwambia mkewe kwa kumuuliza, "Je, wewe siyo mke wa kwanza wa penzi la kweli? Vipi aibu yako isiwe yangu pia? Je, siyo Mimi niliyesimama imara kati ya wazazi wangu na wewe kwa miaka hii yote"? Na mkewe akajibu "Natambua hili sana maana umepigana nao kwa muda mrefu, nawe ulikataa kunirudisha kwetu maan hapo sina dada wa kuchangia naye mkeka, nashukuru sana mume wangu kwa kunifichia aibu yangu.

2. ***Furaha kubwa kwa Sekai***

Muda wa mwisho wa ujauzito wa Sekai ulikaribia na ndipo rafiki yake, mke mwenza Pindai anamsaidia kazi za nyumbani. Amai Pedzisai ni mzee aliyekuwa kipenzi cha Sekai na aliweza kuwa karibu sana na Sekai mpaka alipokaribia kujifungua. Sekai alipata maumivu makubwa ya uchungu kuliko maumivu yote aliyowahi kuyapata, mbali na maumivu hayo lakini alitarajia kuwa na furaha kubwa siku chache zijazo.

Hatimaye Sekai alijifungua mtoto wa kiume. Taarifa hii ilipelekea furaha kubwa kwa mume Makwati. Lakini mtoto huyu aliyezaliwa aligundulika kuwa ni Sope(zeruzeru) na hata Sekai aligundua hilo na ndipo Sekai anaonyesha kuwa na woga juu ya mtoto yule lakini kwa upande mwingine anaonyosha ujasiri wake kwa kusema, “Lazima mtoto aishi maana nimesubiri kwa muda mrefu na nimeshateseka sana juu yake, hivyo mtoto huyu ni wangu na wala sitamuachia mtu”. Ambuya alimwambia, “hujui ulisemalo hivyo usihofu maana uzazi umeshafunguka na watafuata watoto wengine”.

Mzee Makwati anapata taarifa juu ya mtoto aliyezaliwa kuwa ni sope(zeruzeru) naye anaonyesha kuchukizwa na kiumbe hicho na alihoji kwa mkewe katika hali ya maswali ya mfululizo mfano, “Huo ni uchawi au ni laana ya mizimu? Na kwa nini huyo Sope yungali nasi”?, maswali haya yalimtatiza Sekai katika kuyajibu, na ndipo mzee Makwati alitoa suluhisho kwa kusema wazee ndio watatoa suluhisho la kuwepo au kutokuwepo kwa mtoto yule.

Mganga mashuhuri aitwaye Zviyedzo anashirikishwa katika kutatua tatizo lile la mtoto ambaye ni Sope.

3. ***Gumzo dhidi ya mtoto Zeruzeru***

Kuzaliwa kwa mtoto wa ajabu pale kijijini kulizua gumzo kubwa na habari kuhusu mtoto huyo zilienea kwa haraka kijijini hapo hivyo kila mtu alishikwa na butwaa.

Wake wenza na Sekai walimkejeli kwa maneno mabaya na wengine walionyesha chuki zao lakini ilikuwa tofauti kwa Pindai ambaye alionyesha upendo kwa mke mwenza huyo.

Pindai na Pedzisai walimtembelea Sekai na waliweza kujadili mambo mbalimbali zikiwemo mila na desturi za hapo kijijini . Pia waliweza kumuuliza Sekai ni kwanini aliendelea kuwa na mtoto yule na hivyo walimueleza kuwa alikuwa akipinga mila na desturi zao hapo kijijini na kutojulikana kwa ufumbuzi wa mtoto yule kulimpelekea Sekai kuwa na mawazo mengi yasiyo na kikomo, hata mzee Makwati pia naye alikuwa na mawazo mengi juu ya mtoto yule aliyezaliwa akiwa Sope.

Mzee Makwati anakasirika kwa kuona mtoto yule aliye Sope na anamshutumu mkewe labda ametembea na mwanaume mwingine hivyo amevunja mila ma desturi zao. Sekai aliumizwa sana na tuhuma hizo maana alijiona hana maana tena mbele ya mumewe na anajihisi aliyetelekezwa zaidi wakati huo. Mtihani mkubwa

ulikuwa kwa Sekai na alichokuwa akisubiri ni hukumu kutoka kwa wazee juu ya yeye na mwanae kuendelea kuishi au kutoendelea kuishi.

Mikakati mikubwa ilipangwa na Sekai ili kunusuru kifo chake pamoja na mwanaye hivyo alipanga kutoweka upesi katika kijiji kile, lakini uamuzi wake ulihitaji ujasiri mkubwa na ungeweza kuleta matumaini ya kuishi maisha mapya kwa Sekai na mtoto wake.

Alfajiri ilipofika, Sekai alijiandaa kwa safari, alifungasha vitu vyote ambavyo vilikuwa muhimu katika safari yake na bila kusahau zana za kujilinda dhidi ya wanyama wakali ambazo ni ngao na mkuki. Kabla ya kuanza safari, Sekai aliketi na kuiambia mizimu matatizo yake na akaomba akingwe na mambo yote ya hatari mbele ya safari yake.

Wakati alipo wasiliana na mizimu, punde jina likamjia moyoni aliweza kumpa jina hilo mtoto wake ambalo ni TAKADINI, ni jina ambalo hakuwahi kulisikia mahali popote pale. TAKADINI maana yake ni “Sisi tumefanya nini?” Jina hili lilisawiri vyema mambo yote yaliyomtokea Sekai wakati wa uzazi wa mwanae na huu wa sasa wenye hatari zaidi kwake.

4. ***Safari ya Sekai***

Alfajiri na mapema Sekai alianza safari yake kimyakimya toka kibandani mwake.

Alimchukua mwanae Takadini na vifurushi alivyoviandaa kwa ajili ya safari bila kusahau mkuki na ngao.

Sekai alivuka milima, mabonde na tambarare akielekea asikokujua. Kijiji alichotoka Sekai aliacha gumzo kubwa juu yake ambapo wengine walisema, “Labda alikwenda kujinyonga au amekwenda kujitosa majini.

Habari za kutoweka kwa Sekai zilienea kijiji kizima na ndipo Mtemi Zvedi aliitisha mkutano ili kujadili ni wapi aloko kwenda Sekai na ndipo Mtemi alitoa agizo la kumtafuta Sekai popote pale kuzunguuka kijiji chote.

Katika safari yake Sekai anakutana na mzee Chivero na anamueleza mkasa wote uliompata na lengo la yeye kutoroka. Mzee Chivero anamkaribisha Sekai katika kijiji chake na anamtambulisha kwa mtemi wa kijiji aitwaye Masasa. Katika kijiji waliweza kumjadili Sekai na mtoto wake ingawa ilikuwa vigumu kumkaribisha Sekai katika kijiji chao lakini hatimaye walimruhusu. Mzee Chivero ndiye aliyekuwa mlezi mkuu wa Sekai na mtoto wake.

5. ***Maisha mapya ya Sekai***

Ujio wa Sekai katika kijiji kile kipya ulikuwa gumzo kijiji chote. Wazee wa kijiji walikutana na kuweza kumjadili mgeni huyo aliyeingai katika kijiji chao. Wazee hao waliongozwa na mtemi Masasa.

Kulikuwa na imani zilizofuatiana juu ya ujio wa Sekai na mtoto wake maana walijiuliza maswali mengi pasipo kupata majibu sahihi. Na hatimaye walifikia tamati na wote walikubaliana kutomfukuza mgeni huyo maana mizimu ya kijijini hapo ilipinga kumfukuza mgeni yeyote atakayeingia kijijini hapo kinyume na hivyo kungepelekea laana kubwa toka kwa mizimu ya hapo kijijini.

Matumaini ya kuishi kwa Sekai na mtoto wake aliyekuwa Zeruzeru yalirejea upya baada ya kukubaliwa na wazee wa kijiji kuishi katika kijiji kile alichofikia.

Sekai aliweza kujengewa makazi yake pamoja na mwanae na kujishughulisha na shughuli zote za uzalishaji kama wanakijiji wengine.

Baadhi ya wanakijiji walimtenga Sekai na mtoto wake hasa upande wa wanawake wenzake. Lakini hili halikuwa tatizo kwake bali yeye alifurahia maisha mapya na yenye matumaini na aliweza kumshukuru sana mzee Chivero kwa usamalia wake wa kumsaidia yeye na mtoto wake ambaye ni Zeruzeru.

6. ***Sekai apata rafiki***

Sekai alikuwa mwanamke mchapakazi na hodari kama wanawake wengine hapo kijijini. Mzee Chivero alipata msaada mkubwa kutoka kwa Sekai kwa kufanya shughuli za nyumbani kwa mfano, kuandaliwa chakula.

Sekai alikuwa mpweke na mwenye huzuni maana wanawake wenzake walimtenga na mbaya zaidi alipokuwa akitoka shamabani njiani alikuwa akikutana na wanawake wenzake. Wanawake wajawazito hawakupenda kupishana naye na punde walipomuona walijifunika mikono yao usoni au walirudi nyuma ilimradi tu wasikutane uso kwa uso na Sekai. Mzee Chivero alitambua hilo na hivyo alikwenda kuomba msaada wa ufumbuzi wa tatizo hilo kwa mtemi Masasa na ndipo mtemi alimruhusu mzee Chivero amchukue Tendai ili amtambulishe kwa Sekai ili awe rafiki yake.

Tendai alikuwa mke wa mwisho na mdogo wa mtemi Masasa. Mzee Chivero alimtambulisha Tendai kwa Sekai. Hatimaye, Tendai ndiye aliyekuwa rafiki mkubwa wa Sekai na waliweza kushirikiana katika shughuli mbalimbali za kijamii.

Takadini sasa alifikia umri wa kuweza kukaa na hata kumtambua ipasavyo mama yake. Tendo hili lilimuongezea furaha na matumaini makubwa Sekai.

7. ***Tukio la ajabu lamtokea Sekai***

Siku moja alikuwa akirejea nyumbani toka shambani njiani aliona vijana ambao walikuwa wakirina asali.

Ghafla kundi la nyuki lilimvamia na ndipo Sekai alimtupa mtoto kichakani na yeye alijitosa majini ili kunusuru maisha yake pamoja na mwanae. Sekai alifanikiwa kuokoa maisha yake na ya mtoto pia ingawa walipata maumivu makubwa ya kuumwa na baadhi ya nyuki.

Mzee Chivero alipata taarifa hizo na aliweza kutoa msaada wake kwa kuwatibu na alitumia dawa za mitishamba na hatimaye Sekai na mwanae walirejea katika afya yao ya kawaida kama ilivyokuwa awali.

Lakini kwa Takadini haikuwa hivyo kwani alidhurika sana na aliweza kupata kilema cha maisha katika mguu wake ambacho kilitokana na kutupwa kichakani na mama yake katika harakati za kunusuru maisha yake. Huzuni kubwa ilimjia tena Sekai na aliwaza mengi juu ya mtoto wake. Pia alipatwa na uchungu na alijiuliza maswali mengi kwa kuhisi ameikosea mizimu yao kwa yeye kutoroka kijijini kwake.

Lakini Sekai alijikaza na aliamini kuwa yeye ni shupavu na yote hayo aliwaachia mizimu, hivyo muda mfupi alirejea katika hali yake ya kawaida kama alivyokuwa awali.

8. ***Maisha ya Takadini***

Takadini alikuwa na furaha kubwa bila kujali hali yake na wakati huo alianza kutambaa kwa kuvuta mguu mbovu wa kushoto. Pia. Takadini alitaabika sana wakati wa mwanga mkali na joto la jua lilimuumiza kiasi ambacho shingo yake ilienea michubuko. Kwa mapenzi ya mzee Chivero, Tendai na mama yake, Takadini alijiona ametimia kwani waliongea naye, wakacheza naye na wakamfanya ajisikie anapendwa na mwenye furaha.

Takadini alitengwa na watoto wenzake na pia walimdharau kwa kumwambia yeye alikuwa ni Sope na tena amelaaniwa.

Mzee Chivero alipokuwa akielekea msituni aliongozana na Takadini huko msituni alimfundisha jinsi ya kufahamu dawa za mitishamba na matumizi yake mbalimbali.

Takadini alionekana kuwa ni mtoto mwelevu mwenye kupenda kufahamu mambo mbalimbali. Siku moja Takadini alihuzunika sana pale alipoambiwa na watoto wenzake kuwa yeye ni Sope na tena amelaaniwa, ndipo kitendo kile kilimfanya Takadini akose raha kabisa. Mzee Chivero na mama yake walimfariji Takadini na ndipo mzee Chivero alimfariji kwa kumwambia, “Mbuyu sio mwembamba na mzuri kama miti mingine, lakini ni imara na unaishi maisha marefu kuliko miti yote msituni na ni mti wenye matumizi makubwa”. Hivyo Takadini alipofikiri akajilinganisha na mti ule kama ulivyotofautiana na miti mengine ndivyo yeye alivyotofautiana na wengine.

Akaongeza kwa kumwambia tena “Hakika wewe ni wa kipekee, na ndiyo maana upo tofauti nao, lakini bado hawajui kuwa wewe ni pekee kiasi gani.

9. ***Maisha ya Takadini***

Siku moja mzee Chivero anamletea Takadini mbwa ambaye alikuwa ni rafiki sana na Takadini hasa alipokuwa akienda msituni peke yake. Mzee Chivero alitambua hatokuwa na Takadini siku zote maishani hivyo mbwa yule angekuwa mlinzi mkubwa wa Takadini, mbwa huyo aliitwa Shumba.

Takadini alipenda sana kusikiliza hadithi mbalimbali zilizokuwa zikisimuliwa na wazee katika dare kama vile Tsuro mwenye busara. Takadini alipofikisha miaka kumi na tatu hali ya afya ya mzee Chivero ilidhohofu na alianza kukohoa muda wote, ndipo alianza kumuagiza Takadini dawa za kumletea toka msituni na Sekai aliendelea kumtunza vyema.

Takadini alijifunza kutabiri kwa kutumia mifupa na kujua sifa mbalimbali za miti shamba ambayo mzee Chivero alikusanya maishani katika kutibu maradhi mabalimbali.

Katika kijiji hicho kulitokea matukio makubwa mawili, kwanza ni sherehe ya mavuno ambayo iliambatana upigaji wa mbira na pia watu hucheza wakubwa kwa watoto, wanaume kwa wanawake.

Takadini alivutiwa sana na upigaji mbira lakini aliwaza ni nani atakayemfundisha maana alikuwa hana rafiki. Lakini hakukata tamaa ndipo akamueleza mzee Chivero. Mzee Chivero alimahidi kumtafutia mtu atakayemfundisha.

Tukio la pili katika kijiji hicho ni kutokea kwa mvua kubwa na kufariki kwa wazee maarufu kijijini hapo. Alianza kufariki mtemi Masasa ambaye alikuwa kiongozi wa kijiji kile na ndipo akafuata mzee Chivero ambaye alkuwa mganga mashuhuri kijijini hapo.

Wanakijiji wotw walihuzunika sana Sekai na Takadini walihuzunika sana baada ya kuondokewa na mzee Chivero ambaye alikuwa ndio mlezi wao na mwenyeji wao mkuu. Baada ya miezi kadhaa Sekai na mwane Takadini walirejea katika hali ya kawida na kuendelea na shughuli za kila siku.

10. ***Maisha ya Takadini baada ya kifo cha mzee Chivero***

Ulipita mwezi baada ya kifo cha mzee Chivero, ndipo siku moja mcheza mbira maarufu alipomtembelea Sekai na kumfahamisha juu ya ujio wake pale nyumbani kumfundisha Takadini kupiga mbira. Kwani aliagizwa na mzee Chivero kabla hajafariki. Takadini aliitwa na akaelezwa na baba Kutukwa kuhusu kumfundisha jinsi ya kupiga mbira. Takadini allifurahi sana na muda mfupi alianza mazoezi hatimaye alikuja kuwa hodari wa kupiga mbira.

Mzee Kutukwa alikuwa ni mzee mwenye busara kwani alimpenda sana mtoto yule aliye mpweke na alimsaidia sana kwani siku moja aliwaza kumsaidia Takadini ndipo alimtengenezea mti mzuri ambao ungemsaidia Takadini wakati wa kutembea kwani hapo mwanzo alipata shida sana kwa kutembea kwa kurukaruka.

Takadini alijawa na furaha baada ya kukabidhiwa mti ule na alianza kutembea kwa haraka sana, na huku akiwasalimu rafiki zake njiani, na wao walimshangaa sana.

Furaha na shukrani vilimjia Takadini katika nafsi yake na ndipo alichukua mbira akaanza kupiga huku akiimba wimbo mpya ambao ulimjia kama taswira akilini mwake:

*“Nawashukuruni baba zangu, Chivero kwa kunikamilisha, kwa kunipa fruraha kwa kunijaza moyo wangu kwa muziki na amani”.*

Sekai alivutiwa sana na wimbo huo uliokuwa mpya masikioni pake hivyo naye aliishukuru mizimu kwa furaha aliyonayo.

11. ***Tukio la kusikitisha latokea kijijini***

Miezi sita ilipita baada ya Takadini kuanza kupiga mbira. Vijana wote wa kijijini hujishugulisha na uchungaji wa mifugo yao na pindi wawapo machungani huonyeshana ubabe wa kupigana ili kujua nani zaidi.

Ilikuwa ni tofauti na siku zote siku hiyo waliendekeza mchezo wao kama kawaida yao kumbe siku hiyo alitokea simba mkubwa na akamla ng’ombe mmoja ambaye ni maksai. Kitendo hicho kiliwasikitisha sana wanakijiji hivyo walijawa na woga dhidi ya simba huyo.

Wanakijiji wanapanga kuingia msituni ili kumsaka simba huyo na hatimaye wanafanikiwa kumuua simba huyo. Baada ya ushindi huo, wanakijiji wanafanya sherehe kubwa ili kujipongeza kwa ushindi huo.

Takadini alikuwa mmoja kati ya wapigaji mbira katika sherehe hiyo. Lakini baadhi ya watu walikasirishwa na tendo la kumhusisha Takadini ambaye alikuwa ni Sope (zeruzeru) watazamaji na wachezaji siku hiyo walifurahishwa sana na upigaji mbira wa Takadini na wimbo wake ambao watu wote waliupenda.

Baadhi ya wasichana walivutiwa sana na uhodari wa Takadini akiwepo msichana mmoja aitwaye Shingai.

Shangai alitoke kuvutiwa sana na Takadini hivyo alitumia kila mbinu ilimradi awe karibu na Takadini.

Siku moja Shingai aliteka maji mtoni na kumpelekea Sekai nyumbani kwake na ndipo Sekai anastaajabu kwa tendo lile lakini Shingai anathibitisha kwa kumwambia amejitolea tu kwani kwake anaona si vibaya kumsaidia mtu mkubwa.

Hatimye habari zilienea kijiji kizima kuhusu kitendo cha Shingai alichofanya.

Wazazi wa Shingai walichukizwa sana. Wazee wa kijiji nao waliweza kujadili hili na ingawa hawakufikia muafaka wa tukio hilo.

12. ***Gumzo kijijini dhidi ya Takadini***

Tendai anamtembelea Sekai nyumbani kwake na wanajadili juu ya Takadini na Shingai. Baada ya Shingai kuzuiliwa kutokewenda tena nyumbani kwa Sekai, hivyo Shingai alikuwa mpweke sana na mwenye mawazo juu ya Takadini. Hivyo ndivyo ilivyokuwa hata kwa Takadini kwani alijihisi kukosa amani.

Shingai alipendwa sana na kijana aitwaye Nhamo, lakini Takadin na Nhamo walikuwa maadui toka utotoni.

Ilifanyika tena sherehe nyingine kubwa hapo kijijini maalumu kwa kumkumbuka marehemu mzee Chivero na Takadini alichaguliwa katika kupiga mbira. Takadini alionyesha umakini wake hasa pale alipoimba wimbo wake mwenyewe wa kumtunza mzee Chivero. Sauti yake ilikuwa nzuri na kila mtu alivutiwa naye na kusahau kama aliyecheza na kuimba ni Sope(zeruzeru). Shingai naye hakuwa mbali, bali naye alikuwepo katika sherehe hiyo pia hata Nhamo alikuwepo akifuatilia nyendo za Shingai na Takadini.

Hatimaye Nhamo aliweka mambo wazi juu ya azma yake ya kumuoa Shingai na alimtuma munyai (mshenga) akatoe taarifa nyumbani kwa akina Shingai lakini Shingai hakuvutiwa na Nhamo bali alivutiwa na Takadini.

Siku moja Nhamo alikwenda nyumbani kwa akina Takadini na akamtahadhalisha aachane na Shingai vinginevyo atampiga. Kitendo hiki cha kitisho kilimnyima raha Takadini lakini alipiga moyo konde.

Chido naye alikuwa msichana ambaye naye alivutiwa Sana na Nhamo hivyo Chido na Shingai alikuwa hawapatani. Swala hili lilimjengea sana hofu Shingai kwani hakupenda kuchangia mume mmoja na Chido. Shingai alitamani awe na ujasiri kama wa Sekai ambapo alipingana na wazee wa kijiji na hata Takadini akakua baada ya kuuawa.

Wakiumizwa na haja ya kuficha hisia zao za kweli, Shingai na Takadini walitafuta mbinu za kuweza kuonana. Tambudzai alikuwa ni rafiki wa Shingai na alikuwa akimsaidia sana Shingai pindi wasichana wenzake walipomsema baada ya yeye kuhisiwa kuwa ana mahusianao na Takadini.

13. ***Furaha ya Takadini.***

Ulibaki mwezi mmoja kabla ya ndoa kati ya Nhamo na Shingai. Takadini alitumia muda mwingi kujifariji na mbira yake kwa kumkomoa mpenzie. Kabla ya ndoa, mzee maarufu aitwaye Makaure alifariki dunia hivyo wanakijiji walihuzunika sana.

Siku moja katika kibanda chake Takadini alisikia mtu akifungua mlango na alipotahamaki alimuona Shingai akiingia ndani mle katika usiku wa kiza. Shingai alimkaribia Takadini na akavuta gudza na wakajikuta wanafanya tendo la ndoa. Jua lilipochomoza Shingai hakuonekana kwao na walipomtafuta walimkuta kwa akina Takadini.

Familia ya akina Shingai ilimtenga kuanzia siku ile lakini Sekai hakumfukuza Shingai nyumbani kwake. Wazee wa kijiji waliwajadili sana Shingai na Takadini lakini walifikia tamati kwa kusubiri kitakchoendelea.

Nhamo aliamua kumua Chido badala ya Shingai. Chido na Nhamo wakaungana kumchukia Takadini. Chido alimchukia sana Shingai baada ya kujulikana ana mahusiano na Takadini.

Baada ya siku chahe Shingai aligundulika kuwa ni mjamzito. Muda mfupi alijifungua mtoto wa kiume ambaye si Sope(Zeruzeru) tena, bali alikuwa kama watoto wengine. Sekai alijawa na furaha na kujisemea moyoni, ***"kumbe Takadini ni rijali".***

Tendai alimshukuru sana Sekai na alimwambia kuwa yeye na Takadini wameleta mabadiliko kijijini hapo hasa katika kumdharau mtu aliye na ulemavu kama Takadini. Sekai alimshukuru rafiki yake na alipanga kurejea na familia yake katika kijiji chake cha nyumbani.

Je, taswira hiyo ya mila dhidi ya Masope(mazeruzeru) ingepokelewaje na jamii ya mama yake Takadini pindi watakaporejea?

**C. MAUDHUI**

**DHAMIRA KUU:**

**Ukombozi wa kiutamaduni**

Dhamira kuu katika riwaya hii ni ukombozi wa kiutamaduni.

Mwandishi anaonekana kusukumwa na tatizo la jamii kukumbatia mila na desturi zilizopitwa na wakati.

Katika jamii kuna mila na desturi zimetumika kama chombo cha ukandamizaji. Mila na desuri zimeelezwa kutumika kukandamiza wanawake na watooto katika vipengele vifuatavyo:

1. Ndoa
2. Mirathi
3. Uhai
4. Maamuzi
5. Mgawanyo wa kazi
6. Mgawanyo wa mapato na umilikaji wa mali
7. Elimu
8. Utu

Waandishi wengi kama vile Ebrahimu Hussein katika tamthiliya yake ya *Kwenye Ukingo wa Thim,* Penina Mhando katika *pambo,* N.k. wamejadili namna baadhi ya mila na desturi zinavyotumika katika ukandamizaji wa wanawake, watoto na walemavu.

Mwandishi wa riwaya hii, anaonesha namna mila na desturi mbaya zinavyotumika kuwakandamiza wanawake na makundi mengine ya wasiojiweza. Mfano wa mila na desturi zinazotishia uhai, haki na maisha ya watoto walemavu kama Takadini, kijana aliyejaliwa akiwa zeruzeru ambaye jamii yake iliazimia kumuua siku ya pili baada ya kuzaliwa kwake. Katika ukuraasa wa 19 mwandishi anasema.

*"Sekai alimpenda Makwati – siku zote alimpenda . Na sasa anamuacha aamuliwe na wazee kwa sababu ameshindwa kumpatia aina ya mtoto aliyetaka… mtoto huyu asiye na msaada alimtegemea yeye kama tu alitaka aishi. Katika kijiji hiki, kati ya watu wa Makwati, Zeruzeru hakuwa na nafasi"*.

Kauli hii inathibitisha kuwa jamii haikuthamini mtu ambaye alikuwa ni mlemavu. Wazee wa kijiji ndiyo walikuwa wasimamizi wa mila na desturi hizi za kikatili. Takadini kama mlemavu maisha yake yaliokolewa na mama yake ambaye aliamua kuvunja shina na miiko iliyowekwa ili kuangamiza Zeruzeru.

Uonevu wa mila na desturi huakuwalenga watoto tu, bali ukandamizaji uliwagusa pia wanawake katika jamii. Mwandishi anamuonesha Sekai kama mhanga wa mila na desturi zinazokandamiza wanawake. Baada ya kuzaa mtoto aliyekuwa na ulemavu (zeruzeru) na kukataa mwane asiuawe, Sekai naye kifo kilimkabili kwa mujibu wa mila na desturi za kabila lao. Haya yanaweza kuthibitishwa na maelezo ya Makwati akimtahadharisha Sekai, alisema,

***"Lakini Sekai kama wataamua mtoto auawe, hata nawe utauawa kwa sababu ya kupinga sheria za kale".***

Kauli hii inaonyesha namna wazee walivyotumia mila na desturi 'katili' kutoa hukumu kubwa ambayo Mungu pekee angestahili kuitoa na si mwanadamu yeyote. Hukumu ya kukatisha maisha ya binadamu ni ya ukatili. Wazee waliazimia kutekeleza sheria, mila na desturi za kabila lao bila kujali madhara yake.

Je, haitupasi sasa kuleta ukombozi wa kiutamaduni kwa kurekebisha baadhi ya mila na desturi zilizopitwa na wakati? Wakati umefika sasa kwa jamii kuliona hilo. Kuwa tayari kuzifanyia marekebisho baadhi ya mila ambazo zinatuumiza wenyewe. Kwa gharama yoyote ile tunapaswa kutetea haki, uhuru na utu wa watu wote dhidi ya mila na desturi zinazokiuka haki, uhuru na utu wa mtu.

Mwandishi anasema,

***Sekai alikwishaamua: lazima aondoke asubuhi itakayofuata.Sekai hakuwahi kutenda jambo kinyume na Makwati wala mila zao, isipokuwa kwa hili, kulilia uhai wa mtoto wake. Uamuzi wake ulikamilika kwa usahihi na ushwari, sifa ambazo hakujua kuwa alikuwa nazo."***

Jamii inapaswa kuwa jasiri kama Sekai aliyeamua kuvunja, sheria zilizokuwa zimepitwa na wakati.

Mwandishi anaonesha pia namna mila na desturi zinavyoingilia hata masuala ya ndoa. Mwanamke alinyimwa haki ya kuchagua mtu anayempenda kuwa mume wake, kama inavyoonekana kwa Shingai. Hata kivyo Binti huyu pia alipigania haki na uhuru wake kwa kumkataa mchumba aliyechaguliwa na wazazi wake. Katika kutetea uhuru na haki yake, Shingai anasema,

***"Huyu ndiye mtu ninayetaka aniowe. Hakuna aliyeniuliza kama nampenda Nhamo. Wewe na baba mlikuwa na hamu ya kuniozesha katika familia ya Manyamombe hata matakwa yangu hayakusikilizwa. Sasa nimechagua . Nakuomba msamaha wako mama, unaweza ukaniua kama ukitaka, lakini katu kwa Nhamo siendi hata kama angekuwa nami sasa".(uk118).***

Je, ni nani ataleta mabadiliko kama siyo sisi wenyewe tunaoathirika na milahizi mbaya? Shingai anatuonesha njia kuwa ukombozi wowote ule ni lazima tuwe tayari kujitoa mhanga kama alivyofanya Sekai na Shingai ambao walileta mabadiliko katika jamii zao. Tendai anashuhudia hilo kwa kusema.

***"….Sekai. Wewe na Takadini mmebadilisha mambo mengi kijijini hapa. Kwa sasa, sifikirii kwamba kuna mtu yeyote atakayekuwa na moyo wa kuharibu watoto wachanga Masope au wenye ulemavu. Ahsante nyingi kwako na Takadini na kwa baba Chivero. Ndiyo hurejea huko baada ya muda mrefu hivi huenda kukawapa funzo kama hili pia….."(uk.126).***

Kwa ujumla mwandishi amejaribu kuonesha baadhi ya mila na desturi zenye walakini katika jamii nyingi za kiafrika na ameonesha njia za kuondoka nazo ili kuleta ukombozi.

**Dhamira Ndogondogo**

Katika riwaya hii, kuna dhamira mbalimbali ambazo zimeijenga dhamira kuu. Dhamira hizo ni pamoja na hizi:

i. Mapenzi

ii. Ndoa

iii. Imani potofu

iv. Upendo

v. Ujasiri

vi. Umoja na mshikamano

vii. Elimu

viii. Nafasi ya mwanake

Dhamira hizi zote zinajenga dhamira kuu ya ukombozi wa kiutamaduni kwa kuonesha sheria, mila, na deturi zinavyogusa dhamira zote hizo.

i. **Mapenzi**

Mapenzi ni dhamira ambayo imejadiliwa katika riwaya hii ya *Takadini*. Mwandishi amejaribu kuonesha kuwa katika jamii kuna aina mbili ya mapenzi. Mapenzi ya dhati na mapenzi yasiyo ya dhati. Mwandishi anaona kuwa mapenzi ya dhati ndiyo humfanya mtu aheshimu wengine, ajali haki na utu wa mtu, ajisikia uhuru na kukwepa kupandikiza chuki na badala yake humfanya ahimize ushirikiano, umoja na upendo.

Katika riwaya hii ya *Takadini* tunaona mapenzi ya dhati kati ya Takadini na mama yake. Takadini na mzee Chivero, Takadini na Shingai, Sekai na Pindai, na Sekai na mzee Chiro.

Mapenzi ya Sekai kwa Takadini (mwanae) yalikuwa ya dhati kwa sababu Sekai alikuwa radhi kufa ilimradi mwanae Takadini asipate madhara. Sekai alimlinda mwanae wakati wote, Sekai alikabiliana na mumewe katika hali ya kumlinda Sekai anasema,

***"Ni mtoto wangu wa kwanza niliyemsubiri kwa miaka mingi. Siwezi kukubali kumpoteza. La humataki, nirejeshe kwetu au hata msituni, lakini usije kunilazimisha nitengane naye. Nitajitoa mhanga kwa ajili yake".***

Haya ni mapenzi ya dhati ya mama na mtoto wake. Mama alijitoa mhanga kumlinda mwanae katika hali ya hatari. Alijua fika nini kitamkabili mbeleni kwa kufanya mambo kinyume na taratibu za kabila lake.

Mapenzi ya dhati yanajitokeza kati ya Takadini na Shingai. Takadini ni kijana mwenye ulemavu wa aina mbili (mguu na ni zeruzeru) hivyo alitengwa na jamii.

Katikati ya upweke wake ambao umetokana na ulemavu anapumzishwa machungu hayo na binti aitwae Shingai . Shingai alikuwa na mapenzi ya dhati kwa Takadini. Ingawa wazazi wake walimkataza na kumchagulia mchumba, Shingai alikuwa na msimamo na kuelezea wazi hisia zake kwa wazazi wake. Katika hali ya kutetea penzi lake la dhati Shingai anasema,

***"Huyu ndiye mtu ninayemtaka anioe. Hakuna aliyeniuliza kama nampenda Nhamo. Wewe na baba mlikuwa na hamu ya kuniozesha katika familia ya Mnyamombe hata matakwa yangu hayakusikilizwa. Sasa nimechagua. Nakuomba msamaha wako mama, unaweza ukaniua kama ukitaka, lakini katu kwa Nhamo siendi hata kama angekuwa namI sasa."(uk118).***

Uamuzi huu unadharirisha kuwa mapenzi ya dhati hayachagui rangi, kabila, mali au vitu vingine. Mbali ya kukanwa na wazazi wake Shingai hakubadili msimamo wake. Alitunga mimba na kuzaa mtoto. Shingai anadhihirisha penzi la dhati kwa Takadini.

Mapenzi mengine ya dhati ni kati ya mzee Chivero na Sekai. Wakati wa kutoroka, Sekai anakutana na mzee Chivero na anamweleza mkasa wote uliompata na lengo lake yeye kutoroka. Mzee Chivero anamkaribisha Sekai katika kijiji chake na anamtambulisha kwa Mtemi wao. Mzee Chivero ndiye aliyekuwa, mlezi mkuu wa Sekai na mtoto wake hadi kifo kilipomchukua. Hivyo inaonesha wazi kuwa mzee Chivero alikuwa mkarimu na mpole kwa wageni na hivyo alikuwa na mapenzi ya dhati.

Mapenzi kati ya mzee Chivero na Takadini vilevile yalikuwa ya dhati. Mzee Chivero alimpenda sanaTakaini kwani alimfundisha mambo mbalimbali kama vile uwindaji, alimfundisha jinsi ya kufahamu dawa za mitishamba na matumizi yake mbalimbali. Kila wakati Takadini alipokuwa na huzuni alifarijiwa na mzee Chivero.

Vilevile mapenzi kati ya Sekai na Pindai yalikuwa ni ya kweli. Pindai alikuwa mke mwenza wa Sekai na alimpenda sana kuliko wake wenzake ambao kila wakati wakilimsengenya Sekai kwa sababu ya kutopata mtoto. Lakini wakati wote Pindai alifariji Sekai kutokana na kusengenywa na wake wenza.

Mapenzi mengine ya kweli ya dhati ni kati ya Sekai na Tendai. alikuwa mke wa mwisho na mdogo wa Mtemi Masasa. Tendai ndiye alikuwa rafiki mkubwa wa Sekai na aliweza kushirikiana katika shughuli mbalimbali za kijamii.

Kwa upande wa mapenzi ya oungo yasiyo ya dhati nayo yamejadiliwa katika riwaya hii, kwanza mapenzi ya uongo ni kati yam zee Makwati kwa mtoto wake Takadini. Mzee Makwati alikasirishwa na kitendo cha kuzaliwa takadini akiwa Zeruzeru, kutokana na kitendo hicho mzee Makwati alifuata mila na alitaka Takadini auawe kwani aliona kuzaliwa kwake ni kama kuleta balaa katika familia yake, lakini mama yake Sekai alitoroka na mtoto ili asiuawe.

Mapenzi ya uongo ni kati ya mzee Makwati na Sekai baada ya kujifungua mtoto Zeruzeru. Mzee Makwati alikasirishwa kwa kuona mtoto yule na alimshutumu mkewe kuwa alitembea na wanaume wengine hivyo alivunja mila na desturi zao. Sekai aliumizwa sana na tuhuma hizo maana alijiona hana maana tena mbele ya mumewe na alijihisi ametelekezwa zaidi wakati huo.Kutokana na kitendo hicho cha kutelekezwa na mume wake sekai aliamua kutoroka.

Mapenzi mengine ya uongo ni kati ya Dadirai na Rumbiozai kwa Sekai, hawa walikuwa ni wake wenza wa Sekai na waliishi maisha ya kumsengenya Sekai kila wakati. Hawa hawa kuwa na mapenzi ya kweli kwa Sekai, kwani waliishi kwa kumbaguana Sekai walikuwa na wivu naye na matokeo yake kukawa na mvurugano wa kifamilia.

ii. **Ndoa**

Ndoa ni makubaliano kati ya watu wawili wapendanao ambao wameamua kuishi kama mume na mke. Maamuzi ya juu ya nani awe mume au mke ni juu ya wale wapendanao. Mila na desturi zimeingilia ndoa za watu katika jamii madhara yake yamekuwa makubwa: Ndoa zimevunjika na hata kukosekana kwa amani.

Katika riwaya hii , Shingai alilazimishwa kuolewa na Nhamo. Kitendo hiki hakikumfurahisha Shingai. Alisema

***“Ama! siyo kama ninamchukia Nhamo, la hasha. Isipokuwa sidhani kama nitakuwa na furaha kuishi naye.” (uk.110).***

Ingawa mila na desturi ziliwabana watoto wa kike kuwa na uhuru lakini ukweli ni kwamba mila hizo zilisababisha ndoa nyingi kutokuwa na furaha. Shingai anasisitiza.

***“Sikumwambai kufanya hivyo na simtaki. Nataka waniache peke yangu ili naimue mwenyewe…..” (uk115)***

Pia mwandishi wa riwaya hii amegusa suala la ndoa za mitala. Mwandishi ameonesha kuwa ndoa za mitala ni desturi ambayo jamii inapaswa kuachana nayo.

Mwandishi ameonesha namana ndoa za mitala zinavyochangia kuleta mifarakano katika familia. Mfano mzuri ni namna wake zake Makwati walivyokuwa wakiishi kwa kusengenyana na uadui mkubwa ulizuka miongoni mwao. Haya yanajitokeza (uk 1- 20). Katika (uk.3) Pindai anasema,

***"Si ajabu wale wawili wanahofu utapata mtoto wa kiume…. Wanaamini kuwa Makwati atahamishia mapenzi na uangalizi kwa mtoto huyo. Pia, mume wetu atazidisha mapenzi kwako. Aidha wana imani kwamba umepa dawa Makwati ili akupende wewe zaidi ya mwingine."***

Makwati alikuwa na wake wanne ambao walioishi katika maisha ya uhasama sana. Walitukanana na kusingizia mambo mabaya kama uchawi. Kimsingi, penzi haligawiki. Wanajamii wanapaswa kuachana na mila hiyo mbaya ya kuishi katika ndoa inayohusisha mke zaidi mmoja.

iii. ***Dhana potofu***

Katika jamii kumekuwa na hali ya watu kuamini vitu ambavyo havina msingi. Watu wamekuwa wakitelekeza walemavu wa viungo vya mwili, Zeruzeru na hata mapacha kwa kuamini kuwa miungu yao isingefurahia kuwaona watoto hao wenye ulemavu katika jamii. Mwandishi wa riwaya hii hakufumbia macho tatizo hili, amelizungumzia kwa kina na kuwaonyesha njia kuwa mambo ambayo walidhani kuwa yamewezekana. Ziki ni mfano wa watu ambao wamekuwa na dhana potofu maishani mwao. Sekai na Takadini (Zeruzeru) wanapokaribishwa katika kijiji cha watu wa Masasa, Ziki alipinga kuwepo kwao hapo. Anasema,

***"Sote tunajua mila za mababu zetu katika kila koo na kijiji. Watoto kama huyu lazima wauawe, wenye ulemavu lazima wauawe, na hata pacha mmoja lazima auawe".***

Hii ni kauli ya Ziki ambayee alirejea mila na desturi potofu kuhalalisha dhana potofu alizonazo dhidi ya walemavu. Huyu si mtu ambaye ana dhana potofu, wapo wengi sana. Katika riwaya hii, wapo wazee wengine kama Mapunzure ambaye katika ukurasa 35 alisisitiza, ***"Mtoto lazima auawe."***Pia kama mzee Manyamombe ni mmoja wa watu wenye imani potofu juu ya watoto walemavu.

Kuna dhana potofu pia kuhusu jinsia ya watoto. Wazazi wengi wamekuwa na upendeleo zaidi kwa watoto wa kiume kama ilivyo kwa Makwata na wake zake.

Sekai anapopata ujauzito anatamani mumewe kuwa huenda ujauzito alionao ni wa mtoto wa kike. Makwati aling'aka,

***"unasemaje we mwanamke?... Hapa tayari tuna idadi kubwa ya wanawake. Mimi nanyong'onyea kwa kuomba mtoto wa kiume."***

Kila mtoto anayezaliwa ana haki ya kupendwa bila kujali jinsia yake.

Dhana potofu katika ni tatizo linalopaswa kuondolewa kwa kutoa elimu sahihi katika jamii ili kuepuka matatizo yasitokee kama mzee Chivero na mtemi Masasa walivyofanya kwa watu wao.

iv. **Nafasi ya mwanamke katika jamii na ujinsia**

Ujinsia ni majukumu ya kijamii ambayo hupewa mwanaume au mwanamke kwa kuangalia mahusiano ya mtu mume na mtu mke. Ni wajibu wa mume na mke katika jamii.

Katika jamii nyingi kiafrika kumekuwa na matatizo ya jinsia kama vile kuozesha kuwa watoto katika umri mdogo na kulazimishwa kuolewa au bila ridhaa, maamuzi yote yanayohusu jamii na familia hufanywa na wanaume, watoto wa *kike wamekuwa hawapewi thamani sawa na watoto wa kiume na suala zima la* malezi amekuwa akiachiwa mama peke yake.

Katika riwaya hii, mwandishi ameonesha matatizo ya kijinsia. Kwa mfano, Tendai alilzaimshwa kuolewa na mtemi Masasa na alikuwa na umri mdogo. Sekai anapomuuliza Tendai kama alimpenda mzee Masasa, Tendai alijibu,

***“Ni heshima kuwa mke wa mtemi mwenye nguvu kama Masasa. Lakini namchukulia kama baba yangu kuliko mume wangu”…(uk.47)***

Kauli hii inathibitisha kuwa Tendai hakufurahia kuolewa na mume mwenye umri mkubwa sawa na baba yake. Hii ni kasoro kubwa sana katika suala zima la ndoa. Tendai anaendelea kusema,

***“Wake wenzangu ni kama mama zangu. Siku zote wananitazama mimi, wananikaripia, na mabinti zao ambao ni wa umri wangu hunicheka kwa dharau kila wanitazamapo…” (uk.47)***

Mahusisano ya kijinsia katika jamii yamekuwa katika hali ya kukandamiza zaidi, mwanamke na kumpendelea mwanaume. Katika riwaya hii, mwandishi ametuonyesha tatizo jingine la kijinsia kuwa ndoa za mitala. Katika suala zima la ndoa mitala tunaona mwanaume anapewa fursa ya kuoa mke zaidi ya mmoja. Fursa hiyo haionekani kwa mwanamke. Sababu kubwa inaonekana kuwa mwanamke ni kama chombo cha starehe. Kwa mfano Makwati alikuwa na wake wa nne. Mtemi Masasa alikuwa na wake wengi pia. Hapa mwanaume ndiye mwenye nguvu zaidi.

Kuhusu nafasi ya mwanamke mwandishi amemuonyesha mwanamke kama mzazi na mlezi wa watoto na familia kwa ujumla. Kwa mfano, Sekai ni mama mzazi wa Takadini. Alimlea na kumlinda wakati wote mpaka alipopata mke (Shingai). Mashangai alimzaa Shingai na kumlea wakati wote. Kazi ya kulea ilionekana ni ya mwanamke na si mwanaume. Mashangai anasema,

***“Shingai sitakuita mwanangu tena, umefanya kitu gani hiki? Hivi ndivyo bibi yako na tete wako walivyokufundisha?...(uk118).***

Kauli ya mama mzazi wa Shingai inathibitisha kuwa malezi ya mtoto waliachiwa akina mama, mama wazazi, Shangazi na bibi. Haya si mawazo ya wanawake kuona ni jukumu lao tu, pia hata wanaume walikuwa na dhana hiyo hiyo. Mfano, Baba yake Shingai alimhoji kewe kuhusu malezi ya Shingai kwa kusema,

***“Hukumfundisha mwanao maana ya tendo hilo, we?...(uk96)***

Mwanake amechorwa pia kama mwanamapinduzi. Haya yanaweza kuthibitishwa na wanawake wawili ambao ni Sekai na Shingai. Ni wanawake walioleta mabadiliko katika jamii kwa mfano, Sekai na mwanamke wa kwanza kuvunja sheria za mila na desturi za jamii yake kwa kukataa Takadini(Zeruzeru) asiuawe na akamlinda wakati wote.na alileta mapinduzi akiwa uhamishoni. Rafiki yake Tundai anasema,

***“Kwa sasa ,sifikiri kwamba kuna mtu yeyote atakayekuwa na moyo wa kuharibu watoto wachanga, Masope au wenye ulemavu…”***

Shinga naye anaonekana ni mwanamapinduzi kwa kukataa kuchaguliwa mtu wa kumwoa. Aliamaini kuwa ndoa ya kweli inahusisha watu wawili waliopendana na ambao wamechaguana. Shingai anasema.

***“Amai, siyo kama ninamchukia Nhamo la hasha. Isipokuwa sidhani kama nitakuwa na furaha kuishi naye”(uk.110)***

Anaendela kusema,

***“Huyu ndiye mtu ninayetaka anioe. Hakuna aliyeniuliza kama nampenda Nhamo… lakini katu kwa Nhamo siendi hata kama angekuwa name sasa”…118***

Shingai alisimamia msimamo wake na hata akaamua kuolewa na Takadini na kupata mtoto ambaye hakuwa Sope.

Kwa ujumla, matatizo ya kijinsia yanachangiwa sana na athari za utamaduni (mila na desturi) katika mfumo wa maisha ya jamii. Jamii kuongozwa kwa mfumo unaoegemea jinsia moja ndiyo chanzo cha ukandamizaji wa kijinsia. Jamii zinazofuata mfumo dume, huwa na mila zinazokandamiza wanawake zaidi. Ukombozi wa kiutamaduni utaleta usawa wa kijinsia katika jamii.

v. **Umoja na mshikamano**

Umoja ni ile hali ya kuwa pamoja : ushirikiano na mshikamano ni ile hali ya watu kuwa na msimamo na ushirikaino wa karibu katika kutimiza azima Fulani.

Mwandishi wa riwaya hii ameonesha mbinu mojawapo katika kupambana na mila na desturi potofu ni kwa jamii kuwa na umoja na mshikamano. Umoja na mshikamano ni silaha katika mapambano haya. Mshikamano mzuri alionesha mzee Chivero, Tendai, mtemi Masasa ulisaidia kumlinda Takadini dhidi ya wanyanyapaa na hatari ya kupoteza maisha. umoja na mshikamano uliendelea kukua zaidi pale Shingai alipoamua naye kuonesha msimao kwa kukataa kufuatia mila na desturi zilizowabagua walemavu, kuwalazimisha wanawake kuolewa kwa nguvu na hivyo kuamua kuolewa na Takadini ambaye alikuwa ni mlemavu wa mguu na pia alikuwa zeruzeru.

Katika hali ya ushindi dhidi ya mila potofu, mzee Makuru anasema,

***"Nilimwambia hivyo….. Sasa tunajua ni kipi ambacho mizimu yetu haikuruhusu kutafuta, Sope hawezi kuzaa Sope! Naamini tutajifunza somo hili, fuvu la nyani limekuwa kijiko kwa mlo wa mahindi: vizazi vijavyo vitatushukuru kwa kile tulichokifanya hapa kijijini."***

Katika mapambano yote yote yale, umoja na mshikamano husaidia sana katika kupata ushindi. Wahenga walisema umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Umoja na mshikamano wa Shingai, Pindai, Chivero, Masasa, Sekai Takadini, Makaru na Tendai ulisaidia kuleta mabadiliko makubwa ya kiutamaduni katika jamii yao.

vi. ***Ujasiri***

Hii ni hali ya kukabili jambo bila ya hofu, uhodari, ushujaaa. Katika riwaya hii ya Takadini mwandishi ameonesha ujasiri kama mbinu muhimu katika ukombozi wa kiutamaduni. Pengine ujasiri siyo mbinu inayotumika katika ukombozi wa kiutamaduni tu, bali ni mbinu ambayo imetumika katika aina zote za ukombozi. Mathalani katika riwaya hii tunakutana na Sekai, mwanamke anayeamua kupambana na mila na desturi ambazo ziliwakandamiza wanawake. Baada ya kumzaa Takadini aliamua kumtorosha mwanawe ili asiuawe. Alimkabili mumewe kuwa alitaka kumuona mwanawe akiwa hai. Na hata anapokuwa uhamishoni.

Shingai ni mwanamke mwingine ambaye alionesha ujasiri mkubwa katika harakati za kujikomboa katika makucha ya mila na desturi zilizokuwa zikiwakandamiza wanawake na watoto. Shingai aliamua kuolewa na Takadini (Kijana mlemavu) na kupuuza uchaguzi wa wazazi wake kwa kuwa aolewe na Nhamo. Kwa ujasiri kabisa Shingai anasema,

***"Huyu ndiye mtu ninayetaka anioe. Hakuna aliyeniuliza kama nampenda Nhamo. Wewe na baba mlikuwa na hamu ya kuniozesha katika familia ya Manyamombe hata matakwa yangu hayakusikilizwa…. Sasa nimechagua."***

Shingai aliendelea nma ujasiri wake huohuo hat baada ya baba yake kutoa kauli za kumkana kuwa mwanae kwa sababu ya kuolewa na Sope (zeruzeru).

Ujasiri ni nguzo muhimu sana katika mapambano dhidi ya mila na desturi potofu katika jamii. Ni lazima tuondoe hofu na woga ili tubadili hali ya ukandamizaji na uonevu ndani ya jamii kwa kunyoshea vidole mila mbaya. Kwa ujumla, malezi ya waatoto ni jukumu la wazazi wote. Mtoto ambaye helelewa vyema na baba na mama ndiye huwa na tabia bora. Jamii inapaswa kutambua kuwa malezi ya baba na mama ni haki ya mtoto, mila ambazo haziendaini na malexi bora hatuna budi kuachana naazo.

vii. ***Malezi ya watoto***

Malezi ni makuzi ya watoto. Ni njia watumiayo wazazi katika ukuzaji wa mtoto kwa kutarajia kufuata tabia na mwenendo unaostahiki.

Malezi ya watoto yanapaswa kusimamiwa na wazazi wote wawili. Baba na mama wanapaswa kushirikiana kwa pamoja katika kulea watoto wote ili watoto wawe na tabia njema. Mila na desturi katika jamii zinazofuata mfumo dume zinakuwa zikaachwa wanawake peke yao kuwa ndiyo walezi wa watoto. Wanawake ndiyo wanawajibika na malezi ya watoto kwa wanaume zao. Mfano mzuri tunaweza kuupata katika riwaya hii ya Takadini.

Malezi anayopa Shingai ni mama, bibi na shangazi. Baba yake Shingai mzee Nhariswa anamwajibisha mkewe kwa kumpiga kwa sababu Shingai anaonekana kutofuata mila na desturi katika ukurasa wa 119 mzee Nhariswa ansema

***"umefanya nini sasa wewe mwanamke? Tangu mwanao alipopeleka maji kwa Sekai ungefuatilia kujua anachokifanya .... Uliona dalili, kwa nini hukutafuta dawa…"***

Mwandishi anasema kuwa Nhariswa alimpiga mkewe kichwani na usoni mara kadhaa, lakini mkewe hakuweza kujibu. Kitendo hiki kinadhihirisha walakini wa baadhi ya mila na desturi kuhusu suala zima la malezi katika kajamii.

***"Hivi ndiyo bibi yako na tete wako walivyokufundisha?" (uk118)***

Mama huyu naye anaona malezi ya watoto yapo mikononi mwa wanawake na si jukumu la wazazi wote.

***"....Mume wangu unasemaje? Kama mtoto wetu ni sope, nitahuzunika sana, lakini nina uhakika atampata wa kumpenda kama nilivyokupenda wewe. Acha kuwa na shaka nimembema mimi na ninaelewa atakuwa kama watoto wengine. Njoo mume wangu tulale sasa."***

Mapenzi ya dhati ni muhimu sana katika ukombozi wowote ule katika jamii.ukombozi wa kitamaduni unawezekana kama kweli watu watakua na mapenzi ya dhati.

***Ujumbe***

***Mwandishi wa riwaya hii anatoa ujumbe ufuatao kwa jamii:***

i. Walemavu wana haki ya kuishi sawa na watu wasio kuwa na walemavu.

ii. Malezi ya watoto yanapaswa kuwa kusimamiwa na wazazi wote wawili ili kujenga jamii inayoheshimika.

iii. Ndoa ni maamuzi ya watu wawili wapendanao na hayapaswi kuingiliwa na mtu yeyote.

iv. Ujasiri, umoja na mshikamano ni mbinu muhimu sana katika ukombozi wa kiutamaduni.

v. Jamii inapaswa kuachana na mila na desturi potofu ili kuondoa ukandamizaji na unyanyapaa kwa watu wenye ulemavu.

***Mtazamo wa Mwandishi***

Mwandishi wa riwaya ya Takadini anaoneka kuwa na mtazamo wa kiyakinifu.

Mwandishi anachukulia matatizo yanayotokana na mila na desturi kuwa yanaweza kutatuliwa na watu wenyewe kwa kuchukua hatua za makusudi kabisa katika kujikomboa kiutamadunio kama anavyofanya Sekai, Shingai, Masasa na mzee Chivero. Mwandishi ameweza kuonyesha waziwazi matatizo hayo ya kiutamaduni kuwa ni ukandamizaji wa kijinsia, uonevu kwa walemavu, n.k. Mwandishi pia ameonesha njia za kujokomboa kiutamaduni kuwa ni umoja, mshikamano, elimu na ujasiri.

Kwa ujumla mwandishi ameainisha matatizo yote ya kiutamaduni na kuweza kuonesha masuluhisho ya matatizo haya, hivyo mwandishi anamtazamo wa kiyakinifu.

***Msimamo wa mwandishi***

Mwandishi ana msimamo wa kimapinduzi kwani ameeleza udhaifu wa baadhi ya mila na desturi zetu. Mwandishi ameonesha madhara ya kuendela kukumbatia mila hizo na akaonyesha hoja ya kufanaya mabadiliko ya badhii ya mila hizo ili kuleta uhuru, haki, usawa na kutahmini utu wa watu wote.

***Falsafa ya Mwandishi***

Mwandishi anaelekea kuamini kuwa binadamu wote ni sawa hata kama kuna tofauti za kimaumbile. Kila binadamu ana haki ya kuishi. Kwa ujumla mwandishi ni muumini wa haki na usawa.

***Migogoro***

Katika riwaya hii kumejitokeza migogoro mingi ambayo imetokana na mgogoro wa kiutamaduni.

**Mgogoro wa kwanza**: Mgogoro wa kiutamaduni kati ya Mkwati na Sekai. Mgogoro huu ulizuka mara bada ya Sekei kuzaa mtoto ambaye ni Sope (Zeruzeru). Kutokana na mila na desturi, mtoto ana ulemavu wowote ule alipaswa kuuawa hivyo Takadini alipaswa kuuawa siku ileile aliyozaliwa. Suala la kuuawa kwa Takadini hakuliafiki Sekai na hivyo kulipinga kwa nguvu zote.

Suluhisho la mgogoro huu ni kwamba Sekai alitoroka na kuishi uhamishoni hadi Takadini alipokua na kuoa na kupata mtoto wa kiume ambaye si sope ndipo aliporudi kijijini kwao.

**Mgogoro wa pili :** Ni kati ya Shingai na wazazi wake. Wazazi wa Shingai walimchagulia mume wa kumuoa Shingai. Kijana aliyependekezwa aliitwa Nhamo. Jambo hili halikumfurahisha Shingai hivyo alikataa kuolewa na Nhamo na hivyo kufanya wazazi wake kukasirishwa sana kiasi cha kumueleza kuwa asiwatambue kama ni wazazi wake.

Suluhisho la mgogoro huu ni kwamba Shingai aliamua kutorokea kwa Takadini (kijana aliyempenda sana) na kuolewa na Takadini.

**Mgogoro wa tatu**: Ni wa kinafsia ambao unajitokeza kwa Tendai. Tendai aliozwa kwa mzee Masasa ambaye alikuwa na umri wa baba yake na wakewenza walikuwa umri wa mama yake na mabinti wa Mtemi Masasa walikuwa umri sawa na Tendai. Tendai alishindwa amuite mume wake au baba yake, alishindwa awaite wake wenza au mama zake. Hakuwa amani moyoni. Alikuwa katika hali ya upweke mno.

Suluhisho la mgogoro huu ni kumtafuta rafiki ambaye ni Sekai ili wasaidiane mambo mbalimbali.

**Mgogoro wa nne:** Ni mgogoro wa kijamii. Mgogoro huu ulitokea kati ya Shingai na Chido. Mgogoro huu ulimhusisha Nhamo kwani Chido alidhani Shingai atolewa na Nhamo na kumfanya awe mkemwenza. Mgogoro ulifanya wanawake hawa wawili watupiane maneno au vijembe.

Mgogoro huu ulisuluhishwa kwa Shingai kueleza msimamo wake wa kutomtaka Nhamo awe mme wake.

Pia Shingai alipoolewa na kuzaa na Takadini ilisaidia kupunguza uhasama huo.

**Mgogoro mwingine ni wa kijamii**: Huu ni mgogoro wa tano ambao unahusisha Takadini na Nhamo. Nhamo alikuwa ni mgomvi, mbaguzi jambo ambalo alililifanya kwa Takadini. Uhasama zaidi uliongezeka pale Shingai alionesha

mapenzi Kwa Takadini Na kumkataa Nhamo. Hakuna suluhisho linalotolewa katika mgogoro huu.

**FANI**

1. ***Muundo***

Katika riwaya hii ya Takadini mwandishi ametumia muundo wa msago (moja kwa moja). Visa na matukio katika riwaya hii vilipangwa kwa mfululizo wa moja kwa moja na kazi nzima ina jumla ya sura kumi na tatu. Kwa ujumla muundo wa riwaya hii ni wa moja kwa moja kwani mwandishi anatuonesha namna Sekai alivyopata mimba, akazaa mtoto wa kiume ambaye ni sope(Zeruzeru), kisha anatoroka kwenda kuishi, uhamishoni, maisha ya Sekai uhamishoni, Takadini anakua na kupata mke aitwae Shingai na mwisho tunaona kijijini kwao.

1. **Mtindo**

Mwandishi ametumia mtindo wa masimulizi katika riwaya yake. Sehemu kubwa mwandishi amehadidhia mwenyewe kuhusu maisha ya Sekai na Takadini.

Vile vile kuna matumzi ya dayolojia katika sehemu chache. Mwandishi ametumia dayolojia kuonesha uahalisi wa kauli za wahusika wake. Mfano Dayolojia imetumika katika (uk.1)

***"Je, Na yule mbuzi wako uliopewa Na baba Makwati, amekupatia watoto wangapi?"***

***"Tangu nimpate ni miaka miwili tu na tayari ana watoto wawili nabado anatarajia mwingine".***

Haya ni majibizano kaati ya Dirai na Rumbidzai.

Nafasi zote tatu zimetumika. Nafasi ya tatu umoja ndiyo imetalawa katika sehemu kubwa ya riwaya. Kwa mfano:

- Nafasi ya I ------- "Ndiyo, Pindai, anaogopa……" - (uk.3)
- Nafasi ya II ----- "Unasemaje wewe mwanamke?''' (uk.4)
- Nafasi ya III ------ "Sekai alipofumbua macho yake……" (uk.5)

Kuna matumizi ya tanzu nyingine ndani ya riwaya. Mwandishi ametumia nyimbo. Kaatika ukurasa wa pili Rumbidzai aliimba,

***"Mashamba yote yamelimwa***

***Mbegu nazo zimepandwa***

***Zimechipua na kumea,***

***Sisi watatu tumepata mavuno yetu;***

***Mheshimiwa wetu amemiliki mavuno***

***Kwa mikono yake halisi***

***Kutoka mashamba yetu yote***

***Lakini ni kipi alichoambulia***

***Kutoka ardhi ile isiyomea kitu?..."***

Nyimbo nyingine zinajitokeza (uk34, 57, na 90)

Matumizi ya monolojia yamejitokeza pia katika riwaya hii: Mfano wa monolojia:

***"Hatimaye!" Sekai alijinong'oneza peke yake.***

***"Mababu zangu wamenitimizia ombi langu kuu. Sasa wake wenzangu wataniheshimu kama mke wa kwanza. Hata wakwe zangu watakoma kumwambai mume wangu anirejeshe kwetu. Nina hakika ya kijifungua mtotot wa kiume…." (uk1)***

Mwandishi pia ametumia mbinu ya hadithi ndani ya riwaya. Mbinu hii imejitokeza katika uk. 82 -84. Kwa ujumla, mwandishi amesheheneza mbinu mbalimbali za kimtindo katika kazi yake.

**Matumizi ya Lugha**

Lugha iliyotumika inaeleweka kwa wasomaji kuwa wengi. Mwandishi ametumia tamathali za semi, misemo na mbinu nyingine za kisanaa.

**a) Misemo na Nahau**

Katika riwaya hii kuna matumizi ya misemo na nahau mbalimbali. Misemo na nahau zimetumia kupamba lugha na pia kuonesha uzito wa ujumbe uliokusudiwa.

Kwa mfano:

*"Lakini mbwa huyu amepoteza meno yake yote". (uk31).*

Hii ni nahau zenye maana ya mtu kutoakuwa rijali tena. Mifano ya misemo ni:

***"Habari njema huchechemea kwa mguu mmoja, lakini mbaya hukimbia kama sungura." (uk.15).***

Msemo huu una maana ya kuwa habari nzuri hazienei haraka lakini zile mbaya huenea haraka sana. Mifano mingine ya misemo ni:

***"Pokea upewacho"...(uk10)***

***"…Maisha ni matamu"..(uk83)***

***"Kanga hawezi kutua juu ya bua la mtama…..(101).***

***"Mume ni kiungo kwa mwanamke.".(110).***

b) Tamathali za Semi

**Tashibihi:**

Mwandishi ameweza kulinganisha vitu kwa kutumia vuinganishi kama vile: kama,mfano wa, sawa na, nk

Kwa mfano:

- *Giza jepesi tu lilibaki ukutani kama mgeni asiyekaribishwa na asiyetaka kuondoka.(uk...5).*
- *Muda huenda polepole sana mithili ya mwendo wa kakakuona. (uk. 6)*
- *Mwanzo maumivu hayo yalitulizana sawa na mwisho wa sentensi ndefu. (uk.6).*
- *Mtoto alionekana mweupe sana na funza mkubwa (uk. 16)*

**Tashihisi**

katika riwaya hii ya Takadini mwandishi amevipatia vitu sifa walizonazo watu. Kwa mfano:

- *Ndege mbalilmbali wakiimba kukaribisha siku mpya. (uk. 5)*
- *Ubongo wake ulioathirika kwa mawazo uliufukuza usingizi. (uk. 17)*
- *Fikra zilizopingana zilijichomeka katika nafsi yake(uk. 17)*
- *Miaka mingi iliyomchakaza iliufanya uso uwe sawa na mlima uliomomonyoka ardhi. (uk... 20)*

**Mubaalagha:**

Kuna hali ya utiaji chumvi au chuku nyingi katika masimulizi ndani ya riwaya ya *Takadini*.

***"Mtemi Masasa na wenzake walimtazama Sekai, mcho yao yakipiga mahesabu. Kila mmoja aliridhika naye – tangu monifu nyuma ya miguu yake, mapaja yaliyojaa na hata matiti yake ya duara yaliyojaa maziwa".(uk.37).***

Je, ni kweli wanaume wote waliokuwepo walipiga mahesabu sawa kuhusu Sekai? Mwandishi ametia chumvi kuonesha mvuto tu wa Sekai.

**Ritifaa:**

Tamathali hii imetumiwa na baadhi ya wahusika kwa kuzungumza nakitu au mtu ambaye husikika katika fikra.

Kwa mfano: Sekai anasoma;

*"Hatimaye! Mababu zangu wamenitimizia ombi langu kuu…."(uk.1).*

pia katika ukurasa wa 107 manyamombe anasema,

*"...Njoo,mpendwa Chivero,umezurura milimani na msituni kwa muda mrefu...*

*Tusamehe kwa kukuacha mbalimbali …. Njoo rejea nyumbani…. Kunywa pombe hii ….”*

Wahusika wote wawili ( Sekai na Manyamombe) walizungumza na watu ambao hawaonekani. Mbinu hii ndiyo tunayoiita Ritifaa.

**Dhihaka**

Kuna matumzi ya tamathali zenye kunesha dharau na yenye lengo la kumweka mtu katika hali duni kupita kiasi, lakini kwa mbinu ya mafumbo.

Kwa mfano:

- *“Naamini alichobeba ni mtoto halisi, siyo dubwasha.” Haya maneno yalimlenga Sekai kwa kuwa siku zote waliamini hazai.(uk.2).*
- *Ha! Yawezekana hana tatizo lolote lile, labda alikunywa maziwa mengi wakati wa ujauzito….”*

Kauli hii ilitolewa kwa Sekai baada ya kubaini kuwa amezaa mtoto Sope.

**Tafsida:**

Mwandishi kwa kiasi kikubwa amezingatia utamaduni wa lugha ya Kiswahili. Ameweza kutumia maneno ambayo yanaficha ukali wa maneno. Hakutumia lugha ya matusi. Kwa mfano:

- *Akamshambaulia hata sehemu zake za siri. (uk.83)*
- *“A kajivuta karibu zaidi naye, chini ya gudza. Hawakuzungumza, wakafanya kile ambacho kilitokea kwa asili ya maumbile. Wakakata kiu ya hisia zilizowavuta pamoja miezi mingi”. (uk.117)*
- *“Walifanya tena tendo la ndoa, …”(uk. 117)*

**c) Mbinu nyingine za kisanaa**

i) ***Takriri****:* Kuna baadhi ya silabi, maneno na sentensi zimejirudia kwa lengo la kuonesha msisistizo.

Kwa mfano takriri imejitokeza katika (uk.62)

Pale Nhamo anaposema,

- *“Wewe ni Sope, sope, sope”*
- *“Najua, najaua” (uk.79)*

***ii) Mdokezo:***

Kuna hali ya kutatiza maneno bila kukamilisha sentensi katika riwaya hii.

Kwa mfano:

- *“Siku moja sijui lini …. Lakini hivi” (uk.75)*

- *“Sukuma mara moja tena…” (uk.125)*
- *Mtu mzima kama watu wengine na amea…..?*

**Nidaa:**

Kuna kauli ambazo zinaonyesha kushangazwa kwa jambo Fulani. Kwa mfano:

*“Ah, Ha! – (uk.118)*

*“Kumbe maisha ni matamu!” (uk83)*

**Tashititi:**

Hi ni mbinu ya kuuliza swali kwa jambo ambalo anafahamu jibu lake.

Kwa mfano:

*“Huenda atakuwa wa kike”. Sekai alisema bila dhamira kubwa.*

*“Unasemaje we mwanamke? Makwati aliongea kwa sauti kali.*

Swali analouliza makwati tayari jibu lake analo.

**Wahusika**

**A.Takadini**

- *Huyu ndiye mhusika mkuu wa riwaya hii.*
- *Ni mtoto wa kwanza wa Sekai.*
- *Ni mlemavu wa ngozi (Zeruzeru) n*a ana tatizo la mguu.

Kijana wa kiume.

- *Ni mchapakazi na mtu anayependa kujifunza.*
- *Ni mwenye huruma.*
- *Ni mtiifu.*
- *Ni jasiri.*
- *Ni mwanamapinduzi.*
- *Ni mhanga wa mila na desturi mbaya zinazobagua walemavu.*
- *Anafaa kuigwa na jamii.*
-

**B:Sekai**

- Huyu ni mhusika mkuu mwingine.
- *Ni mke wa kwanza wa Makwati.*
- *Ni mwanake mchapakazi.*
- *Ni mhanga wa mila na desturi zilizopitwa na wakti.*
- *Ni mwanamapinduzi.*
- *Ni mama mzazi wa Takadini.*
- *Ni jasiri.*
- *Ni mwenye huruma.*

- *Ni mwenye busara.*
- *Ni mvumilivu.*
- *Ni mnynyekevu.*
- *Ni mchapakazi.*
- *Ni mpole.*
- *Ni mama mzazi na mlezi mzuri wa familia*
- *Ni mama mwenye upendo.*
- *Ni mpishi mzuri wa chakula.*
- *Anafaa kuigwa na* jamii

**C: Makwati**

*Anafaa kuigwa na jamii.*
*Ni mkale.*
*Ni mwoga.*
*Ana upendo kwa mkewe.*
*Ni mume mwenye wake wanne.*
*Ni baba mzazi wa Takadini.*
*Ni mume wa Sekai.*

**D:Chivero**

- *Ni mzee wa makamo.*
- *Ni mganga wa kienyeji.*
- *Alikuwa mpiganaji katika vita.*
- *Mtu mwenye upendo.*
- *Ni mtu mwenye busara.*
- *Ni mshauri mkuu wa mtemi Masasa.*
- *Mpenda mabadiliko.*
- *Ana huruma.*
- *Ni mfanyakazi shupavu.*
- *Ni mzalendo.*
- *Ndiye aliyewapokea Sekai na Takadini.*
- *Anafaa kuigwa na jamii*

*E*:**Mtemi Masasa**

- *Ni mzee wa makamo.*
- *Ni mtemi wa kijiji cha watu wa Masasa.*
- *Ni mpole.*
- *Ni mcheshi.*
- *Ni mzee mwenye hekima*
- *Ana wake wengi.*
- *Ni mpiganaji wa vita.*
- *Ni mfugaji.*
- *Anafaa kuigwa jamii*

**F:Shingai**

- Anafaa kuigwa na jamii.
- Ni jasiri.
- Ni msichana mwenye msimamo.
- Ni jasiri.
- Ni mwanamapinduzi.
- Ni mke wa Takadini.
- Ni binti wa mzee Nheriswa.

  **G: Tendai**

- Ni mpole.
- Ni mwanamapinduzi.
- Ana upendo.
- Ni mkarimu.
- Ni mke mdogo wa mtemi Masasa.
- **H:Darai**

- Ni mke wa tatu wa Makwati.
- Ni mtu makali.
- Ni mpenda majungu.
- Ana wivu.
- Mbinafsi.
- Ni mama wa Chipo
- Ana mawazo potofu
- Ni mnafiki.
- Hafai kuigwa na jamii.
- 
- **I:Rumbidzai**
- 

- Ni mke wan ne na mdogo kabisa wa Makwati.
- Ni mtu mkali.
- Ni mpenda majungu.
- Ana wivu.
- Mbinafsi.
- Ana mawazo potofu.
- Hafai kugwa na jamii

**J:Manyamombe, Mukaru, Chimbiri, Makaure**

- Hawa ni wazee kwa umri.
- Ni wazee wa baraza la mtemi Masasa.
- Ni wasimamizi wa mila na desturi za kabila lao.
- Ni wapiganaji wa vita.

**Wahusika wengine:**

- Nhamo
- Maishingai
- Pindai
- Ambuya Tungai
- Ambupa Shungu
- Pedeisai
- Mtemi Zvedi
- Tupfumaneyi
- Chengatai
- Chido
- Ambuya Rekai
- Mtemi Chinjeyari

**Mandhari**

Riwaya hii ya *Takadini* imetumia ya vijijini katika nchi ya Zimbabwe katika karne ya 19. Katika masimulizi haya ya riwaya mandhari yake inaweza kugusa vijiji vya nchi nyingi za Kiafrika ambazo zipo katika dunia ya tatu. (Nchi zilizoendelea)

**Jina la Kitabu**

Jina la kitabu ni *Takadini*. Ni jina ambalo linatoka na jina la mhusika mkuu anayeitwa *Takadini*. Jina hili pia alipewa na mama yake aliyeitwa Sekai. Jina la Takadini lina maana ya "Sisi tumefanya nini"'?

Jina la kitabu linasanifu yaliyomo katika kitabu hiki kwani kwa kiasi Fulani jina hili linajumuisha mambo yaliyotokea wakati wa uzazi wa mtoto Takadini na matatizo yote waliyokumbana nayo yanayotokana na mila na desturi zinazowabagua watoto na wazazi wa watoto ambao ni Zeruzeru. Takadini yaani "Sisi tumefanya nini?" Linaakisi vilio vya walemavu wote ambao wanatengwa na kuuawa kwa Baraka za wazee wanaosimamia mila hizo. Hawakupenda kuzaliwa viwete, zeruzeru, vipofu na viziwi. Wazazi wao pia hawakupenda iwe hivyo. Kama ndivyo kwa nini kuna adhabu kama hizo? Kwani wamefanya nini? Muumbaji na Mungu na Mungu hana makosa katika uumbaji wake.

Kwa ujumla jinala kitabu linasadifu yaliyomo ndani ya kitabu kwa kuangalia maisha ya mhusika mkuu na matatizo anayopata yanamfanya mhanga yeyote wa mila mbaya aulize swali hili muhimu la **SISI TUMEFANYA NINI**? Na maana ya swali hili ndilo linatupatia jina la **TAKADINI.**

## KUFAULU NA KUTOFAULU

### Kufaulu Kimaudhui

Mwandishi amefaulu kwa kuweza kuonesha matatizo wanayopata watu wenye ulemavu. Mwandishi pia ameweza kuainisha tatizo kubwa linalichangia walemavu kutokubalika ndani ya jamii kuwa ni mila na desturi ambazo zinapandikiza dhana potofu kuhusu walemavu.

Mwandishi pia hakuishia kubainisha matatizo tu, pia ametoa masuluhisho ya matatizo hayo kuwa ni elimu, ujasiri, kuachana na mila na desturi zilizopitwa na wakati.

### Kufaulu Kifani

Mwandishi wa riwaya hii amefaulu sana kuonesha ufundi wake katika kusuka kazi yake. Ametumia lugha rahisi ya kueleweka lakini yenye tamathali za semi za kutosha na kuna matumizi ya mbinu nyingine za kisanaa. Vilevile ameweza kuhusu visa na matukio kwa muundo wa moja kwa moja ili kuwapatia wasomaji urahisi wa kufuatilia kwa umakini matukio yote.

Mwandishi pia ameonesha kupevuka sana katika kipengele kizima cha mtindo. Ameweza kutumia nafasi zote, matumizi ya tanzu nyingine kama vile nyimbo na hadidhi ndani ya riwaya.

Amefaulu pia kuteua jina la kitabu ambalo linabeba jina la mhusika na maudhui yaliyomo ndani ya kitabu.

### Kutofaulu

Kimaudhui mwandishi ameshindwa kuhusisha walemavu wengine katika kilio cha Takadini yaani tumefanya nini? Mwandishi ameonesha Zeruzeru tu. Angeweza kuonesha matatizo ya mila na desturi yanavyoathiri walemavu wengine.

Kifani mwandishi ametumia idadi ya wahusika bila sababu ya msingi. Idadi kubwa ya wahusika inatakiwa kuwa kielelezo cha upana wa maudhui yaliyomo ndani ya kitabu. Mwandishi pia ameshindwa kuonesha wanakijiji na watu wa kijiji cha asili cha Sekai walipokeaje hali ya takadini kwa kuoa mtu ambaye si mlemavu na kuweza kuzaa mtoto ambaye hakuwa na ulemavu ili liwe funzo kwa jamii zote.

## UHAKIKI WA TAMTHILIYA

**Jina la kitabu – *Ngoswe- Penzi kitovu cha Uzembe***

**Mwandishi - E. SEMZABA**

**Mchapishaji - Nyambari Nyangwine Publishers, 2006**

**Utangulizi**

Wasanii kama sehemu ya jamii wanapaswa kushirikiana kikamilifu katika mipango ya kitaifa. Mipango mingi inahusishwa na mipango mingine ya kisiasa, kiuchumi, na kiutamaduni. Ili mipango hii iweze kukamilika, suala la kujua idadi ya watu ni la msingi.

Ngoswe ni tamthiliya inayoangalia kwa makini suala la uhesabuji wa watu na utayari wa watu wenyewe kuhesabiwa. Aidha tamthiliya inaonyesha hali na wajibu wa watu wanaokabidhiwa dhamana ya kupanga kazi ya kuhesabu watu.

**Maudhui**

*Ngoswe* – Penzi Kitovu cha Uzembe ina dhamira mbalimbali zinazojitokeza:

**Suala la mapenzi**

Tamthiliya ya Ngoswe - Penzi Kitovu cha Uzembe inaliweka suala la mapenzi kuwa *"kitovu"* kikubwa cha uzembe. Katika kufafanua na kuthibitisha hoja au dhamira hii mwandishi anawatumia Ngoswe na Mazoea. Ngoswe kama kijana wa kiume na ofisa mhesabuji wa watu, anaonekana kuwa na uchu wa mapenzi mara anapomwona Mazoea (uk 5).

Kitendo cha *"kupenda"* si kibaya kwani ni sehemu ya maisha ya binadamu lakini jambo la msingi kuelewa hapa ni *"jinsi na namna ya kupenda"*Tatizo kubwa linalojitokeza katika tamthiliya hii kile kinachomfanya afisa Ngoswe kupenda kiasi cha kuharibu kazi. Ngoswe hawezi kulaumiwa kwa kumpenda Mazoea, ila analaumiwa kupenda bila kujizuia na kufika hatua ya kumtorosha Mazoea (uk 24-28). Katika mapenzi yanayoonyeshwa na Ngoswe. Athari zifuatazo zinajitokeza: Ngoswe anapotoroka baada ya kumuiba Mazoea anasahau karatasi za takwimu ya hesabu ya watu kwa vile kitendo cha kumtorosha Mazoea kinamuudhi baba yake, baba huyo anaamua kuchoma moto karatasi za takwimu (uk 28)

Mapenzi ya ngoswe yanaonyesha kuwa ni ya kitoto, na kwavile ni ya kitoto, inaonekana wazi hayakufuata taratibu za mila na desturi zinazofuatwa na wanajamii.

Kutokana na hali hiyo, kazi ya kuhesabu watu inaharibika. Labda jambo la kusisitiza ni kuwa mapenzi ni kipengele tu kilichosaidia kuleta au kuharibu kazi.

**Hasara za ulevi**

*Ngoswe - Penzi Kitovu cha Uzembe* inaonyesha tatizo la ulevi linavyochanganya akila na kuharibu kazi nay a kuwa pombe inaathiri mambo mengi.

Ulevi unachelewesha kazi, Mfano wa wazi ni wakati wanapopanga kuanza kazi ya kuhesabu watu, kila wakiwafuata baadhi ya watu hukuta wamekwenda kwenye pombe. Mito mingi anasema (uk 6).

**Mitomingi**: *Haya ni matatizo. Yote hii shauri ya pombe. Sina shaka yuko kilabuni.*

**Ngoswe:** *Haitasaidia. Mkewe tu hana habari ya kuhesabu watu, sembuse hao wengine! Kwa leo haiwezekaniki.*

Pili Ngoswe na balozi Mitimingi walikunywa pombe aina ya mnazi mpaka wakalewa na kusababisha kuchoma baadhi ya karatasi za takwimu (uk 18-19) ulevi ni jambo la hatari katika kazi na ni lazima upigwe vita.

**Umuhimu wa elimu**

Elimu ni chombo muhimu kwa jamii kama inatumiwa inavyostahili. Katika tamthiliya hii, suala la elimu linaonekana kutotiliwa maanani sana na wanakijiji ambako Ngoswe alikwenda kuwahesabu. Familia nyingi zanaeleza kuwa watoto hawasomi kwa sababu shule ziko mbali na pale wanapoishi wao (uk16).

Kutokana na shule kuwa mbali yaelekea maendeleo ya kijiji yamebaki kuwa duni. Mfano unaoonekana ni ule wa huduma muhimu kama vile Hospitali kuwa mbali na pale wanapoishi (uk 16)

Ili kupata maendeleo suala la elimu lazima litiliwe mkazo, watu wengi wakielimika wataweza kutumia huduma vyema- kama vile kwenda hospitalini kwa matibabu kuliko kushiriki mitishamba tu.

Lakini kwa upande mwingine elimu imeonyesha kwenye tamthiliya hii kuwa ikitumiwa vibaya haiwezi kuleta faida. Kwa mfano Ngoswe aliyekuwa amepata elimu ya kutosha ameshindwa kuitumia vyema katika kuleta ufanisi wa kazi na kuleta amani na utulivu miongoni mwa wanajamii.g

Ili elimu iweze kuwa ya manufaa ni lazima itumike katika kuibadilisha jamii na kuisukuma mbele katika maendeleo. Na ili kupata maendeleo, lazima shule au huduma nyingine muhimu kama hospitali zisogezwe karibu na watu. Kijiji cha Mitomingi kinahitaji msukumo mkali ili kufikia maendeleo bora.

**Malezi na ndoa za mitara**

Kijiji kinachojadiliwa katika tamthilia hii kinaelekea kuwa katika mila na desturi za kuoa wake zaidi ya mmoja. Balozi Mitomingi ameoa wake wawili na kuna wanaume wengine waliofanya hivyo.

Suala la kuoa mitara limeonyesha athari mbovu katika malezi na utulivu wa familia nzima. Mwanaume akioa wanawake wengi familia inaongezeka na kuwa kubwa kiasi cha yeye kushindwa wakati mwingine kutoa huduma zinazotakiwa.

Familia ya Mitomingi ina watoto ambao huduma zao zinatia mashaka ndio maana pengine Mazoea aliweza kumkubalia Ngoswe ili kukimbia matatizo yanayojitokeza katika familia yao.

Pia wanawake walioolewa katika mitara hawaelekei kuwa na upendo wa kweli katika jamii yao. Kwa mfano, mama Inda na mama Mazoea hawakuwa wanapendana kwa dhati kwa wake zake wote wawili kwa kina kilekile. Kwa sababu ya kutopendana miongoni mwao ugonvi hauepukiki.

Ikiwa tabia ya kuoa wake wengi ni mila, basi hii ni mila isiyofaa. Sawa na hili pia, mila mbovu ambazo hazifai, kama vile kuchaguliwa mchumba kama ambavyo Mazoea alifanyiwa, sijambogg zuri. Tamthiliya ya Ngoswe inatoa tahadhari na hatari ya kuwa na mitara.

**Hatari ya uvivu**

Kijiji cha balozi Mitomingi kwa ujumla kinaelekea kuwa na watu wengi wavivu. Suala hili lauvivu linaelekea kuathiri *kazi* zozote zinazowahusu watu hao. Kutokana na uvivu, jamii ya Mitomingi haina maendeleo. Hakuna shule wala hospitali. Maisha yao ni ya ulevi tu. Watu wanajihusisha zaidi na ulevi kuliko kufanya kazi. (Hapa mwandishi anaitahadharisha jamii kuwa, uvivu ni sumu ya maendeleo).

**Imani za uchawi na ushirikina**

Jamii ya Balozi Mitomingi inaelekea pia kuwa na imani ya uchawi na ushirikina.

Kwa mfano, wakati wa kuhesabu watu baadhi wanaamini kuwa wachawi ndiyo wanaohesabu watu ili wawaue. (uk, 14),

Mama : *"Sasa baba utatuhesabu vipi?"*

Mitomingi: *"Kwanini?"*

Mama : *"Kama utatuhesabu wewe basi u mchawi"*

Mitomingi: *"Mbona sikuelewi!"*

Mama : *"Mchawi ndiye anayehesabu watoto wa wenzie ili awaroge sasa wewe umchawi? Hata kama hu mchawi siwezi kukubali utuhesabu maana siwezi kujua kama nia yako ni mbaya au nzuri."*

Kutokana na jamii ya Mitomingi kuwa na imani hii, zoezi zima la kuhesabu watu linakwama. Hali kadhalika katika jamii hii waliarnini kuwa mtu akifa basi amerogwa. Kama asemavyo mama wa kwanza. (uk. 16) *"Wamemroga bure mume wangu. Alikufa akiwa na nguvu zake"*.

Kwa ujumla haya ni mawazo ambayo hayana umuhimu wowote kwa jamii zetu. Kufa kwa mtu si kurogwa tu, ni pamoja na kutompeleka hospitalini. Hivyo msanii anatahadharisha jamii kuwa imani hizi potofu lazima zipigwe vita.

**Nafasi ya mwanamke katika jamii**

Tamthiliya ya Ngoswe imemchora mwanamke katika vipengele mbalimbali. Kwanza, kama chombo cha starehe. Katika kijiji hiki wanaume wanaonekana kuwatumia wanawake katika starehe. Hii inathibitishwa na tabia ya kuoa mitara kila mara ili wanawake watumike kukidhi haja ya wanaume.

Pili, amechorwa kama mzazi, Hapa wanawake wanaonekana wakijishughulisha na kazi za malezi baada ya kuzaa.

Tatu, Amechorwa kama kiumbe. duni. Hapa mwanamke anadharauliwa na mwanaume na akili zake kufananishwa na za mtoto. Mwanamke hathaminiwi na

hafikiriwi kuwa anaweza kuchangia jambo lolote la maana. Wakati Mazoea

anatoroshwa na Ngoswe, Mitomingi anauliza (uk. 26),

Mitomingi: ' *'Hivyo na nyie hamkuona dalili zozote juu ya watu hawa wawili?"*

Mama Mazoea : *"Zilikuwepo "*

Mitomingi : *Kumbe mliziona mkanyamaza tu!"*

Mamainda : *"Sasa baba Mazoea tungefanya nini?"*

Mitomingi: : *"Mngefanya nini? Nyie wanawake akili zenu wote sawa." Si Mazoea, si mamayake...."*

Kauli hii inaonyesha kuwa Mitomingi humthamini mke wake kwa sababu anaona kwamba hana akili za kikubwa. ni kama mtoto wake Mazoea, Tabia hii ya Mitomingi na ya wanaume wengi kuwadharau wanawake ni jambo ambalo lazima lipigwe vita.

Mvutano baina ya mji na vijiji

Mwandishi ameonyesha tofauti za kiutamaduni kati ya maisha ya mjini na yale ya vijijini. Tamthiliya hii inaonyesha athari za maisha ya mjini juu ya yale ya kijijini. Kwa mfano, utulivu wa kawaida wa kijijini tumeona jinsi unavyoingiliwa na fujo za mjini za akina Ngoswe.

Kitendo cha Ngoswe kumtorosha Mazoea bila ridhaa ya wazazi wake ni kinyume na taratibu za vijijini lakini ni jambo la kawaida kwa upande wa mjini na ni kutokana na kitendo hicho, Mitomingi anachoma karatasi za hesabu ya watu. Katika kutatua mvutano huo kati ya miji na vijiji Ngoswe anapendekeza kuwa,

*"Hesabu ijayo ifikapo*

*Sharti vijiji kurekebishwa*

*Ujinga. Magonjwa na*

*Umaskini kupigwa vita*

*Na njia ni moja tu*

*Kuishi pamoja; kijamaa,"* (uk. 29).

Wakati Ngoswe anapendekeza watu kuishi pamoja kijamaa kwa upande wa Mitomingi anaona kuwa kuna umuhimu vilevile kwa watu wa mjini kufundishwa kuishi kijamaa ili waweze kuyajua vizuri maisha ya watu wa kijijini na bila hivyo basi mvutano utaendelea kuwepo. Mitomingi anasema hivi,

*"Mijini pia budi wafundishwe kuishi kijamaa maisha yetu kuyajua ama sivyo patatokea matata wawili hawa wakutanapo."* (uk. 30)

Kwa ujumla mwandishi anaona kuwa ili kuondoa mvutano huu kati ya miji na vijiji, ni lazima watu wa mjini wajifunze taratibu za maisha ya watu wa vijijini ambao bado hawajaathiriwa sana na utamaduni wa kigeni

**Ujumbe**

- Si jambo zuri kuchanganya suala la kazi na starehe au mapenzi; wakati wa kazi uwe wa kazi na wakati wa starehe uwe wa starehe, na starehe ziwe mbali naofisi.

- Wavulana wanaovuruga wasichana siku moja watakamatwa; na wasichana wenyewe wanapewa tahadhari kuwa wasifanye maamuzi bila kufikiri

- Elimu ni kitu cha muhimu sana katika jamii na jamii isipokuwa na watu walioelimika haiwezi kuendelea.

- Ili tuendelee tunahitaji kutupilia mbali ulevi na uvivu katika jamii zetu.

**Migogoro**

1. Mgogoro kati ya Ngoswe na wazazi wa Mazoea, unatokana na uamuzi waNgoswe kumpenda Mazoea na kujaribu kumtorosha.
2. Mgogoro kati ya Mazoea na wazazi wake unatokana na kitendo cha Mazoea kujaribu kutoroka na Ngoswe wakati anajua kuwa alikuwa anataka kuolewa.
3. Mgogoro kati ya Ngoswe na serikali unatokana na kitendo cha Ngoswe kuharibu kazi ya hesabu ya watu,

**Falsafa**

Mwandishi anaamini kuwa jamii inaweza kuingia katika matatizo pale mapochanganya vitu viwili kwa wakati mmoja. Hivyo si vizuri Migogoro

kuwatumikia mabwana wawili kwa wakati mmoja.

**Msimamo**

Mwandishi ana msimamo wa kimapinduzi, kwani amezungumza wazi juu ya matatizo mbalimbali yanayoikabili jamii kama vile umaskini, uvivu, ulevi. tatizo la ndoa za mitara na imani za uchawi na ushirikina.

**Fani**
Muundo

Muundo wa moja kwa moja umetumika. Tamthiliya imegawanywa katika maonyesho matano na kila onyesho lina kichwa cha kitaswira kinachoendana na yale yanayojadiliwa katika onyesho hilo.

**Mtindo**

Mwandishi ametumia mbinu ya dayolojia ambapo watu huzungumza wakijibizana na kutenda mambo mbalimbali, Katika kutajirisha mtindo wake, ametumia lugha ya kishairi pia (uk, 29 - 30).

**Lugha**

Tamthiliya ya *Ngpswe - Pen^i Kitow cha U^embe* imetumia lugha laini (rahisi) na nyepesi inayoeleweka kirahisi. Licha ya hiyo ametumia tamathaU za semi na mbinu zingine za kisanaa. Pia kuna ujenzi wa taswira.

**Misemo**

- Hebu keti tutupe mawe pangoni (uk. 11).
- Kupeleka chakula ndio unafanya makao kabisa (uk. 1 1) .

**Methali**

Penye nia pana njia (uk. 22).

TamathaU za Semi

***Tashibiha***

- Vumbi jekundu kama ugoro wa subiana (uk. 1).
- Hebu kwanza tazama sarawili yake miguuni kama kengele ya bomani, (uk. 7).
- Nilitoka hapa na kujitupa kitandani kama gogo. (uk. 18).

***Tasfida***

Wala hajarudi kama ingekuwa ni kujisaidia si angekuwa amekwishamaliza? (uk. 21).

**Mbinu nyingine za kisanaa**

**mdokezo**

- Mazoea: Sijui ... Siwezi... Narnuogopa baba (uk. 22),
- Mltomingi: Usizidl kuniambia mama; Tambitambi mambo yake hakuna asiyeyafahamu ... sasa mama .... (uk. 14).

Ngoswe: "Huyo mtoto wenu wa kwanza anaishi hapa au ...." *(uk., 16)*.

***Tunakaii Sauti***

Mfano. Ngoswe anacheka. ha! ha!, n.k.

*Takriri*

- Karibu. karibu (uk. 2).
- Hodi! hodi! (uk. 5).

***Taswira***

Taswira mbalimbali zimetumiwa na mwandishi katika tamthiliya hii. Msanii ametumia taswira ya mto kwa kuhusisha na matukio ya wahusika. Mwandishi analinganisha mwanzo wa mchezo na kijito. kijito ni mto mdogo sana. Hivyo

maelezo ya sehemu hii yanategemea kuwa madogo. Si makubwa. Matatizo yanayoelezwa katika sehemu hii ya awali tu.

Sehemu inayofuata inahusu vijito. Taswira ya vijito inaonyesha kuwa masuala yanayoshughulikiwa kujadiliwa hapa yanaongezeka ingawa bado si mazito.

Sehemu ya mto inaonyesha ukubwa wa shughuli ya Ngoswe. Ngoswe yuko kazini yuko mtoni tayari, yuko katika juhudi ya "kuvuka" kilichoko humo, bila shaka maji ya mto ni mengi (matatizo) na hivyo yeyote atakayeingia mtoni yampasa awe mwangalifu.

Sehemu ya jito inaashiria kuna hatari mno (matatizo). Kuna mengi katika jito. Kulivuka si kazi rahisi. Hatimaye tunaonyeshwa kuwa Ngoswe amezama baharini na amepotea. Tukihusisha na yale yaliyotokea na taswira ya bahari tunasema kuwa Ngoswe amezama, makaratasi ya takwimu yamechomwa moto na Mitomingi kutokana na kosa la kumtorosha Mazoea.

**Wahusika**

***Ngoswe***

Huyu ndiye mhusika mkuu katika tamthiliya hii. Ni msomi anayepewa kazi ya kuhesabu watu. Lakini kutokana na tamaa ya mwili wake anaharibu kazi baada ya takwimu zote kucttgmwa" moto na Mitomingi. Kutokana na kitendo chake cha kujaribu kumtorosha 'Mazoea bila ridhaa ya wazazi wake. Ngoswe ni mfano wa watu wanaochangartya kazi na starehe. Matokeo yake ni kuharibu kazi. Hivyo hafai
Kuigwa.

**Ngengemkeni Mitomingi**

Huyu ni balozi na baba yake Mazoea. Ni mzee ambaye ameshikilia ukale na anayependa ndoa za mitara. Huyu anachoma karatasi za takwimu kutokana na Ngoswe kujaribu kumtorosha mtoto wake Mazoea.

**Mazoea**

Msichana mwenye umri kati ya miaka 18-20 ambaye ni mtoto wa balozi Mitomingi. Mazoea anawakilisha wanawake wasio na misimamo maalum katika mapenzi.

**Mama Inda na Mama Mazoea**

Hawa ni wake wa Mitomingi na walezi wa Mazoea.

**Mandhari**

Mandhari ya kijijini imetumika. Kijiji hicho kipo katika nchi ya Tanzania. (Aidha inawezakana kikawa kijiji chochote katika nchi zinazoendelea).

**Jina la Kitabu**

Jina la kitabu *Ngoswe Penzi Kitovu cha uzembe* linasadifu vizuri yale yaliyomo ndani ya kitabu hiki. Ngoswe ni jina la mhusika mkuu ambaye msanii anaonyesha jinsi kuendekeza kwake penzi kulivyomharibia kazi yake ya kuhesabu watu.

**Kufaulu kwa Mwandishi**

Mwandishi ameonyesha kwa Masi kikubwa kuyajadili matatizo yanayozikumba jamii zetu katika fani mbalimbali za maisha. Matatizo hayo ni kama uchawi. uzembe, n.k. Pia ametumia lugha rahisi inayoeleweka.

**Jina la kitabu: - Kilio Chetu**

**Waandishi – Medical Aid Foundation**

**Wachapishaji: TPH**

**Mwaka: 1996**

**Utangulizi:**

Kilio Chetu ni tamthiliya iliyotungwa na Medical Aid Foundation. Katika tamihiliya hii kama asemavyo Vivian Mmari, Makamu Mwenyekiti wa *Medical* Aid Foundation katika utangulizi wake, Inajaribu kjvunja ukimya uliotawala miongoni mwa wanajamii katika kutatua matalizo makubwa ya kijamii yatokanayo na mahusiano ya kijinsia.

Tunasikia sauti ya jitimai itolewayo na watoto. Sauti iliyojaa sononeko na shutuma dhidi ya wazazi, walezi na watawaJa wenye kuufumbia macho msiba huu mkubwa wenye kuwaangamia.

Tunasikia sauti za vilio vya watoto wanaodai haki ya kuelimishwa kuhusiana na mambo yanayoweza kuathiri maisha yao. Wanataka wazazi, walezi na watawala wao kuwa wazi ill kunusuru maisha yao.

Hii ni tamthiliya inayopendekeza na kuibua mjadala miongoni mwa wanajamii kuhusiana na suala hili muhimu. Ni maoni ya mwandishi kwamba wakati tulionao sasa sio sawa na ule wa zamani. Mambo mengi yamebadilika, hivyo hata medani za vita hazina budi zibadilike katika kutatua matatizo ya wakati huu. Ushauri unaotolewa katika tamthiliya hii ni kwamba zile kuta zinazozuia mawasiliano ya wazi baina ya wazazi, walezi na watoto wao lazima ziangushwe.

Ni imani ya mwandishi wa tamthiliya hii kwamba, matatizo kama yale ya mimba katika umri mdogo, magonjwa ya zinaa kama UKIMWI, na kusambaratika kwa maadili katika jamii yanaweza kutatuliwa kwa kuwapa watoto elimu ya jinsia badala ya kuwajengea hofu na vitisho ambavyo kusema kweli vimedhihirika kuwa ni silaha duni katika mapambano haya.

**Maudhui**

TamthiJiya ya *Kilio Chetu* inabeba maudhui yanayozungukia mambo kadha wa kadha yahusuyo gonjwa hatari la **UKIMWI,** Kwa kutumia mbinu mbali mbali, mwandishi amelijadili kwa kina suala la malezi kwa \ijana/watoto. Anakemea vilivyo suala zima la mahusiano ya kijinsia wakati huu wa hatari tulionao. Pengine ni

vizuri tukazipitia dhamira zilizojitokeza katika tamthiliya hii moja baada ya nyingine.

**Dhamira**

Dhamira kadhaa zimejitokeza katika tamthiliya hii na zinajionyesha wazi kupitia migogoro anayoijenga mwandishi na pia matendo ya wahusika.

**Dhamira kuu**

***Elimu ya jinsia***

Umuhimu wa elimu katika familia, hususani elimu ya jinsia ni suala ambalo limetawala katika tamthiliya hii. Kwa upande mmoja kuna wazazi/walezi ambao wapo teyari na wameamua kuvunja ukimya uliokuwepo kati yao na watoto wao na kuzungumza nao waziwazi juu ya masuala ya mahusiano ya kijinsia na hadhari zake. Wahusika hao ni mjomba na baba Anna. Mathalani baba Anna anasema:-

*"Hili ndilo nimefaulu mwenzenu Nimemwambia mama Anna akae na mabinti nami nikae na wakiume …… Tumewaelimisha juu ya madhara ya tabia hiyo...*"(uk. 10).

Kwa upande mwingine kuna wazazi/walezi wanaoshikilia ukale. Hawa bado wanaamini kwamba kutozungumza na watoto habari zinazohusu ngono kutawazuia wasijihusishe na mambo ya kujamiiana mapema. Mama Suzi na baba Joti ni watetezi wa msimamo huu. Matokeo ya msimamo huu ni kupoteza watoto. Kwa mfano, mama Suzi anasema:- *"Tena ishia hapo hapo kaka! Huko si ndiko kunifundishia mwwanangu habari za ngono, ilitoka wapi hiyo*?.."(uk.9).

Matokeo ya msimamo hii miwili imejadilliwa barabara katika tamthiliya hii. Mjadala unaohitimishwa kwamba ni bora watoto wakaelimishwa na kupewa habari sahihi kuhusiana na ngono na afya zao za uzazi kuliko kuwatia hofu na kuwatisha kwani hiyo kamwe haisaidii.

Mwandishi kwa kumtumia kumtumia Anna, binti ambaye wazazi wake wameamua kuvunja ukimya na kuongea naye waziwazi juu ya mambo ya mapenzi na hatari yake anatanabaisha faida za elimu hii. Anna mara zote anachukua uamuzi wa busara huku akijiamini kwa kila analolisema. Hii ni kutokana na msingi imara aliopewa na wazazi wake baada ya kuamua kuwa wazi kwake. Kuonensha namna Anna anavyopikwa akaiva kufuatia elimu ya jinsia aliyopewa na wazazi wake, mwandishi anamchora akisema:-

*"Hujui, mjinga mkubwa we! Hujui kama kuna madhara mengine. Hujui magonjwa ya zinaa wewe, hujui kisonono, kaswende, na mengine kedekede, Haya hata juu ya UKIMWI hujui? Hebu nitolee uchafu wako mie ptuu!"*(uk.25).

Kauli hii ya Anna inaonyesha jinsi ambavyo watoto, wawe wa kike au wa kiume, wakielimisha na wazazi, kwa vile ndio walimu wao wa kwanza, wanaweza kujijengea uwezo wa kujiamini na hivyo kuepukana na vishawishi vinavyoweza kusababisha maambukizo ya UKIMWI. Wanapotishwa bila kuambiwa ukweli wa mambo kwa visingizio vya makatazo ya dini, mila na desturi wanakuwa mbumbumbu katika suala zima la kujamiianana madhara yake ni kama tuonavyo kwa wahusika Joti na Suzi katika tamthiliya hii.

**Dhamira ndogondogo**

Zipo dhamira nyingine kadhaa ambazo zimejadiliwa chini ya dhamira kuu, nazo ni:-

**Mapenzi katika umri mdogo**

Kimsingi watoto wadogo (vijana wadogo) bawapaswi kujihusisha na mambo *ya* ngono mpaka hapo umri wao unapowaruhusu kuoa au kuolewa. Huu ndiyo msingi na msimamo wa mila na desturi za kiafrika na hata dini. Kinyume chake watoto wanaanza kushiriki vitendo vya kujamiiana katika umri mdogo jambo ambalo ni hatari kwa maisha yao. Hiyo ndiyo hali halisi. Ni mara ngapi unasikia wanafunzi wa shule wanafukuzwa kwa sababu ya kubeba mimba? Hali hii imesawiriwa barabara katika tamthiliya hii ya *Kilio Chetu*. Watoto wa shule ya msingi kama vile Joti, Suzi na wengine wanaonekana kushiriki vitendo vya kujamiiana katika umri mdogo (uk. 16 -17, 19 - 21), Baya zaidi baadhi ya watoto wanashiriki matendo ya kujamiiana na wanawake au wanaume wanaowazidi umri., na pengine wenye wapenzi wengine jambo ambalo ni hatari kwa maisha yao. Kwa mfano, katika tamthiliya hii, mwandishi anatanabaisha kuwa Joti alikuwa anaparamia mpaka wasichana wakubwa wa mitaaani. Kwa maneno yake mwandishi anasema:-

*"Sasa ndiyo kuparamia mpaka wasichana wakubwa wa mtaani? Fikiri juu ya Chausiku, yule msichana mjuvi wa mji, ambaye pia anachukuliwa na yule Mpemba muu^a duka"* (uk. 23).

Suala hili linaweza kuwa limechochewa pamoja na mambo mengine, kuzagaa kwa sinema za utupu, vijalida vanavyohamasisha ngono na zaidi ya yote, kuna mtandao wa *internet* ambao watoto wadogo wanatumia kuangalia picha za utupu zinazowahamasisha kufanya ngono. Mwandishi ameisawiri hali hii barabara. Anawaonesha vijana wanne, Joti, Jumbe, Choggo na Mwarami wakikumbushana kwenda kuangalia picha za -X, ingawa kuna zuio kwamba picha hizo ni kwa wakubwa tu (uk. 17-18).

**Mapenzi na ndoa**

Pamoja na kuwepo janga la UKIMWI bado watu wameendelea kutokuwa waaminifu katika ndoa zao. Wanandoa wanathubutu kutembea nje ya ndoa bila woga. Mwandishi anasawiri hali hii kwa kumtumia mama Joti. Mama Joti analalamika kuwa ndoa yake imeingiliwa. Hivyo kama suluhisho anaamua kununua kanga zenye maandishi yanayomsuta huyo anayeingilia ndoa yake. Mfano maneno

*"Makapera kibao mume wangu wa nini"* (uk. 7).

Swali la kujiuliza hapa ni je hili litasaidia? UKIMWI je? Mwandishi pia anafichua fikra za walio wengi kwamba wanaougua UKIMWI ni makapera na sio wanandoa (uk. 7). Hata hivyo dhana hii sio sahihi maana UKIMWI hauchagui wenye ndoa au wasio na ndoa.

**Huduma kwa wenye Ukimwi**

Mwandishi anajadili suala hili. Anatueleza kwamba.kugusana kwa kawaida na mgonjwa kugusa nguo zake na kupeana mikono na mgonjwa hakuambukizi mtu ugonjwa huo. Aidha anajadili umuhimk wa kumtunza mgonjwa wa UKIMWI. Ingawa hataji waziwazi, lakini anaongelea suala hili kwa kumtumia mhusika Mjomba (uk. 34). Mjomba anawashauri baba na mama Joti kumpa matunzo mazuri na upendo mgonjwa Joti. Anashauri mgonjwa asitengwe maana ugonjwa huu hauambukizwi kwa njia ya kuvuta hewa ya mgonjwa au kula naye. Zaidi mwandishi anasema;

“*mgonjwa apewe chakula bora na yanapojitokeza magonjwa mengine kama malaria, apelekwe hospitali kwa tiba* ”(uk. 34)

na upendo mgonjwa Joti. Anashauri mgonjwa asitengwe maana ugonjwa huu hauambukizwi kwa njia ya kuvuta hewa ya mgonjwa au kula naye.Zaidi mwandishi anasema;

“*mgonjwa apewe chakula bora na yanapojitokeza magonjwamengine kama malaria,apelekwe hospitali kwa tiba.”(*uk.34).

**Tiba ya Ukimwi**

Kumekuwepo na mikanganyiko mingi miongoni mwa wagonjwa wa **UKIMWI** na jamaa wanaowauguza.Wengi wao hawataki kuamini kwamba wanaugua **UKIMWI** hata baada ya vipimo vya hospitali kuthibitisha hivyo.Badala yake hutawanya rasilimali zingewasaidia wao wakati wanaugua,na pengine familia zao baada ya kifo,katika kutafuta tiba za asili,Mwandishi akimtumia Mjomba analijadili jambo hili na kupinga waziwazi tabia ya kutapatapa anasisitiza tabia ya kuukubali ukweli ingawa unauma.

“*……………ugonjwa huu hauna tiba.Ushahidi hupo wazi kabisa kwa kadri tunavyowaona wanaopata ugonjwa huu. Kwa hiyo si busara pia kuongeza matatizo hali ukweli tunaujua…*”(uk.34).

Dhamira nyingine zilizojitokeza ni : athari zaakiw marafiki, Nafasi ya mwanamke katika jamii, Mila na desturi, n.k.

**Nafasi ya mwanamke katika jamii**

Waandishi wa tamthiliya hii ya kilio chetu wamemchora mwanamke katika nafasi na sura wa kadha wa kadha. Mathalani, wanamchora mwanamke akiwa mhuni na mwenye dhima ya kukidhi matamanio ya wanaume. Ni kwa kumtumia mhusika chausiku kwa mfano, waandishi wanatuonyesha namna mwanamke anvyotumiwa na

mwanaume katika dhima hii. Chausiku licha ya kuwa mpenzi wa mpemba mwenye duka pia ni mpenzi wa Joti, kijana mdogo aliye bado mwanafunzi wa shule ya msingi. Mhusika mwingine mwenye kudhihirisha surah hii ya mwanamke ni suzi. Huyu ameumbwa katika sura ya kukidhi tama za mwili wa Joti.

Kadhalika, mwanamke anaonekana kuwa mnyonge na duni kiasi kwambahana uwezo wa kuchukua hatua zinazostahili anapoona ndoa yake imeingiliwa. Hili ni tatizo kubwa linalomkabili mwanamke hasa kwa wakati kama huu ambapo dunia imekumbwa na balaa la UKIMWI. Tunamuona mhusika Mama Joti angundua tatizo katika ndoa yake lakini honyeshi ujasiri wa kukaa na Baba joti na kulizungumzia suala hili la unyumba wao, nabadala yake anakimbilia kununua khanga ili kumsuta huyo *"kidudu mtu"* anyeisakama ndoa yake. Nafasi aliyonayo mwanamke katika asasi ya ndoa ndiyo haimruhusu wala kumpa mwanamke ujasiri wa kukaa na kuzungumza na mmewe kuhusu masuala haya.

Kwa upande wa pili wa shilingi, mwanamke katika tamthiliya hii anapewa nafasi kuwa mtu mhimu na wa kutegemewa katika malezi ya familia. Mathalani wahusika wanawake Mama suzi na Mama Joti wanaonekana kutoa mchango mkubwa katika malezi. Wako makini katika kufuatilia mienendo ya vijana wao na kuhakikisha kwamba wanakua katika misingi inayofaa. Tatizo pekee tunalohisi limechangia kwa wao kutofanikiwa katika ama yao ni njia walizotumiakatika malezi. Pengine wangeweza kufaulu kama wangetumia njia ya kuzungumza na kuwaelimisha watoto wao kama walivyofanya Baba na Mama Anna.

Aidha, mwanamke katika tamthiliyaa hji, imejengwa akiwa ni mwenye kuwa na msimamo Thabiti kama amejengewa msingi imara katika malezi yake, mwakilishi wa mwanamke kama kiumbe alien a msimamo madhubuti katika tamthiliya hii ni Anna. Anakataaa kufanya mapenzi katika umri mdogolicha ya kudanganywa kasha kutishwa na mhusika Mwarami. Ingawa ni wachache, lakini wapo wanawake wa aina ya Anna katika jami

Lakini pia, kupitia mhusika Anna, mwanamke anajitokeza kama mshauri na muelimishaji rika. Katika kutimiza Dhima hii, Anna anamshauri mwarami kwamba asikimbilie sut kabla ya kuvaa nepi. Maana yake ni kwamba hana budi kusubiri hadi hapo wakati utakapofika ndipo aingilie masuala ya mapenzi, na sio kufanya hivyo katika umri mdogo alionao.

**Mila na desturi**

Suala l mila na desturi zinazofungamana na ukale pia limechukua nafasi katika tamthiliya hii. Moja ya sababu zinazowafanya baadhi ya wahusika katika tamthiliya hii ya kutokubaliana na ushauri wa kuongea na watoto wao mambo yanayohusu kujamiana nipamoja na mila na desturi, Mila hizi, haziruhusu wazazi kuongelea masuala hayo na watoto wao wa kuwazaa.

Hata hivyo kushikilia mila na desturi hizi katika enzi hizi za UKIMWI ni sawa na kusema waache watoto afe kwa UKIMWI. Ni kutokana na athari jamii inazoweza kuzipata, waandishi wakasema pamoja na kwamba mila na desturi zetu haziruhusuwatu wazima, has wazazi, kujadili masuala wanayoyaita ya wakubwa na

watoto wao wa kuwazaa, bado tunapaswa kuliangalia suala hili kwa jicho pevu. Pengine tuamue kuachana na mila na desturi hizo kwa lengo la kulinusuru taifa la kesho, Lazima jamii ikubali kuachana na maila ana desuri zilizopitw na wakati na kangalia njia ya kuwanusuruwatoto juu ya maambukizi ya UKIMWI.

**Migogoro**

Tamthiliya ya *kilio chetu*imejengwa juu ya migogoro kadhaa. Migogoro mingi ni kati ya kundi linaloshikilia ukale na lile linalotaka mabadiliko katika malezi ya watoto kuhusiana na elimu ya mahusiano ya kijinsia.

Mgogogoro wa kwanza ni kati ya mama suzi na bintiye. Mgogoro huu unatokana na vidonge vya kuzuia mimba kukutwa katika mfuko wa nguo za shule za suzi. (uk.7). mama suzi anchukua hatua ya kumwadhibu suzi kama mwarubaini wa kukomesha tabia hii bila kutmbua kwmba hofu na vitisho haviwezi kufua dafu mble ya silica ya mwili.

Mgogoro huu unaingiliwa na watu watatu. Baba Joti, ambaye anmuunga mkono mama suzi.Ili kusuruhisha mgogoro huu rai inatolewa kwamba lazima akina Mama Suzi wabadilike na wavunje ukimya uliotawala miongoni mwao kama kweli wamedhamilia kutatuamatatizo yanayoweza kuwaangamiza waoto wao.

Mgogoro mwingine ni kati ya Joti na mpenzie (Chausiku). Huu ni mgogoro unaotokana na tabia ya Joti kuwa na wasichana wengi anaotembea nao. Chausiku anamkaripia Joti kwa tabia hiyo chafu na anahahidi kumuunguza Joti na wasichana wake kwa moto hasa baada ya kugundua kwamba vitu anavyomhonga Joti anavitumia kwa wasichana wake wengine (uk. 22). Chausiku anasema:-

"*me nakununulia fulana ya mazoezi wewe unahonga kinyago chako kile…… Nikikupa hela ya kununua peni we unanunulia bazoka visichana vyako*"

Pia kuna mgogoro kati ya Mwaratni na rafikize ( Joti na Jumbe) juu ya suala la ngono, Mwarami na Anna juu ya suala la kufanya ngono katika umri mdogo, Suzi na Anna juu ya suala la utoaji mimba nk.

**Ujumbe na Maadili**

Baada ya kuisoma tamthiliya hii tunapata rundisho kuwa kweli "Asiyefunzwa na wazazi hufunzwa na Ulimwengu" ikiwa na maana kuwa mafunzo wayapatayo watoto toka kwa walezi wao ni bora na ndiyo yawasaidiayo kuishi kwa kujiamini na kutohadaika na mambo yasiyofaa. Hivyo si vizuri kuwanyima fursa hiyo kwa kisingizio cha dini, mila, desturi au sababu nyingine yoyote.

Mwandishi anatoa ujumbe kwamba ugonjwa wa UKIMWI hauenezwi kwa njia za kugusana au kula na mgonjwa. (uk. 34) bali ni kwa njia ya kujamiiana na mtu mwenye ugonjwa huo. Ujumbe huu unasawiri mazingira yetu kwa sasa ambapo kuna ongezeko kubwa la maambukizo ya ugonjwa wa UKIMWI. Hivyo anatoa wito kwa wazazi na walezi kutofumbia macho hali hii bali wawe wazi kwa watoto wao kwa

kuwapa elimu ya kijinsia na jinsi ya kuepuka ugojwa huu. Kwani hauna kinga wala tiba.

**Mtazamo na msimamo wa mwandishi**

Msanii anautazama ulimwengu kwa jicho pevu na yakinifu. Anauona kama kitu kinachobadilika, hivyo hata jamii inapaswa kubadilika. Anayachunguza mazingira yanayo mzunguka mtoto katika zama hizi na kugundua kwamba watoto wako hatarini kuteketea kutokana na kukosa habari zozote za kuwasaidia. Mwandishi anatoa msimamo ambao ni tofauti na wazazi/walezi wengi. Msimamo wa kuvunja ukimya na kuzungumza na watoto kwa kuwapa elimu ya jinsia ili kuwanusuru wasiangamie.

**Falsafa ya Mwandishi**

Mwandishi anaamini kwamba kuwapa watoto elimu ya familia ikiwa ni pamoja na elimu ya jinsia si kuwafundisha umalaya kama wanavyoeleza wapinzani wa hoja hii. Badala yake, ni kuwafanya watoto wajitambue na kuyaelewa barabara madhara ya kujiingiza katika matendo ya kujaamiiana katika umri mdogo, Hii ndiyo njia pekee ya kuwanusuru vijana/watoto dhidi ya "dubwana" linalotishia maisha yao. Hii ndiyo falsafa ya mwandishi wa tamthiliya hii.

**FANI**

Tamthiliya ya *Kilio Chetu*imedhihirika kuwa ni mojawapo ya tamthiliya zenye utajiri wa vipengele vya kifani. Mwandishi amtumia vipengele kadha wa kadha vya fani.

Katika kufikisha maudhui yake kwa walengwa. Vipengele vya fani ambavyo vimejitokeza mara kwa mara katika kazi hii ni hivi vifuatavyo:

**Wahusika**

Wahusika wa fasihi ni watu ama viumbe wanaowakilisha tabia halisi za watu katika jamii. Tamthiliya ya *Kilio Chetu* ina jumla *ya* wahusika kumi na wawili, na wengi wao karibu wana hadhi sawa kiasi kwamba sii rahisi kuwatenga katika makundi ya wahusika wakuu na wadogo kama tulivyozoea.

**Wasifu wa Wahusika**

**Mama Suzi:**

Huyu ni mama yake Suzi. Ni mwenye kushikilia msimamo wa kizamani, kwamba mzazi hawczi kuongea na mwanae masuala ya kujamiiana (uk. 6). Haamini kwamba watoto wadogo, kwa mfano, wanaosoma darasa la tano wanaweza kuwa wameanza tabia ya kujamiiana (uk. 5). Kwa maneno yake anasema:

*"Fausta alikuwa mtoto sana. Mtoto wa darasa la tano. Mambo hayo asingeyajua"* (uk. 8.)

Mama Suzi anawiakilisha kundi la wazazi ambao hawaamini katika kusema na watoto wao mambo yanayoweza kuhatarisha maisha yao, kwa mfano, anapomkuta mwanae Suzi ana vidonge vya kuzuia mimba anachukua jukumu la kumpiga badala

ya kumwelimisha juu ya madhara yake (uk. 7 - 9). Haamini kwamba binti mdogo kama Suzi anaweza kuyafahamu mambo ya kujamiiana mpaka anapomkamata na vidonge vya kuzuia mimba. Ndipo anasema:

*"Mwanetu huyu keshakua sasa anabugia vidonge vya kuzuia mimba ... wewe unataka kuniumbua mie, we mbwa mweusi... "* (uk. 8).

**Suzi**

Huyu ni mtoto wa mama Suzi. Ni binti mdogo anayesorna darasa la sita. Ni mpenzi wa Joti, mwanafunzi mwenzake. Amekwisha jiingiza katika masuala ya mapenzi katika umri huu mdogo kinyume na matarajio ya mama yake. Mwanzoni mama yake hakuwa na habari kuhusiana na tabia hii ya Suzi hadi alipomkamata na vidonge vya kuzuia mimba (uk. 8). Anamwogopa mama yake sana lakini hawezi kushinda nafsi yake iliyokwishatekwa na mambo ya ngono kutokana na ukosefu wa elimu juu ya mambo haya. Anapata mimba na inaelekea ana UKIMWI kwani Joti aliyempa mimba hiyo imedhihirika kuwa ana UKIMWI.

***Baba Joti***

Huyu ni baba yake Joti kijana ambaye amepata ugonjwa wa UKIMWI kutokana na kijiingiza katika mambo ya mapenzi akiwa mwenye umri mdogo. Ni jirani yake na akina Mama Suzi. Kama alivyo Mama Suzi, Baba Joti pia haamini katika kuwaelimisha watoto kuhusiana na masuala ya kujamiiana. Anamwona Suzi kuwa ni "kitoto kidogo" kama alivyo mwanae Joti hivyo kumpa elimu ili aifahamu jinsia yake na ajijue alivyo ni kumharibu.

Sado ameshikilia msimamo wa kizamani kwamba wazazi hawawezi kukalishana kitako na watoto wao na kuwaeleza habari za ngono (uk.10). Kwa mawazo yake,dawa peke ya kuwadhibiti watoto wasijiingize katika masuala hayo ni viboko au mijeledi tu (uk. 10).

**Mama Joti**

Huyu ni mke wa Baba Joti na mama yake Joti. Anaamini kuwa watoto wanajua makubwa maana "Wembamba wa reli treni inapita" (uk. 6). Hakubaliani na kitendo cha kumkingia kifua mtoto maana si rahisi kujua huko waendako wanafanya nini (uk. 6). Ndoa yake imo matatani kufuatia kuingiliwa na nyumba ndogo yeye anaita *"Kidudu mtu"* (uk. 7).

**Mjomba**

Ni kaka yake Mama Suzi. Ana upeo rnpana wa kuelewa mambo. Anafahamu ulimwengu wa sasa ulivyo. Maoni yake ni kwamba watoto wapewe elimu ya familia, ikiwa ni pamoja na elimu ya jinsia ili waweze kujua kinagaubaga juu ya mambo yahusuyo mapenzi na hatma yake. Anamini kwamba hii itasaidia kuwaonesha watoto madhara ya kufanya mapenzi kabla ya ndoa. Ana ushauri mzuri, anamshauri Baba Joti asihangaike kwenda kwa waganga wa jadi kwa ajili ya tiba ya Joti aliyegundulika kuwa ana UKIMWI. Badala yake anashauri Joti apewe matunzo mazuri ili aweze kuishi kwa matumaini (uk. 34).

**Baba Anna**

Kama mjomba, Baba Anna pia ana upeo mpana wa kuelewa mambo. Yeye na mkewe, mama Anna, wameweza kukaa na watoto wao na kuwaelimisha juu ya madhara ya tabia ya kufanya mapenzi katika umri mdogo. Kwanza kwa watoto wenyewe na pia kwa familia nzima na hasa kwa wazazi wao (uk. 10). Anaamini kwamba iwapo watoto wataelimishwa barabara kamwe hawatathubutu kujihusisha na masuala ya kujamiiana.

**Jirani**

Ni jirani yake Baba Joti. Hana imani na matokeo ya vipimo vya hospitali hivyo anashauri wampeleke Joti kwa *"mafundi"* zaidi wa tiba. Huyu anawakilisha wananchi wengi ambao hawataki kuamini kwamba UKIMWI upo katika jamii, na mtu ukimpata sio kwamba amerogwa.

**Chauslku**

Ni msichana wa mtaani, jirani na akina Suzi. Si msichana mzuri kitabia. Anafanya mapenzi na watoto anaowazidi mbali kwa umri. Ni mjuvi wa mji na anachukuliwa pia na Mpemba mwenye duka.

**Chogo, Mwarami na Jumbe**

Wavulana wanaosoma pamoja na Joti. Kama Joti, nao wamekwishajiingiza katika mapenzi na wasichana. Wana tabla ya kuangalia magazeti ya picha za uchi na sinema za "X". Wana tabia ya kukaa vijiweni na mazungurnzo yao ni kuhusu masual,.a ya ngono.

**Joti**

Mwanafunzi wa shule ya msingi darasa moja na akina Suzi, Chogo Jumbe na Mwarami. Ana mahusiano ya kimapenzi na wasichana kibao, kwa mfano Suzi, Chausiku, Yoranda, Gelda na Sikujua. Kwa sababu wazazi wake hawakuongea naye ili kumpa elimu juu ya athari za ngono aliendelea na tabia hii hadi akaukwaa UKIMWI

**Muundo:**

Tamthiliya ya kilio chetu imechuka muundo wa moja kwa moja, yaani sago. Visa vinaelezwa kwa mtiririko bila kukatizwa. Mchezo unaanzia katika sehemu ya kwanza ambapo maelezo kuhusu kuingia na dubwana (UKIMWI) katika kisiwa kunaelezwa. Sehemu ya pili intujulisha juu ya kifo cha Fausta na pia habari za Suzi kufanya mapenzi zinajulikana kufuatia kukutwa na vidonge vys kuzuia mimba katika mfuko wake. Ni katika sehemu hii mjomba na baba Anna wanaelezea umhimu wa elimu ya jinsia ili kuwanusuru watoto na janga hili la UKIMWI.

Ni katika sehemu ya tatu na ya nne inpodhihirika kwamba wanaoitwa watoto si watoto tene maana wameshajiingiza katika mambo ya ngono, na hivyo wako hatarini kuangamia. Mahusianao ya kati ya joti na Suzi, na wasichana wengine kama vile Chausiku, Yoranda, Gelda na Sikujua yamefunuliwa katika sehemu hizi. Aidha, kwa kututmia mhusika Anna, inaoneshwa katika sehemu ya nne, namna motto aliyepwa elimu ya jinsia anavyoweza kukabiliana na vishawishsi na hivyo kuepukana na balaa la UKIMWI

Sehemu ya tano, suzi anagundulika kuwa na mimba ya Joti . sehemu ys saba intupeleka nyumbani kwao Joti ambapo inadhihirika kwamba joti anaugua UKIMWI na ushsuri unatolewa na mjomba kwamba apewe matunzo mazuri ili aweze kuishi kwa matumaini.

**Mtindo:**

Mwandishi wa tamthiliya hii amedhamilia kuifanya tamthiliya yake iwe na umbo la kiafrika kufuatia kutumia baadhi ya vipengle vya sanaa za maonyesho za kiafrika katika tamthiliya hii ya *kilio chetu.* Baadhi ya vipengele hivyo ni pamoja na matumizi ya nyimbo, (uk.1)……, niendelee, nisiendelee?......au mmechoka? (uk.113). pia katika uk. 36, mwandishi anamalizia …Na hadithi yangu imeishia hapo.

Mwandishi pia amemtumia mtambaji kutoa maelezo na ufafanuzi kuhusu matndo ya wahusika na matukio katika tamhiliya yake , mtindo uliozoeleka.

Aidha, mwandishi ametumia mtindo wa diologia. Amefaulu kuleta diologia inayovutia na kuaminika baina ya wahusika.ni diologia ambayo, kwa kweli, ametumia maneno machache lakini yaliyoteuliwa kwa ufundi na ustadi mkubwa sana.

**Matumizi ya lugha:**

Mwandishi wa tamthiliya hii ya kilio chetu ameonesha ustadi mkubwa katika uteuzi wa lugha ya kutumia. Ametumia lugha inyowafanya wasomi watafakari kwa.

Makini kile wanachokisoma, Lugha iliyotumika ni nyepesi kwa hadhira lengwa, yaani watuwa kawaida, hasa wazazi la walezi. Aidha ni lugha iliyoshehenezwa tamathali za semi na mbinu nyingine za kisanaa

***Methali,***

“Asiyefundwa na mamaye hufundwa na walimwengu” (uk.36)

“Wembamba wa reli treni inapita “(uk. 6)

***Misemo;***

“….kukimbilia suti na nepi hujavaa” (uk.26)

“Mapenzi ni tiba” (uk. 22)

: Nakuwa nyumanyuma Kama koti” (uk.4)

Útakatifu wa usoni” (uk.4)

***Nahau***

”kufa kwa kunyaga nyaya” (uk.4)

***Matumizia ya lugha ya kingereza na asili***

Mwandishi ingawa ni Kwa kiasi kdogo, ametumia lugha ya kuchang'nya lugha ya Kiswahili na kingereza. Lengo hasa la kuchanga'nya lugha lilikuwa ni kusawiri namna nijana weing wa siku hizi wananyoongea Kwa kuchanga'nya Kiswahili na kingereza. Mfano mzuri 9uk.16)

"Ndo ume-come sio?"

Kwa upande wake, lugha ya asili haijatumika katika mazungumzo ya kawaida. Imetumika tu katika wimbo wa maombolezo (uk.35)

***Tamathali za semi.***

"Mbona unakuwa mgumu Kama mpingo"? (uk.5)

"Miti inayoungua Kama mabua" (uk.6)

"…..Wakapukutika Kama majani" (UK 3)

***Sitiari***

"Ndio wa kumvumilia buyu nguru anayechimba ndoa yangu" (uk.7)

"Huyu kinyago wako anakimbia nini?" (uk. 21)

Mbinu nyingine za kisanaa

***Onamatopea***

"Wacha moyo unipwite pwi, pwi, pwi," (uk .16)

"Basi vupu nikadondoka…." (uk. 16).

***Takriri;***

"Piga domo, piga domo" (uk.16).

"Watu walipukutika, wakapukutika Kama majani ya kiangazi; wakapukutika" (uk.1).

**UJENZI WA TASWIRA**

Mwandishi anatujengea taswira ya Dubwana lililoleta balaa kisiwani (uk. 1).

Anaeleza kwamba kila mtu aliyeguswa na dubwana hili alipata madhara. Watu waliotoka mapele, wakaharisha, wakanyonyoka nywele, wakakonda na kupoteza uzito kabla ya kufa. Haya ni maelezo yanayomfanya msomaji ajenge woga juu ya dubwana hili yaani UKIMWI.

**Mandhari**

Mandhari katika tamthilia ni ile sehemu au mazingira ambamo makutano yanatokea. Mandhari ya tamthilia hii ni ya mjini. Hii inathibitishwa na mhusika jirani anaposema:

*“Mie toka siku ile niwaone hospitali sijakaa mjini. Nilikwenda zangu shamba kupambana na nyani wala nafaka” (uk.32)*

Lakini pia habari za kuangalia sinema za “X” (uk.18) zinatuthibitishia mandhari ya mahali matendo haya yanapotendeka ni ya mjini. Zaidi ya hapo, lugha inayozungumzwa na wahusika vijana kama vile Joti, Jumbe, Chogo na Mwarami ni lugha ambayo imezoeleka mazingira ya mjini kulIko vijijini (Rejea kwa mfano mazungumzo yao (uk.16).

Tunaelezwa pia kwenye tamthilia hii kwamba mhusika Mwarami alikuwa akimnunulia Anna soda na mihogo kule uwanja wa Sabasaba (uk.26). Zaidi Anna anaeleza katika wimbo wake kuwa hataki pesa za wanaomhonga wala lift zao (uk.27). Ni wazi kwamba uwanja wa Sabasaba upo mjini na lift kwa akina dada, hasa wanafunzi zinatolewa mjini kuliko vijijini.

**Jina la kitabu**

*Kilio chetu*ni jina la kitabu linalo akisi yale yaliyo katika kurasa za ndanio zatamthiliya hii.*Kilio chetu*ni kilio cha jamii nzima kuhusu gonjwa la UKIMWI. UKIMWI umepoteza maisha ya watoto, vijana, wazazi na ndugu zetu ambao ni muhimu sana kwa ustawi wa familia na jamii kwa ujumla.

*Kilio chetu* kama jamii ni muhimu ili kuonesha huzuni yetu dhidi ya gonjwa hili la UKIMWI ili jamii isiendelee kuwa na kilio.

Kwa ujumal, *kilio chetu* ni jina la kitabu ambalo lina sadifu yaliyo ndani kwa namna mbili.

1. *“Kilio chetu”* ni kielelezo cha huzuni walizonazo wahusika ndani ya kitabu kutokana na ugonjwa wa UKIMWI kuathiri watu wengi.
2. 
3. *“Kilio chetu”* pia inawakilisha mahitaji au matakwa ya kuwepo kwa elimu ya UKIMWI na Jinsia ili kupambana na UKUIMWI.

Hivyo, *Kilio chetu* imesadifu yaliyomo ndani ya kitabu kwa kuonesha vilio vinavyotokana na UKIMWI na pia vilio vya kuhitaji msaada madhara ya UKIMWI.

**KUFAULU N A KUTOFAULU KWA MWANDISHI**

1. **Kufaulu**

Kimudhui, mwandishi amefaulu kueleza jamii UKIMWI ni kitu gani, njia zinazoambukiza na kujikinga na namna ya kuhudumia wagonjwa wa UKIMWI. Mwandishiamesisitiza umuhimu wa Elimu, uwazi na ukweli kama mbinu muhimu ili kuvunja ukimva.

Kifani, mwandishi ameweza kuumba wahusika wa rika tofauti amabao ni muhimu katika kupambana na UKIMWI

B. **Kutofaulu**

Mwandishi ameonesha vijana ndio waathirika pekee wa UKIMWI. Mwandishi angeweza kwenda mbali zaidi kuwa watu wazima, na hata baadhi ya watu wanonesha kama watakatifu wanaweza kuwa chanzo cha UKIMWI. Mwandishi angeweza kugusa hata ndoa. Namna watu wanavyopaswa kulinda na kuheshimu ndoa zao ili kuepuka UKIMWI. Mama wajawazito wangehimizwa zaidi kupima virusi ili kuwa namna ya kumsaidia kiumbe aliye tumboni. Si wote wenye UKIMWI hupata kwa njia ya ngono, kuna wengine hupata virusi vya UKIMWI kwa njia nyingine.

## NADHARIA NA UHAKIKI WA USHAIRI

**Jina la kitabu - MALENGA WAPYA**

**Waandishi – TAKILUKI**

**Wachapishaji – OUP**

**Utangulizi**

*Malenga wapya* ni kitabu kinachozungumzia masuala mbalimbali ya kijamii kama vile ukombozi wa mwanamke, umuhimu wa Kilimo,
umuhimu wa kutatua matatizo katika jamii, umuhimu wa kutenda mema, matumizi mazuri ya pesa pamoja na athari za ukoloni mamboleo.

**Maudhui**

**Dhamiri kuu: Ukombozi**

Katika diwani hii msanii amejadili dhamira ya ukombozi wa kiuchumi, kisiasa, kitamaduni na kifikra.

**Ukombozi wa Kiuchumi**

Katika kujadili ukombozi wa kichumi msanii amesisitiza mambo muhimu yafuatayo:

Kwanza, Umuhimu, wa kuinua uchumi wetu. Katika suala la kuinua uchumi wa nchi yetu wasanii wanasema kuwa kuna umuhimu wa kujenga uchumi imara ili kujenga taifa lenye uwezo wa kujitengemea kiuchumi.

Katika shairi la *"Tuzingatie Haya,"* (uk .27 – 28) wasanii wanasisitiza umuhimu wa kufufua uchumi wa nchi. Pia ili tufufue uchumi wa nchi ni lazima tupunguze maneno na sote tufanye kazi kwa bidii, wananchi wote tuungane na kuhamasishwa (ubeti 2.) raia na viongozi sote tufanye kazi kwa bidii (ubeti

3) tuondoe tofauti zetu za tuepukane na tamaa ya utajiri. Beti za (2 na 4) zinasema:

2. *Uchumi kufufua, si hotuba refu sana.*

*Moja litosaidia, ni kuhamasishana,*

*Jingine linalofuatia, sote kushirikiana,*

*Tuyazingatie haya, wala tusirudi nyuma.*

4. *Kufanya kazi lazima, tuacheni utegezi,*

*Na jingine la kukoma, kuwepo kwa uchaguzi,*

*Kutupiana lawama ni mambo ya kipuuzi,*

*Tuyazingatie haya, wala tusirudi nyuma.*

Hapa inaonekana kuwa ili tuweze kuinua uchumi wa nchi ni lazima tuwahamasishe watu; tujenge umoja na ushirikiano, tuondoe ubaguzi na tufanye kazi kwa bidii.

Shairi hili, pamoja na mambo mengine linawataka viongozi waache kupora mali ya umma na badala yake washiriki barabara katika kujenga uchumi. Iwapo tutajenga uchumi imara tutaondokana na mtatizo yanayoonekana.Haya tunayapata katika shairi la Tunzo (uk.29 – 30).

Jambo la pili ambalo wasanii wanalisisitiza katika ukombozi wa kiuchumi ni umuhimu wa Kilimo.Wasanii wanasema kuwa iwapo tutazingatia Kilimo tutapata chakula cha kutosha na ziada ya kuuza nje ya nchi kwa ajili ya kujipatia pesa za kigeni na kwa ajili ya kuboresha maisha yetu. Iwapo utazingatia Kilimo tutaepukana na tabia au hali ya kutegemea chakula kutoka nje. Suala la kupata chakula cha kutosha litatuepusha na masharti magumu yanayoweza kupewa na watu wanaoweza kutupatia chakula pindi tunapopata tatizo la uhaba wa chakula.

Washairi wanadhihirisha haya kwa kutumia shairi la Adui (uk. 13)

4. *Tulime jama tulime, tushinde adui njaa,*

*Hapa kwetu ituhame, kwingine kutokomea,*

*Wala sisi tusikome,, chakula kujilimia,*

*Tutie jembe mpini, tuteremke shambani*

5. *Chakula kujilimia, ziada kujipatatia,*

*Tuache kutegemea, vya nje kuagiza,*

*Siku watojigomea, nani tutamkimbilia*

*Tutie jembe mpini, tuteremke shambani*

Katika shairi la "Mkulima" (uk. 3 – 4) linaonyesha mkulima kama mtu duni likimlinganisha na watu wengine. Huyu ni mtu ambaye analima ili kulisha watu wote nchini na kuinua pato la taifa, lakini hathaminiwi na watu wanaohusika.

5. *Wakazi wa mjini, na wafanyakazi pia,*

Na viongozi nchini, huduma awapatia.

*Sijui kukosa nini, thamani kutomtia,*

*Mkulima naye mtu, yafaa kuthaminiwa*

Hivyo basi, ili tuimarishe Kilimo ni lazima kumthamini mkulima. Na kumpa huduma muhimu anazostahili. Pia chakula kipunguapo nchini wa kutupiwa lawama ni mkulima ambaye hathaminiwi. Wanasema:

7. *Upungufu wa chakula, utokeapo nchini,*

*Hukumbana na suala, shambani wafanya nini,*

*Kazi yako unalala, watia njaa nchini,*

*Mkulima naye mtu, yafaa kuthaminiwa.*

Licha ya Mkulima kufanya juhudi kubwa katika kuinua uchumi wa nchi hapewi huduma muhimu, badala yake huduma hizo hupelekwa mjini; Kama wanasemavyo waandishi;

8. *Starehe kwa jumla, zinaishia mjini,*

Maji safi ya muala, njia na umeme ndani,

*Aliyezichuma hela, ni Mkulima shambani,*

*Mkulima naye mtu, yafaa kuthaminiwa.*

Hapa inaonyesha kuwa licha ya kwamba mkulima ndiye anayezalisha kila kitu.Wanaofaidi matunda ya Mkulima ni watu wa mjini. Ili tuweze kuinua na kuimarisha Kilimo chetu, ni lazima tumthamini mkulima na apewe misaada na huduma mbalimbali.

Kwa upande mwingine wasanii wanaonesha kuwa ili tuweze kujikomboa kiuchumi ni lazima tuachane na uzembe kazini. Washairi wanadai kuwa kuna baadhi ya watu hasa, wafanyakazi maofisini ni wazembe ,hawatimizi wajibu wao kama ipasavyo.pindi tu waingiapo ofisini wanajifanya wana kazi nyingi kiasi kwamba kiasi kwamba wanashindwa kuwahudumia wananchi kama wasemavyo washairi katika shairi la *Puuzo (uk. 8)*.

1. *Ofisini ukifika, wanajitia pirika,*

   *Haja unayoitaka, mwenyewe tuhangaika,*

   *Wajifanya hawajali*

4. *Baoni utapokaa, mwishowe tapakataa*

   *Shida iliyokukaa, nayo yazidi chakaa,*

   *Sababu puuzo zao*

Wasanii hawa wanakemea tabia hiyo na kuwataka wanajamii wachape kazi kwa bidii ili kuinua uchumi wa nchi. Uchapaji kazi huo lazima uanzie katika ngazi ya chini kama vile familia, hadi kitaifa. Wafanyakazi, wakulima na wasomi wote sharti wachape kazi kulingana na majukumu yao ili kuteketeza adui uzembe. Haya tunayapata katika shairi la Charuka (uk. 53 – 55).

Vilevile wasanii wanonesha kuwa ili tujikomboe kiuchumi tupige vita ukoloni mamboleo na unyonyaji. Ukoloni mamboleo ni hali ya nchi moja kuitawala nchi nyingine kiuchumi. Hii inaathiri uchumi wa nchi maskini. Katika shairi la “22” *Nipatieni Dawa,”* jinsi ukoloni ulivyoondoka nchini inazungumzwa lakini ukoloni huo umerudi kwa umbo lingine la ukoloni mamboleo. Kuja kwa ukoloni mamboleo, kuliendeleza taratibu na desturi za kunyonya uchumi wa nchi masikini.

6. *Pale pale penye donda, ndipo apojanibana.*

*Nikawa sasa nakonda, pumzi nikawa sina,*

*Nikabaki kama ng'onda, la kufanya sikuona,*

*Nipatieni dawa, nipate kutononoka.*

7. *Kila nikifurukuta, donda apate toa,*

*Najuta kwenye tata, shina kujizidishia*

*Dawa nimeshatafuta, ili nipate kutoa,*

*Nipatieni dawa, nipate kutononoka.*

Beti hizi zinaweka wazi jinsi ukoloni mamboleo unavyozibana nchi maskini kiuchumi mpaka zinashindwa hata kupumua. Ili tujikomboe kiuchumi, ni lazima tufate dawa ya kuondoka ukoloni mamboleo hapa nchini. Kwa hiyo ili tujikomboe kiuchumi lazima tupege vita ukoloni mamboleo.

**Ukombozi wa kiutamaduni**

Katika ukombozi wa kiutamaduni wasanii wanazungumzia juu ya ukombozi wa mwanamke. Ukombozi wa mwanamke ni jambo la msingi na muhimu katika jamii. Mwanamke akikombolewa ni sawa na jamii nzima kukombolewa. Shairi la 10, "Kifungo", waandishi wanasema;

7. *Kwa kuwa ni mwanamke, ndani mnanifutika*

*Lazima nje nitoke, kupata ninayotaka,*

*Nimechoshwa na upweke, sitaka kudhalilika,*

*Kifungo kimenichosha, minyororo nafungwa.*

Ili aweze kujitegemea mwenyewe, mwanamke anahitaji kuwa huru, na siyo kufugwa fugwa ndani na kumtegemea mwanamme.

"Hina inapapatuka" Linaonyesha jinsi mwanamke alivyogandamizwa na mwanaume hapo zamani:

2. *Zamani tukikumbuka,watiaji walivia,*

*Nyumbani  katu kutoka, ndani walijichimbia,*

*Mabwana walitamka, marufuku kutembea,*

*Unyonge inaondoa, Hina inapatikana.*

Hapa wanaonyesha kuwa mwanamke hakuruhusiwa kwenda kutembea. Mwanamke aliwekwa utawani na kazi yake kubwa ilikuwa kupika chakula.

Hakuruhusiwa kabisa kusoma na kuandika.

Hata hivyo mabadiliko ya jamii kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni yanamkomboa mwanamke kidogo kidogo. Kwa wakati huu nao wanafanya kazi mbalimbali ambazo hapo zamani hawakuruhusiwa kuzifanya kwa mfano:

7. *Leo wanamakanika, hadhi yao kutetea,*

*Kila mahali kufika, na wao wameenea,*

*Kazini wajumuika, shime wanajifanyia.*

*Unyonge inaondoa, hina inapapatuka.*

8. *Kila utapopashika, nao wameshafika,*

*Zege inapopondeka, ni wao hujipondea,*

*Matofali kupeleka, mafundi kusaidia,*

*Unyonge inaondoa, hina inapapatuka.*

Kujikomboa kwa mwanamke kunatokana na juhudi zake chini ya Umoja wa Wanawake ambao umewaongoza wanawake katika kudai haki zoa na kuondoa dhuluma wanazofanyiwa na wanaume (ubeti 6).

Kwa sasa, wanawake wanajua kusoma na kuandika (ubeti 9) wengine wamejiunga na jeshi (ubeti 11) na wengine ni viongozi (ubeti wa 10).

Tena wananasisitiza kuwa, wanawake washikilie uzi walio nao. Wasipunguze mkazo bali wakazane ili waufikie ukombozi wa kweli, utakaowapa uhuru wa kuamua mambo yao wenyewe bila kuingiliwa na wanaume (ubeti 14).

**Ukombozi wa Kisiasa**

Katika shairi la “Samaki Mtungoni,” (uk. 19) linaonyesha harakati za watu wa tabaka la chini kuondokana na utumwa wa kutawaliwa na kugandamizwa na mkoloni. Samaki anaashiria watu wa tabaka la chini wanaonyonwa na kugandamizwa; Na mvuvi ni wakoloni au tabaka tawala.

**Ukombozi wa Kifikra**

Katika shairi la “Usiwe Bendera” (uk. 31) linazungumzia juu ya ukombozi wa kifikra na kimawazo.jamii inatahadhariswa isiwe bendera kufuata kila uelekeo wa upepo bali ijitegemee kimawazo.

**Dhamira nyinginezo.**

1. ***Matabaka***

“*Samaki Mtungozi*” linaonyesha matabaka ya aina mbili: tabaka la chini (samaki) na tabaka tawala (mvuvi). Tabaka tawala linanyonya na kulingandamiza tabaka tawaliwa.

Shairi la 14, “*Punda*” waandishi wanaonyesha jinsi tabaka la chini linavyotumikishwa kwa kulinganishwa na punda.

“*Nini Wanagu*” inaonyesha hali ya maisha ilivyongumu na duni kwa tabaka hili la chini ambalo halina kitu, ukilinganisha na tabaka la juu.

Shairi 2,”*mkulima*” linaonyesha jinsi mkulima asivyothaminiwa na tabaka la juu (viongozi).Mpaka inafikia hatua ya kumyima hata huduma muhimu anazo ta kiwa kuzipata.

2. **Uongozi mbaya**

Katika kujadili dhamira hii waandishi wameonyesha kuwa uongozi uliopo hauwajibiki na hivyo ni mbaya.

Shairi la 5 “*Puuzo*” linazungumzia jinsi viongozi wasivyotoa huduma zinazotakiwa maofisini mwao, badala yake husumbua watu wanaohitaji huduma hizo:

2. *Unapokuwa na shida, wao wanakupuuza*

*Watajitia kidada, na kuifanya ajiza,*

*Wajifanya hawajali.*

3. *Ofisini ukifika, wanakuweka baoni*

*Wakati uliofika, wao hawathamini,*

*Wanakwambia subiri.*

Shairi la 4, *“Bahari’* inazungumzia jinsi viongozi wanavyowadhulumu raia haki zao:

7. *Hudai ni haki yao, Mola amewajalia.*

*Kuwadhulumu wenzao, wao wanafurahia,*

*Nao kwa unyonge wao, wadogo wateketea,*

*Bahari ina hatari, wala usiichezee.*

*“Mpaka Lini”* inahusu jinsi viongozi wamejitia uziwi ili wasisikilize matatizo ya raia na wasivyotatua matatizo yao. Viongozi huwakumbatia wasema uongo na wasema kweli hunyanyasika.

Katika shairi la 32. *“Payuka”* wasanii wanaonyesha jinsi viongozi wetu wanavyopayuka ovyo na kuahidi mambo mengi wakiwa jukwaani lakini hawatekelezi yale wanayoongelea. Badala yake,wanabaki kuwaonya na kuwanyanyasa wananchi.

3. **Umuhimu wa kutatua matatizo katika jamii**

Matatizo ya jamii ni mengi mno hasa baada ya kupata uhuru wa bendera. Hivyo ni vyema yashughulikiwe ili kuepusha migongano na majungu ambayo yanaweza kujitokeza na kuchukua sehemu kubwa ya muda wa kujenga nchi yetu.

Shiri la 19. *“Tunzo,”* wasanii wanazungumzia umuhimu wa kutatua matatizo mbalimbali katika jamii yetu ili tuweze kuishi kwa Amani. Matatizo ni kama vile, ongezeko la watu (ubeti 2), kuanguka kwa uchumi (ubeti 3) maradhi mbalimbali (ubeti 3), ubaguzi (ubeti 4) n.k. matatizo hayo yanatatuliwa kwa ushirikaino wa watu wote katika jamii:

6. *Kwenu ninalo tamko, kwa yote jamii nzima fuatizo,*

*Sote tuwe unganiko, kina baba kina mama ni himizo*

*Tuondoshe sawijiko, ili yapate tuhuma matatizo.*

*7. Tuyatende kwa pangiko, ili yasije tukwama mzozo,.*

*Tufanye kimzunguko, vijana watu wazima saidizo,*

*Tulipata ongezeko, la mazao yenye nema na uwezo.*

4. **Mapenzi na ndoa**

Katika kuongelea suala la mapenzi wasanii wamejaribu kugusia hata mapenzi ya watu wawili ambao tayari wako katika ndoa. Katika kujadili suala hili la mapenzi msanii anaanza kumsifia mwanamke ampendaye. Wanasema kuwa mwanamke huyo ni mzuri sana kiasi kwamba kila mtu huvutiwa na uzuri wake. Haya yanadhihirishwa na shairi la Ua (uk. 21 – 22) lisemalo,

3. *Rangi yake ya sanaa, machoni inavutia*

*Ukiliona lang'aa, moyoni lakuingia,*

*Ua sasa limejaa, macho walikodolea.*

Wasanii wanadai kuwa ataendelea kumpatia matunzo ili wengine wasimpatie na hatimaye awe mwenzi wake siku itakapofika. Wasanii wanasema,

7. *Nami sitoliachia, matunzo talipatia,*

*Hadi nitapofikia, mkononi kulitia,*

*Ua sasa limepea, macho walikodolea*

Kutokana na mapenzi ya dhati aliyonayo mshairi huyo, anatoa majonzi yake kwa mwenza wake aliyeishi naye kwa muda wa miaka sita kabla ya kifo kumchukua. Anadai kuwa mpendwa wake huyo alikuwa na tabia nzuri na hakuwa na matatizo yoyote. Haya yote yanadhihirishwa na shairi la Nipate Wapi Mwingine (UK. 32 – 33),

4. *Njiwa ali maridadi, kwa tabia hana shaka,*

*Na hakuwa mkaidi, umwitapo kakufika,*

*Mfanowe kama radi, chini inapoanguka,*

*Njiwa ameshanitoka, nipate wapi mwingine?*

Hata hivyo, washairi hawa anakemea mapenzi yasiyo ya kweli, yaani wanalaani mapenzi yasio ya dhati. Wanasema kuwa kuna baadhi ya wanaume hawana mapenzi ya dhati kwa wake zao. Watu hawa huwaacha wake zao na kuvinjari na vimada. Shairi la kwa nini? (Uk. 1 – 2) linadhihirisha haya

4. *Mke wake, atamwacha,singizini,*

*Atoroke, parakacha, migombani,*

*Kumbe kake, anakochani, mwa jirani,*

*Kwa nini?*

Wasanii wanaendelea kulaumu mapenzi ya ulaghai katika mashairi ya *kuunge* (uk. 25) *utanikumbuka* (uk. 44) na *Kitendawili* (uk. 14). katika shairi la *kuunge* wasanii wanasema kuwa katu hawakubali kushiriki na mtu asiye na msimamo katika mapenzi. Anasema:

2. *Silipandi asilani, gogo lilokauka,*

*Naraduwa kuwa chini, japo nitahangaika,*

*Mnaosema semeni, kisha mutapumzika*.

Wasanii wanasema kuwa hawataki mtu kama huyu ili kuepuka maafa ya kimapenzi ambayo yamewahi kuwapata wengine.

Vilevile, katika shairi la Kitendawili, wasanii wanaendelea kulaumu tabia ya baadhi ya watu ambao hawatuliii katika mapenzi yaani wanafanana na jongoo ambaye hawezi kutulia kwa mfugaji wake.

Pia, katika shairi la "*Utanikumbuka*" mshairi anamwambia mpenzi wake ambaye amemsaliti kuwa atamkumbuka siku za badayae kutokana na ukweli kuwa msanii alishamtendea mambo mengi sana ambaye aliyemlaghai hataweza kumtendea. Anasema.

3.*Umeona bora kitu,ukasahau ya nyuma,*
*Umetupa mbali utu, na zote zangu huruma,*

*Kwako kutokaa katu, ipo siku utakwama,*

*Utaumiza uwatu, iwe na yako hatima*.

**Kupiga vita unyonyaji**

Wasanii wa diwani hii wanaosha kuwa katika jamii yetu kuna unyonyaji wa hali ya juu kama ilivyokuwa enzi za ukoloni. Katika shairi la *Bahari* (uk 6 – 7) linaonesha waziwazi jinsi viongozi wanavyowanyonya watawaliwa. Shairi hili linasema.

6. *Suala wajiuliza, katika jamii zao,*

*Wanaona miiujiza, wanayotenda wenzao,*

*Wakubwa wanajiweza, kula wadogo zao,*

*Bahari ina hatari wala usich*ezee.

Shairi hili linaendelea kudai kuwa kitendo cha viongozi kuwanyonya wazalishaji mali mumehalalishwa na viongozi wenyewe. Viongozi wanaona kuwa kunyonya wananchi wakawaida ni haki ya msingi waliyopewa na mwenyezi Mungu. Kitendo ambacho washairi wanakataa. Washairi wanaonesha unyonyaji wa aina hii katika shairi la "*Samaki Mtungoni*" (Uk. 19 – 20) .katika shairi hili tunaona samaki (watawaliwa) wakinyanyaswa, kuuliwa na kunyonywa na mvuvi (mkoloni au mtawala).Hali hii imesababisha kutoweka kwa utu wa samaki (watawaliwa) kama asemavyo mshairi.

5. *Haki yao mepotea, na heshima kuondoka,*

*Mebaki waninginia, mtungoni mepangika,*

*Bwana amechachama, nyumba kwenda kupika,*

*Leo wako mtongoni, huzuni inawakumba.*

Washairi wanadai kuwa, pamoja na kuondoa ukoloni nchini, bado hali za wa nanchi wa kawaida ni mbaya sana. Haya yote tunayopata katika shairi la "*Hali Halsi*" uk. 5) ambalo linaonesha hali tete kwa mwananchi wa kawaid

**4.** *Nuru tuliieneza, giza kulitokomeza,*

*Wote wasiojiweza, hali kuzifananiza,*

*Mshumaa unawaka, giza mbona limezidi?*

Kwa vile hali za wananchi zinazidi kuwa mbaya tangu enzi za mkoloni hadi leo, washairi wanawataka wanajamii wafanye mapinduzi ya kweli dhidi ya unyonyaji na ukoloni wa aina yoyote. Haya yote yanapatikana katika mshairi ya *Sokomoko baharini* (uk. 63 – 64) *Haki* (uk 47 – 48) na *Payuka* (uk 50 – 52). Mashairi haya yote yanatoa mwamko wa kisiasa, mwamko wa kuleta mabadiliko katika jamii ili haki ipatikana".Katika shairi la *Sokomoko* Baharini, mshairi anakusanya vijana na wanyonywaji ili waungane kwa pamoja na kwa lengo la kuleta mabadiliko. Anasema,

10. *Hapa mbele sirudi tena, nia mimi nimechukiwa,*

*Nenda kusanya vijana, hali wanaoijuwa,*

*Matumbo yalokunjana, wa tayari kuambiwa,*

*Mashua kuiokoa, mbio watakimbia.*

Shairi la Haki linaendelea kuamsha mioyo ya wanyonge ili wapambane dhidi ya unyonyaji na ukoloni, Shairi hili linawataka wanajamii watafute haki yao ambayo imetekwa na watawala wao. Shairi linasema

*8. Haki husimama, kwa Viumbe sisi, tuvyojaaliwa,*

*Na huna ulimi, kuweza tukasi, tukageukiwa,*

*Zama za uchumi, zishashika kasi, nguvu zishapewa,*

*Haki wauliwa*

Mashairi hayo yanafanana na utenzi wa Payuka unaowataka wanajamii wamke na kupigania haki zao ambazo zimevizwa na baadhi ya watu kama vile watawala wao au wakoloni. Utenzi huu unasema,

16. *Amkeni amkeni,*

*Msilale asilani,*

*Vibaya mnaumia*

**6.Maadili mema na maonyo katika maisha.**

Katika diwani hii, wasanii wamejaribu kuwaadili na kuwaonya wanajamii ili waweze kuishi maisha bora. Katika kuzungumzia suala hili, wasanii amegusia masuala yafuatayo:

Moja, matumizi mazuri ya fedha. Wasanii wanaitaka jamii kutumia vizuri pesa inazozipata. Wasanii wanasema kuwa iwapo jamii itatumia pesa zake vibaya itakuja kujuta siku za baadaye. Wanajamii wanatakiwa kutunza pesa vizuri ili kujenga maisha yao ya baadaye. Haya tunayapata katika utenzi wa Israfu (u. 17 – 18).

*6. Huu ni wakati wako,*

*Kujenga kesho yako,*

*Kuepuka chokochoko,*

*Za hao adui zako,*

*Mwenzangu nakuisia, Israfu haifai.*

Hivyo, tutumie vizuri fedha zetu ili kuepukana na majonzi au majuto tunayoweza kuyapata siku za baadaye.

Mbili, umuhimu wa kusema ukweli, Wasanii wanawataka wanajamii kusema ukweli daima. Katika shairi la *Ulimi* (uk. 41) wasanii wanaziasa ndimi zao tusiropoke bali ziseme ukweli tupu. Hali hii itasaidia kulinda heshima yao katika jamii. Shairi hili linasema.

3. *Usiropokeropoke, kwa wenzio kwanza sema,*

*Usipachikepachike, maneno yasiyo mema,*

*Useme wanufaike, kwa kauli yako njema.*

*Ewe ulimi sikia!*

Wasanii wanaendelea kudai kuwa kwa vile ulimwengu umejaa shida, lakini shida hizo zisiwe chanzo cha kusema uongo.Hayo tunayapata katika shairi la *Ulimwengu* (uk. 42 – 43) ubeti wa 3.

*Shida dhiki ni halali, haramu ikijibari,*

*Ni bora kutoa kweli, uongo uso wa nari,*

*Ni vyema kutakabali dhila na zake hatari,*

*Ulimwengu!*

Ukweli husaidia kujenga jamii iliyo bora, husaidia kuondoa wale wote wenye nia ya kubaguana, hasa katika masuala ya dini, rangi na hata kabila. Haya yote tunayapata katika shairi la *Pasua Uwape Ukweli*. (uk 46).

Nalo shairi la *"Mwabwaja Mwasema Nini"*? (uk. 61 – 62) linadhihirisha dhana ya kusema ukweli kwa kuwataka watu waseme ukweli kwa vitendo. Washairi wanawataka waandishi waseme ukweli kuhusu hali halisi ya maisha ya watu wa kawaida. Vilevile, anawataka waandishi watekeleze kwa vitendo wanayoyasema. Kusema ukweli na kutenda mambo yasemwayo itasaidia sana katika kujenga jamii iliyo bora.

Tatu, umuhimu wa kutenda mema. Wasanii, wanawausia wana jamii kutenda mema kwani mtu yeyote atendewaye mema anastahili kulipa kwa wema aliotendewa, hata kwa kusema ahsante. Na yeyote atendaye mema atalipwa kwa njia yoyote ile,

ikiwemo ya kiroho. Katika shairi la *“Hisani Hulipwa”* (uk. 45) tunaambiwa kuwa,

3. *Akufichiae,siri, zinonuka,*

*Na akurambae, akakusafisha,*

*Akutafutae, unapopotea,*

*Hisani hulipwa.*

Nne ,ni kuachana na anasa za dunia.Wasanii wanawaasa wanajamii kuachana na tamaa za kimaisha. Shairi la *Siharakie Maisha* (uk 11 - 12) linawaasa wanafunzi kuachana na papara za kimaisha na badala yake wasome kwani maisha ni kama kupanda mnazi ambapo mpandaji sharti aanzie shinani kama atakiwavyo mwanafunzi kutong’ang’ania mambo ya anasa za dunia kama vile umalaya, ulevi, uchoyo, wizi n.k. bali ajijengee ya kesho, yaani asome kwa bidii ili apate elimu bora ambayo ndio msingi wake wa maisha ya baadaye. Shairi hili linasema,

2. *Ubado ni mwanafunzi,*

*Usingiwe na simanzi,*

*Ruka vikwazo ja panzi,*

*Ipambe yako enzi,*

*Maisha safari ndefu, kutembea usichoke.*

*3. Somo babo endelea,*

*Sicheze pata potea,*

*Muda wako ukimea,*

*Maisha kufurahia,*

*Usiache kutegua, kwa kutegemea tega*

Wasanii wanaendelea kudai kuwa raha za dunia hazina thamani kwani waliowahi kupata raha sasa wanajuta. Wanaonesha kuwa watu hao pindi wapatapo pesa huwasahau wengine kwa kuwaona kama hawafai huyafakamia maisha kabla dunia haijawafundisha. Haya yote tunayapata katika shairi la *Raha* (uk – 24) ambapo mponda raha anajuta,

4. *Leo raha naiwacha, atakaye aje kwetu,*

*Nami nataka kututa, nitulie kama watu,*

*Nimechoka kuzorota, nakubakia sukutu,*

*Chukueni mtumie.*

**7.Umuhimu wa kutumia pesa vizuri.**

Matumizi mabaya ya fedha ni kujitia kwenye umasikini, na mali bila daftari hupotea bila kujua. Katia diwani hii, waandishi wanaonyesha au wanasisitiza juu ya matumizi mazuri ya pesa.

Katika shairi la 11, "*Israfu*" wasanii wanaionya jamii juu ya matumizi mabaya ya fedha zinazopatikana:

1. *Mali ulijichumia,*
*Ni yako nakubalia,*

*Lakini kuangalia,*

*Vipi unaitumia,*

*Mwenzangu nakuusia Israfu haifai.*

Wasanii wanaonyesha kuwa matumizi mabaya ya fedha husababisha umasikini kwa muhusika na umaskini husababisha akimbiwe na watu wote hata marafiki zake.

**8. Athari ya sukari mwilini**

Sukari ni kitu cha muhimu sana katika mwili wa binadamu. Lakini sukari hiyohiyo ikizidi inaleta madhara mbalimbali mwilini.

Katika shairi la 34 *“Sukari”* Wasanii wanaonyesha madhara mbalimbali yatokanayo na sukari kuzidi katika mwili wa mwanadamu. Athari hizo ni kama vile meno kung’oka (ubeti 2)

Pia sukari huleta safura mwilini na ugonjwa wa kisukari.

**Ujumbe (Maadili mabalimbali)**

1. Kuinua uchumi wa nchi ni jambo la muhimu sana, ili tuweze kuondokana na utegemezi wa kutegemea misaada toka nje.

2. Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wetu, hivyo ni lazima tukiimarishe na Mkulima lazima athaminiwe.

3.Ukombozi wa mwanamke ni muhimu sana, kwani mwanamke akikombolewa atazijua na kudai haki zake kwa ujasiri,na atakuwa msaada mkubwa zaidi kwa jamii.

4. Ni muhimu kutatua matatizo mbalimbali yanayoikabili jamii yetu ili tuweze kuishi kwa Amani na utulivu.

5. Ni vizuri kuwa na maadili yaletayo kutendeana mema katika jamii, kwani kufanya hivyo tutajenga jamii yenye haki na usawa.

6. Ni vizuri kuwa na matumizi mazuri ya pesa zetu ili kuukwepa umasikini.

**Falsafa (Mwelekeo)ya Waandishi**

Waandishi wanaamini kuwa tukisisitiza Kilimo na kumthamini mkulima tutainua uchumi wetu kwa kiasi kikubwa. Pia wanaitaka jamii ifuate misingi ya haki na usawa katika maisha. Wanatetea haki na usawa kwa watu wote.

**Msimamo wa Wandishi**

Waandishi wana msimamo wa kimapinduzi kwani wamejadili masuala mbalimbali ambayo ni nyeti kwa jamii yetu na kukemea uonevu kwa ujumla.

**Fani**

**Muundo**

Miundo changamano umetumika. Kuna muundo wa tathlitha (mistari mitatu)-shairi la 5 *“Puuzo”* 13 *“Ua,”* na 32 *“Payuka”*: tarbia (mistari minne) – shairi la 4 *“Bahari”*/ 2 *“Mkulima”* 20 *“Usiwe Bendera”* 27 *“Utanikumbuka”* na sabilia au takhmisa (mistri mitano na kuendela) shairi la 7 *“Siharakishe Maisha"/*“11 *Israfu*” na 14 *“Punda”*.

- **Mtindo**

Waandishi wametumia mtindo unaofuata kanuni za ushairi wa kimapokea na urari wa vina na mizani kwa mshairi mengi, mfano shairi la 2,3,4,6,8,9,10,12, n.k. Pia wametumia mtindo unaofuata ushairi wa kisiasa kwa mfano katika shairi la 19.

**Matumizi ya Lugha.**

Lugha waliyoitumia waandishi ni ya kishairi yenye methali, tamadhali za semi, mbinu nyingine za kisanaa na taswira mbalimbali.

**Methali**

- *Subira yavuta heri (shairi la 7 ubeti 8)*
- *Aisifuye mvua kaloa mwilini mwake (shairi la 23 ubeti 12)*
- *Fahari wapiganapo nyasi ndizo huonewa (shairi la 37 ubeti 7)*

- **Misemo:**
- *Siharakie maisha (shairi la 7).*
- *Kusumbukia kichaa (shairi la 23).*
- *Sokomoko baharini (shairi la 37).*

- **Tamathali za semi**
- **Tushibiha**

*Ubaguzi umezama kama nguzo (shairi la 19 ubeti 4).*

*Maisha ni kama njia (shairi la 24).*

- **Tashihisi**.

-Katika shairi la "*Samaki Mtungoni*" Samaki wamepewa uwezo wa kibinadamu.

-Katika shairi la "*Nipate Wapi Mwingine*". Hapa njiwa amepewa uhai kama mpenzi aliyefariki.

- **Mbinu Nyingine za Kisanaa.**
- **Tashtiti** – katika shairi la "*Mwabaja Mwasema Nini*?" mfano– *Nasikia mnatunga, mwatungani washairi?*

- **Tanakali sauti** – mfano katika shairi la *"Kwa Nini*"! – neno parakacha, shairi la *"Mkulima*" neno *kokoriko* n.k.

- **Takriri** – kuna matumizi kurudiarudia maneno katika mashairi ya *"Kifungo*" – *"Adui*" *"Majonzi*" n.k

**Ujenzi wa Taswira**

Njiwa – Mpenzi -katika shairi la *"Nipate Wapi Mwingine?'*

Samaki – Watu wa tabaka la chini

Mvuvi – Watu wa tabaka tawala – shairi la *"Samaki Mtungoni*"

Punda – Tabaka la chini linalonyonywa na kuagandamizwa

Ua – Mwanamke au msichana.

- **Jina la Kitabu**

Jina la diwani hii , *Malenga Wapya* linaendana na makusudio ya watunzi. Neno malenga lina maana ya mshairi na neno wapya lina maana ya watu au vitu ambao au ambavyo ni wa / vya kisasa. Hivyo Malenga Wapya lina maana ya washairi wapya. Hali hii inatufanya tuamini kuwa jina Malenga Wapya linaendana na hali halisi ya mambo yaliyo ndani ya diwani hii kwa kuzingatia nyanja kuu, mbili:

Kwanza katika utangulizi tunaambiwa kuwa *Malenga Wapya* ni mkusanyiko wa mashairi 37 yaliyotungwa na wanafunzi mbalimbai katika kipingi cha uwanafunzi wao (uk. 5) kwa maneno mengine *Malenga Wapya* lina maana ya washairi wapya au washairi vijana (wachanga) walioamua kuingia katika uwanja wa ushairi.

Pili, *malenga wapya* lina maana ya washairi wapya wanaotumia mitindo mipya ambayo imo ndani ya diwani hii. Kusema ukweli diwani hii ina upya fulani, hasa kwa upande wa mtindo. Upya huu ni nadra kuupata katika diwani nyingine, ingawa mtindo uliotumika wa kimapokeo peke yake. Hata hivyo mtindo huu umeibua mshairi yenye mitindo tofautitofauti. Jambo hili linaifanya diwani hii ionekane mpya au ionekane tofauti na diwani tulizowahi kusoma. Upya huu kimtindo, unaweza kuelezwa kama ifuatavyo:

Diwani hii ina baadhi ya mashairi yenye vina viwili vya kati tofauti na diwani zilizo nyingi, ambazo tumewahi kusoma. Kwa mfano, katika shairi la "*Tunzo*" (uk. 20) tunaona hali hii,

8. *Tulete mabadiliko, huku nia iwe njema, tangu mwenzo,*

*Matumaini yaweko, tukijachagua mema, kimawazo,*

*Tena aliadi, iweko, kwa nchi yetu nzima, endelezo.*

Tukichunguza shairi hili tutaona kuwa kuna vina vya kati vya aina mbili, ambavyo ni "ko" na "ma" kama vinavyoonekana ndani ya shairi. Shairi jingine lenye vina vinavyofanana na hilo ni "*Haki*" (uk 47 – 48).

Vilevile, kuna upya mwingine katika utumiaji wa mizani. Baadhi ya mashairi kama vile "*Usiwe Bendera* (uk 31) na *Hisani Hulipwa*" (uk. 45) yana mizani 12 badala ya 16 au 8 kama ilivyozoeleka katika mashairi ya kawaida na tenzi zenye kufuata kanuni za kimapokeao. Shairi la Usiwe Bendera linathibisha haya,

*1.Kaa ufikiri, ni tokueleza,*

*Haya udhukiri, ukiyachunguza,*

*Hujawa mazuri, hwenda yakatunza.*

Ubeti huu una mizani 12, kwa maana kuwa kila nusu mstari una mizani 6 Mwisho, washairi hawa wametumia mtindo wa tenzi ambao pia una upya fulani. Upya huo unaonekana katika mstari wa mwisho ambao una mizani nyingi tofauti na mistari mingine ya tenzi ambayo kwa kawaida huwa na mizani 8. Lakini mstari wa mwisho una mizani 16. Hali hii inajionesha katika tenzi za *Siharakishe Maisha*. (Uk 11 – 2) *Israfu* (uk. 17 – 8). Mfano mmojawapo ni ubeti wa 2 wa utenzi wa *Sibarikie Maisha*.

*Ubado ni mwanafunzi*

*Usingiwe na simanzi*

*Ruka vikwazo ja panzi*

*Uipambe yako enzi,*

*Maisha safari ndefu, kutembea usichoke.*

Tunaweza kusema kuwa ingawa hakuna upya wowote kimaudhui lakini kifani kuna upya mwingi. Upya huu, ikiwa ni pamoja na uchanga wa watunzi au washairi ndio unaotufanya tusema kuwa jina la diwani *Malenga Wapya* linasadifu yale yaliyomo ndani yake

- **Kufaulu kwa Mwandishi.**

**Kimaudhui**

-Mwandishi amefanikiwa kutuonyesha dhamira mbalimbali ambazo zinaonyesha maisha yetu kabla ya uhuru na baada ya uhuru mpaka sasa.

-Waandishi wameonyesha mvutano kati ya tabaka la chini na tabaka la juu (uongozi mbaya, n.k)

-Wameshauri jamii kuwa na maadili mema.

-Waandishi wameonyesha matatizo mbalimbali yanayoikabili nchi yetu.

**Kifani**

-Wamefanikiwa kutumia lugha ya kishairi, nyepesi na yenye taswira.

- Kimuundo mashairi yao yanajitosheleza.

**Kutofauulu kwa Waandishi**

**Kimaudhui**

-Waandishi katika mashairi ya *"Mkulima"* na *"Adui"* wameonyesha ukasuku walionao kwani tangu zamani za kale hadi leo hii watu wamekuwa wakilima lakini bado hali zao ni duni.

-Wamerudiarudia maneno yanayoimbwa majukwaani kuhusu viongozi badala ya kutuonyesha njia za kisayansi nakiteknolojia za kuondokana na matatizo ya kiuchumi, kifikra na kijamii.,

-Aidha wasanii wamekuwa na mtazamo potofu na dhaifu katika kutoa baadhi ya maadili mfano: shairi la *"Hisani Hulipwa"*

**Kifani**

Diwani hii imetumia lugha rahisi kiasi kwamba hamfikirikishi msomaji.